# URITHI WA KANISA

# MAFUNDISHO YA HISTORIA YA KANISA

**Hutoa mwangaza juu ya Mada muhimu zenye kuwavutia vijana**

Kimetayarishwa na Idara ya Vijana ya Makao Makuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato
Washington D.C., 20012

(Church Heritages)
A Course in Church History

Kimetafsiriwa na:-
Bevin E.H. Ngenzi
na kupigwa Chapa na Janet Busee
Kwa ajili ya Idara ya Vijana
Tanzania Union

## YALIYOMO

**Utanguzi** i
Mwongozo kwa Mwalimu ii

**SEHEMU YA KWANZA**
Kanisa la Kristo katika Vizazi Vyote 1

**SEHEMU YA PILI**
Wachukuzi wa Ujumbe wa Marejeo - 1755 - 1843 9

**SEHEMU YA TATU**
Mwanzo wa Kanisa la Masalio 1844 - 1852 18

**SEHEMU YA NNE**
Kuundwa kwa Kanisa la Masalio 1853 - 1863 34

**SEHEMU YA TANO**
Kupanuka na matengenezo 1864 - 1873 36

**SEHEMU YA SITA**
Njozi kwa ajili ya ulimwengu mzima 1874 - 1878 39

**SEHEMU YA SABA**
Maendeleo muhimu pamoja na mapungufu 1879 - 1904 40

**SEHEMU YA NANE**
Kukua na kupanuka kwa Injili 1905 – 1023 44

**SEHEMU YA TISA**
Mafanikio dhidi ya vikwazo 1924 – 1946 47

**SEHEMU YA KUMI**
Kukua na mshikamano 1947 – 1959 50

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**
Kumaliza kazi ya Injili - 1960 52

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**
Idara mbali mbali za Kanisa 57

**SEHEMU YA KUMI NA TATU**
Divisheni mbali mbali za Kanisa Ulimwenguni 63

**SEHEMU YA KUMI NA NNE**
Marais wa Jenero Konferensi 66

**SEHEMU YA KUMI NA TANO**
Mwamko mkuu kuhusu Marejeo 1755 - 19-- 74

## UTANGULIZI:

**Mafundisho ya ngazi mbili katika kitabu kimoja**.

Kitabu hiki hutoa mafundisho juu ya Historia ya Kanisa katika ngazi mbili kuu, yaani yale yanayohusu Kozi ya Kiongozi Mkuu pamoja na yale yanayohusu wale waliochukua Kozi ya Kiongozi Mwadventista, pamoja na hayo pia masomo yanayohitajika kwa ukamilishaji wa hitaji linalohusu historia ya kanisa katika darasa la Msimamizi.

Wale wanaochukua Kozi za **Kiongozi Mkuu** pamoja na **Kiongozi Mwadventista** wanahitajika kujifunza kitabu hiki chote bila kusaza hata sehemu moja. Katika kitabu hiki aya zote zilizoandikwa kwa italiki (italics) na kuwekewa alama ya nyota (*) zina umuhimu wa pekee hivyo zinapaswa kukaririwa.

Wale wanaojifunza darasa la Msimamizi wanapaswa kujifunza sehemu ya 2 hadi sehemu ya 13, lakini hawapaswi kujifunza kwa undani sana kama ambavyo inawapasa wale wanaochukua Kozi ya Kiongozi Mkuu. Hata hivyo, wale wanaosoma katika darasa hilo ni lazima wakariri mambo yote muhimu yaliyoonyeshwa kwa kuwekewa alama ya nyota (*).

**Vitabu vya rejea**

Japokuwa kitabu hiki kinayo mafundisho yote yanayotakiwa kwa mwanafunzi ili kuweza kufaulu mtihani, lakini wapo baadhi ya wanafunzi ambao labda watapenda kusoma wenyewe katika vitabu vya rejea. Orodha yake imetolewa hapa chini.

Kila mwalimu ni lazima apate angalao kitabu kimoja cha rejea kinachofundisha historia ya kanisa na akisome ili uwe msingi wa mafanikio ya mafundisho yake kwa darasa.


“The Great Advent Movement” -Emma Howell Cooper
“Light Bearers the Remnant” -Richard Schwarz
“Origin and History of Seventh-day Adventist (4 Vol.) -Arthur W. Spalding
“Tell it to the World” -Mervyn Madwell
“Movement of Destiny -Le Roy Edwin Froom
“Seventh-day Adventist Encyclopedia Revised Edition

# MWONGOZO KWA MWALIMU

Mwalimu yeyote anayefundisha historia ya Kanisa ni lazima yeye mwenyewe ajifunze na kuielewa vema kabla hajadiriki kuanza kufundisha kozi hii yenye umuhimu mkubwa. Inashauriwa kwamba ili kuleta mafanikio katika mafundisho haya wale wanaojifunza historia ya kanisa ili kukamilisha matakwa ya msingi katika madarasa ya chini watenganishwe na wale wanaojifunza ili kukamilisha takwa hilo kwa madarasa ya juu. Wawekwe katika makundi yaliyo tofauti kabisa.

Katika somo la utangulizi, mwalimu anapaswa kutoa mtazamo wa jumla kuhusu historia ya kanisa, ili wanadarasa wanapojifunza waweze kuhusianisha mambo mbali mbali wanayoelezwa na historia nzima ya kanisa.

Walimu watatakiwa kutengeneza majedwali yanayoonyesha vipindi mbalimbali katika historia ya kanisa na vile vile watatakiwa kuwaonyesha wanafunzi ramani ili waweze kufahamu sehemu mbali mbali ambazo hazifahamiki kwao. Darasa la kujifunza historia ya kanisa linapaswa kuwa darasa lenye kuvutia na kuwapendeza wanafunzi. Linapaswa kuwa ni mahali ambapo wanafunzi hawapati habari tu bali pia hupata uvuvio wa Roho wa Mungu. Mwalimu asijaribu kusoma tu kitabu mbele ya wanadarasa na kuwahimiza "Zingatia hili" Ifanye historia hii kuwa jambo halisi lililo hai na hivyo utaamsha usikivu na hamu ya wanafunzi kuendelea kukusikiliza na kujifunza.

## MWONGOZO KWA WANAFUNZI

Wale wote wanaojifunza mafundisho ya historia ya kanisa wanapaswa kwanza kujifunza yaliyomo katika muhtasari wake ili waweze kupata picha kamili kuhusu historia ya kanisa.

Kwa kujifunza kitabu hiki, wanafunzi wataweza kufahamu kwamba historia ya kanisa kama ilivyoandikwa katika kitabu hiki imepangwa kwa mpango wa matukio kwa mfuatano wa miaka na kwamba kila sehemu iliyoonyeshwa katika kitabu hiki hushughulikia matukio yaliyotokea katika miaka fulani maalumu. Muhtasari wa jumla unaoonyesha matukio mwaka baada ya mwaka umeonyeshwa katika sehemu ya 15 ambapo matukio yote yameorodheshwa kwa mfuatano kama yalivyotokea.

## MWONGOZO KUHUSU DARASA LA MSIMAMIZI

Masomo yaliyomo katika sehemu ya kwanza (1) na ile ya kumi na nne (14) hayahusiki kabisa katika ufundishaji mtaala wa darasa la Msimamizi. Masomo hayo yatasomwa au kufundishwa wakati wahusika watakapokuwa wanachukua Kozi ya Kiongozi Mkuu na ile ya Kiongozi Mwadventista.

**Divisheni**: Wakati wa kujifunza sehemu ya historia ya Kanisa kuhusu Divisheni yako, utatakiwa kujifunza kwa undani mambo yafuatayo: Namna Injili au Kanisa lilivyoanzishwa katika nchi yako pamoja na namna lilivyoanzishwa katika nchi mojawapo utakayoichagua miongoni mwa nchi zinazounda divisheni yako na wala siyo vinginevyo.

**Sehemu ya 12:** Chagua Idara tano miongoni mwa Idara za Kanisa na ujifunze historia yake, kazi, pamoja na wakurugenzi wa Makao Makuu ya Kanisa ulimwenguni (General Conference, Divisheni, Union, Konference au Field/Misheni)

**Sehemu ya 13:** Chagua Divisheni tano miongoni ya Divisheni za ulimwengu ikiwemo Divisheni ambamo kanisa lako lipo na ujifunze mambo muhimu yenye kuleta mvuto kama nchi zipi huunda divisheni hizo, idadi ya washiriki pamoja na shughuli zenye kufanikiwa sana katika maeneo hayo.

**Sehemu ya 15:** Ziweke alama tarehe/miaka ambayo unaiona kuwa ina umuhimu sana kwako. Mambo yote ambayo yamewekewa katika chumba ( ) na mengine kupigiwa mstari katika sehemu mbali mbali za kitabu hiki, yanapaswa kuzingatiwa sana. Sehemu hii ya (15) pia hutoa muhtasari wa matukio yote muhimu ya historia ya Kanisa kwa mpangilio kufuata miaka.

**MWONGOZO WA KOZI HII KWA WALE WANAOCHUKUA MASOMO YA KIONGOZI MKUU NA KIONGOZI MWADVENTISTA**

1. Soma kitabu hiki na kukimaliza sehemu kwa sehemu na uweze kuzingatia mambo muhimu kuhusu watu na mahali katika sehemu zote zilizoandikwa kwa italiki.

2. Wakati unaposoma kitabu hiki kila unapokuta miaka iliyopigiwa mstari au kuandikwa kwa italiki, tia alama katika muhtasari wa matukio kwa mpangilio wa miaka yalipotokea ambayo ipo katika sehemu ya 15 ya kitabu hiki.

3. Utakapokuwa unajifunza sehemu mbali mbali za historia ya Kanisa katika divisheni yako, unatakiwa kujifunza kwa undani mambo yafuatayo tu; namna kazi ya Injili ilivyoanzishwa katika nchi yako pamoja na nchi nyingine mojawapo utakayoichagua miongoni mwa nchi zinazounda divisheni yako. (Wasiliana na Mkurugenzi wako wa Vijana wa Field/Conference ili iwapo kuna rejea zozote zenye habari kuhusu mambo yanayotakiwa kujifunzwa katika sehemu hiyo ya ulimwengu uweze kuyapata kutoka kwake).

4. Wale wote waliopo katika kozi ya Kiongozi Mkuu ni lazima waelewe vizuri na kuweza kutoa habari zozote kuhusu idara zote, divisheni na baadhi ya waliopata kuwa viongozi Wakuu wa kanisa la Waadventista wa Sabato ulimwenguni. (General Conference Presidents)

Mitihani ya darasa la Msimamizi pamoja na ile ya kuhitimu Kozi za Kiongozi Mkuu na Kiongozi Mwadventista ni mitihani ya ngazi mbili tofauti nayo hutofautiana kabisa katika viwango vya mambo yanayoulizwa na upana wa majibu yanayopaswa kutolewa. Vile vile, katika Kozi ya Kiongozi Mkuu, mtahiniwa kuhesabiwa kwamba amefaulu iwapo atapata ala 75/100 (sabini na tano kwa mia) au zaidi, wakati katika darasa la Msimamizi, mtahiniwa huhesabiwa amefaulu iwapo atapata alama 70/100 (Sabini kwa mia) au zaidi. Katika sehemu inayohitaji majibu ndiyo au hapana. Kweli au si kweli watahiniwa wa Kozi za Kiongozi Mkuu na Kiongozi mwadventista hupoteza alama za ziada kwa kila jibu lisilo sahihi. Hii ina maana iwapo jibu sahihi lililokuwa Ndiyo na Mtahiniwa akajibu Hapana. Mtahiniwa huyo pamoja na kwamba

amekosa hastahili kupata alama yeyote atapata adhabu ya kupunguziwa alama ambazo amekwisha zipata, wakati katika darasa la Msimamizi. Mtahiniwa akikosea hatapunguziwa alama yeyote ya ziada.
Mitihani hii yote hutayarishwa na Idara ya vijana ya Kanisa la Waadventista Wa Sabato Ulimwenguni (General Conference Youth Department) na kutumwa katika Konferensi au Field. Field/Konferensi zote ambazo zimenunua kitabu hiki cha **Urithi Wa Kanisa** yaani Mafundisho kuhusu Historia ya kanisa wanayo haki ya kuletewa nakala ya Mitihani hiyo bure baada ya kumaliza mafundisho haya.

Kutakuwa na mitihani ya namna mbili tofauti kama jaribio la kufaulu katika mafundisho haya kuhusu historia ya Kanisa kwa darasa la Msimamizi, wakati watahiniwa wa kozi za Kiongozi Mkuu na Kiongozi Mwanadventista watafanya mitihani miwili pia ili kumaliza Kozi hii. Mitihani hii yote itafanywa kwa kuzingatia masharti yote ya mitihani na baadaye kupelekwa field au Konferensi katika Idara ya vijana ambapo itasahihishwa na kuwekewa alama.

Makaratasi yote yaliyotumika katika mtihani hayatarudiswa kwa watahiniwa hii ikiwa ni pamoja na makaratasi ya maswali yaliyotumika katika mitihani; hairuhusiwi kutumia maswali haya kama nyenzo ya kufundishia au kujifunzia.

Kutakuwa na mitihani ya aina mbili kwa watahiniwa wa ngazi zote mbili yaani wale wa Madarasa yaa chini pamoja na wale wanaochukua Kozi ya Kiongozi Mkuu na Kiongozi Mwadventista katika mafundisho haya ya historia ya Kanisa. Mitihani yote iko katika mfumo unaohitaji majibu mafupi na mara nyingi huwa imegawanyika katika sehemu mbali mbali kama ifuatavyo:

**Mtihani wa historia ya Kanisa – Kwa watahiniwa wa Kozi ya Kiongozi Mkuu na Kiongozi Mwadventista.**

**Sehemu ya 1:** Ndiyo au Hapana Mfano:…. Hakuna mabadiliko makubwa ambayo yamekwishafanyika katika Muundo wa Kanisa la Waadventista Wasabato tangu zilipotolewa zile makala 9 (tisa) za awali (Ndiyo/Hapana)

**Sehemu ya 2:** Chagua jibu lililo sahihi: Mfano…. Mhubiri aliyetumwa kuhubiri kusini mwa marekani ambako Wahindi hukaa alikuwa (a) Pedro Kalbermatter, (b) F.H. Westphal (c) Abram La Rue, (d) F.A. Stahi
( )

**Sehemu ya 3:** Jaza maneno katika nafasi zilizowazi Mfano: Idara ya Walei ilianza na chama kilichojulikana kama………………………………………………………

**Sehemu 4:** Kuhusianisha maneno au maelezo Mfano: Wamishonari na sehemu walizofanyia kazi; vitabu na watunzi wake, taasisi na anwani zao, tarehe na matukio muhimu.

**Mtihani wa historia ya Kanisa** - Kwa darasa la Msimamizi:

**Sehemu ya 1:** Kuhusianisha Maneno au Maelezo Mfano: Taasisi na anuani zao; tarehe na matukio wamisionari na maeneo waliyofanyia kazi.

**Sehemu ya 2:** chagua jibu lililo sahihi zaidi: Mfano: Katibu Mkuu wa kwanza Kanisa la Waadventista wa Sabato Ulimwenguni (General Conference) alikuwa (a) James

White (b) Uriah Smith (c) W.S. Walker

( )

**Sehemu ya 3:** Mambo ya jumla Mfano: Divisheni zilizopo ulimwenguni, Idara za Kanisa, uchapaji umishonari, Wakurugenzi wa vijana, shughuli za vijana wa Kiadventista n.k.

**Sehemu ya 4:** Kweli au si kweli Mfano: Wengi wa Waadventista wa sabato walioishi mwaka 1844 waliitunza sabato ya siku ya saba (Kweli/Si kweli).

## KANISA LA KRISTO KATIKA VIZAZI VYOTE

a) **Kaanisa katika Nyakati za Agano la Kale**

Kanisa la ungu huanzia Edeni ile ya kwanza na kuendelea kwa wakati wote hadi Edeni Mpya inayotarajiwa. Wale wote ambao wamemtii Mungu wamekuwa wakiitwwa kwa majina mbali mbali kwa mfano "Wana na Binti za Mungu" "Wazao wa Ibrahimu: "Wana wa Israeli" au "Wakristo" bila kujali jina gani wanaitwa. Lakini wote wanao msingi mmoja juu ya mafundisho makuu ya Imani.

**Kanisa la Agano la kale liliipokea sheria ya Mungu kama Kanuni pekee ya maisha.** Sheria ya Amri Kumi haibadiliki kwa sababu ni Ufunuo wa tabia ya Mungu wa milele asiyebadilika ambaye pia ndiye Mungu wa vyote. Watu wa Mungu walikuwa wakizitunza amri kumi muda mrefu kabla ya Musa kupewa na Mungu pale katika Mlima wa Sinai. Mungu alisema "Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu akayahifadhi maagizo yangu na amri zangu, na hukumu zangu na sheria zangu" (Mwanzo 26:5)

**Mungu amekuwa na njia moja tu ya wokovu, na kiwango cha aina moja katika vizazi vyote.** Tunasoma katika Zaburi 105:5-11 kwamba alifanya agano na Ibrahimu, Isaka, Yakobo na wana wa Israeli alifanya nao agano la milele. Mungu alitangaza wazi kwamba agano alililofanya lilikuwa ni la milele. "Neno lile aliloviamuru vizazi elfu". Si sahihi hata kidogo kusema kwamba watu walioishi nyakati za Agano la kale walikuwa chini ya Sheria na kwamba wale walioishi katika zamani za Agano Jipya walikuwa chini ya Neema. Mungu amedumisha siku zote uhusiano kati ya sheria ya Neema. Tunaokolewa kwa Neema ya Yesu Kristo na kwamba tunapoupokea wokovu huo na kuingia katika uhusiano wa kuokolewa na Kristo. Tunabadilishwa na kufanyizwa tufurahie kutenda mapenzi yake.

**Washiriki wa Kanisa la wakati wa Agano la Kale walithibitisha imani yao kuhusu mpango wa** wokovu kwa tendo la kutoa dhabihu: Kwa imani walikubali mpango wa Mungu kwani dhabihu za kuchinja wanyama walizozitoa zilikuwa ni mfano uliomwakilisha Mwana Kondoo wa Mungu atakayezichukua dhambi za ulimwengu. Kwa imani katika dhabihu walizozitoa waliwekwa huru na kubadilishwa kuwa viumbe vipya kwa njia ya imani katika Masihi aliyeahidiwa. Hivyo tumaini la vizazi vyote limewekwa katika msingi wa kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Mungu aliongoza washirikiwa Kanisa la wakati wa Agano la kale kupitia kwa Manabii. Musa ndiye Mwandishi wa kwanza ambaye kupitia kwake Mungu alimtumia kuweka kumbukumbu za maagizo yote ya kudumu kwa ajili ya kanisa lake ili kudumisha uzoefu wa watu wake kwa vizazi ambavyo vingekuwa baada yake. Maandiko haya yenye uvuvio wa Roho wa Mungu yalisomwa

mbele ya Makutano katika siku za Sabato ya siku ya Saba na pia katika matukio mengine ya pekee. Leo Maandiko haya yanajulikana kama Agano la Kale.

b) **Kanisa katika nyakati za Agano Jipya:**

Kanisa la siku za Agano Jipya lina Msingi wa imani ambao umeridhishwa kutoka Kanisa la siku za Agano la Kale. Lilikubali Sheria ya Mungu kama Kanuni pekee ya maisha. Bwana wetu Yesu Kristo alitambua wazi kwamba wapo baadhi ya watu ambao watadhani kwamba alikuja kutangua mafundisho ya Agano la Kale pamoja na sheria, na hivyo akasema "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au Manabii, La, sikuja kutangua, bali kutimiliza. "Mathayo 5:17. Kanisa la Agano Jipya kama ambavyo lilikuwa lile la Agano la kale liliipenda na kuitumainia sheria ya Mungu. Mtume Paulo alisema "Kwa maana naifurahia Sheria ya Mungu kwa utu wa ndani" Warumi 7:22.

Kanisa la wakati wa Agano Jipya lilipata upendeleo wa kumwona Bwana wa Utukufu ambaye alikuja kwao katika umbo la mwanadamu. Kwa bahati mbaya washiriki wa Kanisa hilo, japokuwa walijifunza maandiko hawakuweza kumtambua Kristo kama Bwana na Mwokozi wa Ulimwengu kwa sababu ya ukuta mzito wa mila na desturi ambao uliwazuia wasiweze kumtambua wala kumpokea. Mitume waliendelea kuhubiri kwamba hakuna wokovu katika mwingine awaye yote kwa maana hapana jina jingine chini ya mbigu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwao". Matendo 4:12.

Baada ya kupaa kwa Yesu, ndipo kanisa la mitume liliposimikwa na hivyo Yakobo akawa ndiye kiongozi wake wa kwanza. Kanisa lilikuwa na mipango madhubiti ya Uinjilisti, zaidi ya wale mitume kumi na wawili, vile vile tunasoma habari za Paulo ambaye amekuwa Mwinjilisti Mkuu katika wakati wote na Barnaba, Sila, Yohana, Marko, Apolo, Timotheo na Tito; tunasoma pia kwamba Mashemasi walichaguliwa kama watenda kazi katika Kanisa la kwanza.

Inaonyesha wazi kwanza Kanisa la mwanzo, makao yake makuu yalikuwa kule Yerusalemu, lakini walimu na Mitume waliagizwa kwenda "ulimwenguni mwote na kuibuhiri Injili kwa kila kiumbe".

Viongozi pamoja na Washiriki wa Kanisa la kwanza la Kikristo waliziandika Injili pamoja na nyaraka mbali mbali, si kwa manufaa ya kanisa la kwanza tu bali hata kwa makanisa ya baadaye katika karne ambazo zingefuata. Majuma machache tu baada ya Bwana Yesu kupaa mbinguni, ndipo washiriki wa kanisa la Agano Jipya walipopata mateso makali. Mitume waliwekwa magerezani kwa sababu ya kuhubiri na hatimaye Stefano, mtu wa Mungu akawa mtu wa kwanza kuuawakwa ajili ya kutetea ukweli wa injili katika mwaka wa 34, pale walipomuua kwa kumpiga mawe. Kadiri ukristo ulivyozidi kuenea katika dola ya Warumi, ndivyo Kanisa lilivyozidi kukutana na upagani na hivyo wafuasi wa Kristo walitiwa magerezani, kuteswa na hata kuuawa. Muda ambapo giza la mateso makali lilisonga ilikuwa ni kati ya miaka ya 100 na 300. Baada ya kuona kwamba upanga wa mateso hauwezi kukomesha Kanisa la Kikristo, ndipo yule adui wa roho za watu akabuni mbinu nyingine ya mashambulizi. Hivyo akaazimu kulifanya Kanisa lipendwe na Serikali na Watawala na kufanikiwa kuingiza amapokeo na taratibu za kipagani katika dini ya Kikristo.

Polepole mafundisho ya uongo yakapenyezwa ndani ya Kanisa. Wale waliokuwa na imani dhaifu hatimaye ilipotea kabisa kwa kadri Wakristo walivyozidi kupata utajiri mwingi katika

biashara na nguvu Serikalini. Katika mwaka wa 476 makabila katili kutoka Kaskazini yalivamia na kuiangusha dola ya Rumi na katika harakati hizo hizo, ndipo Kiongozi wa Kanisa la Rumi aliyejulikana kama Askofu akatawazwa kuwa ndiye Kiongozi wa Kanisa.

Biblia haikuruhusiwa kushikwa na kusomwa na washiriki wa Kanisa wa kawaida, pengine ni kwa sababu zilikuwapo makala chache tu ambazo zilikuwa zimeandikwa kwa mkono. Lakini sababu nyingine kubwa ilikuwa ni mbinu ya viongozi wa kanisa la Kirumi ili kuzuia watu wasisome Maandiko Matakatifu wasije wakagundua mafundisho yaliyopotoshwa. Kwa mfano, imani kwamba roho haifi, kuabudu watakatifu, pagatori (imani ya mafundisho ya Kanisa Katoliki kuhusu hali ya mateso ya muda baada ya kifo ili kutakasika) na utunzaji wa Jumapili kama siku ya ibada ambao hauna msingi wowote katika mafundisho ya Maandiko Matakatifu kama yalivyofundishwa na Bwana wetu Yesu Kristo.

Kanisa la Rumi hujigamba kwamba ndilo lililobadilisha siku ya Ibada kutoka siku ya Sabato ya siku ya saba hadi Jumapili siku ya kwanza ya juma. Historia pamoja na Maandiko Matakatifu ya Biblia huonyesha wazi kwamba utunzaji wa Jumapili kama siku ya Ibada ya Kikristo chimbuko lake ni Upagani. Pamoja na makubaliano na uasi ambao ulitambaa kanisani, lakini daima walikuwepo waaminifu wachache wateule wa Mungu, ambao walidumu kuwa na imani ya Yesu pamoja na kuzitunza Amri za Mungu.

### c) Kanisa katika zama za Giza

Katika karne ya sita Maaskofu wa Rumi walikuwa na nguvu na mamlaka juu ya makanisa mengi ya Kikristo. Utawala huu wenye nguvu ulijulikana kama Upapa na Papa mwenyewe akiwa ndiye Kiongozi wake Mkuu. Mnamo mwaka 538 utawala huu ulifikia kilele cha mafanikio yake katika nguvu za utawala na hivyo mwaka huo ukawa ndio mwanzo wa zama za giza ambapo Rumi chini ya Utawala wa Upapa ilitawala kwa muda wa miaka 1260. Kama ilivyotabiriwa na Nabii Danieli na Yohana katika vitabu vyao vya Unabii (Danieli 7:25; 8:13,14 na Ufunuo 12:6; 13:5). Kipindi hiki cha kushamiri kwa Upapa kilikoma mnamo mwaka 1798 wakati ambapo Papa aliyekuwa madarakani siku hizo alikamatwa na Jemadari wa Jeshi la Kifaransa – Bethier na kutiwa gerezani mwezi February, 1798 ambapo alifia humo gerezani.

Kwa mamlaka ya kibinadamu tu Kanisa liliwalazimisha wafuasi wa Kristo kuchagua kupokea mapokeo na mafundisho ya upagani wa Kikatoliki au kutiwa magerezani na pengine kuteswa hadi kuuawa kwa upanga au kuchomwa moto. Kipindi hiki kirefu cha historia kinajulikana kama zama za giza. Mwanahistoria mmoja alisema. "Wakati ambapo Upapa ulikuwa umeshamiri vizuri sana; kwa ulimwengu ulikuwa ndio usiku wa manane".

"Pamoja na Ukungu mzito wa giza uliokuwa umetanda katika dunia katika kipindi hiki kirefu cha mafanikio ya Upapa, lakini bado mwangaza wa ukweli haukuweza kuzimika kabisa. Katika kila kipindi kumekuwa na mashahidi wa Mungu, wanadamu ambao wamekuwa na imani iliyohai katika Kristo na kwamba Kristo ndiye mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu; ambao waliithamini Biblia kama ndiyo kanuni pekee ya maisha na kuitunza Sabato Takatifu ya Bwana. Ni jinsi gani ulimwengu unawiwa kwa watu hawa, vizazi vyote ambavyo vingekuwa baada yake kamwe haviwezi kufahamu. Watu hawa waliotetea ukweli na kuuhifadhi walipachikwa majina mbali mbali mabaya, wengine waliwaita wazushi, kutilia mashaka maneno waliyoyasema, kuzichafua tabia zao kwa kusingizia ujumbe wao ulidhalilishwa au kupotoshwa. Pamoja na hayo yote, Mashahidi hawa walisimama imara kizazi hadi kizazi, walidumisha imani yao ya usafi na

kuhifadhi kweli hiyo kama urithi na hazina ya pekee kwa viazi ambavyo vingekuwa baada yao" (The Great Controversy pg. 61)

**d) Kanisa la matengenezo:**

"Katika nchi kadhaa za mbali ambapo utawala wa Warumi haukuwa na mamlaka ya Kiutawala pamekuwa na Jumuiya mbali mbali za Kikristo kwa muda wa karne nyingi ambazo hazikukumbwa na mchafuko wa mafundisho ya Upapa… Wakristo hawa walijenga imani yao juu ya ukweli kwamba sheria ya Mungu haibadiliki na hivyo itadumu na kuendelea kufaa kwa vizazi vyote. Makanisa yaliyojengwa juu ya msingi wa Imani ya namna hii yalikuwa huko Afrika ya kati na miongoni mwa Waalmania barani Asia".

"Miongoni mwa wote waliosimama kidete kupinga uvamizi wa mamlaka ya Upapa Waldensia ndiyo walikuwa mstari wa mbele. Walikuwepo katika nchi ile ile ambapo Upapa ulikuwa umeweka kitovu chake, madanganyo na mafundisho yao ya uongo waliyapinga vikali" "Waldensia walikuwa ni miongoni mwa watu wa kwanza barani Ulaya kupata tafsiri ya Maandiko Matakatifu".

"Nyuma ya safu za milima yenye maporomoko ndiko kulikokuwa makimbilio ya watu wa Mungu walioteswa na kukandamiza, katika vizazi vyote, na Waldensia walipata mahali pa kujificha huko, na huko ndiko ambako mwangaza wa nuru ya kweli ulihifadhiwa na kuendelea kumulika katika giza la zama za kati: kwa muda wa miaka elfu. Mashahidi wa Mungu waliendelea kuihifadhi imani hii ya Kale.

John Wycliffe alikuwa mwana matengenezo wa uingereza na ulimwengu wa Kikristo kwa ujumla. Shutuma kubwa dhidi ya Rumi ambalo ndilo lilikuwa msingi wa mahubiri yake kamwe lisingeweza kunyamazisha…."Wakati ambapo usikivu na mawazo ya Wycliffe yalipoelekezwa kwa Maandiko Matakatifu, alitumia muda wake kufanya uchunguzi wa kina na makini ambavyo vilimfanya aweze kupata uwezo mkuu na kuyajua mafundisho kama ambabavyo mtu aweza kujifunza akiwa shuleni. "Mungu alikuwa ameweka kazi yake mikononi mwa Wycliffe; kinywani mwake neno la kweli alihifadhi na kuweka mlinzi atakayehakikisha kwamba neno hilo limewafikia watu waliokusudiwa. Mungu alitunza uhai wake na kuikuza kazi yake pamoja na kurefusha muda hadi hapo msingi imara wa kazi hiyo kuu ya matengenezo utakapokuwa umejengwa. Wycliffe alikuwa miongoni mwa wanamatengenezo wakuuu. (The Great controversy pg. 63-66, 80,81,92-94)

"John Huss alikuwa miongoni mwa washiriki wa Kanisa la matengezo ambaye alisoma na kuamini Maandiko yaliyoandikwa na John Wycliffe, baadaye alipofanywa kuwa kiongozi alikemea mafundisho yote katika kanisa ambayo hayana msingi katika Maandiko matakatifu. Hivyo mahubiri yake yaligonga mioyo ya watu na kuamsha hamu na usikivu wa mamia ya wanafunzi wa Biblia katika sehemu mbali mbali za Bohemia na Ujerumani. Hatimaye John Huss kama walivyomtenda rafiki yake Jerome ambaye pia alikuwa alimwunga mkono, alifungwa katika mti uliosimikwa ardhini kabla ya kumchoma moto hadi kufa, adhabu ya namna hiyo ndiyo iliyotolewa kwa wote waliotiwa hatiani kwa kosa la uzushi.

Msukumo mkubwa wa matengenezo katika Kanisa ulifikia kiwango chake cha juu kabisa katika kipindi kile ambapo Martini Luther alionyesha imani yake kwa ushupavu mwingi. Akiwa na umri wa miaka 21 tu Martin Luther alikuwa tayari ameshakuwa mwanafunzi aliyefuzu katika mafundisho, aliisoma Biblia ya Kilatini ambayo ilikuwa ndiyo Biblia pekee aliyopata kuiona

mpaka wakati huo pia alikariri vifungu mbali mbali katika Biblia hiyo; kwa Jinsi hiyo aliweza kubaini usemi kwamba “Mwenye Haki ataishi kwa Imani”.

Mnamo November mosi, 1517 Luther alibandika orodha ya mambo tisini na tano katika lango kubwa la mbao la Kanisa la Wittenberg Castle, mambo hayo ambayo baadaye yalipigwa chapa na kusambazwa katika Ulaya yote. Na alipotakiwa kukanusha mambo hayo aliyoyaorodhesha alikataa kata kata na kujibu kwamba

> “Kamwe siwezi kufanya hivyo, sitakanusha mambo hayo, kwa kuwa si salama kwa Mkristo kusema kinyume cha dhamira yake mwenyewe. Ninasimama imara, sitaweza kufanya jambo tofauti, Mungu anisaidie Amina.”

Kanisa la matengenezo lilikua na kupanuka kama matokeo ya kazi ya kutafsiri Biblia katika lugha ya Kijerumani iliyofanywa na Martin Luther.

Philip Melanchthon alikuwa rafiki wa karibu sana wa Luther na vile vile alikuwa mwalimu kule Wittenberg, alisaidia katika kutayarisha rasimu ya toba ya Augusburg ambalo ndilo jambo kubwa ambalo lipo katika matengenezo ya Waprotestanti.

John Calvin huyu ni Mfaransa ambaye aliwatia moyo na kuwaimarisha watengenezaji wa awali wa huko Ufaransa. Wengi wa wanafunzi wake baada ya kutoa Giniva na Uswissi walikwenda Hispania. Uingereza na nchi zingine ambako waliimarisha matengenezo: miongoni mwa wanafunzi wake waliokuwa na hamasa kubwa alikuwa John Knox ambaye mafundisho yake yaliisukasuka misingi ya mafundisho ya uasi huko Scotland.

Ulrich Zwingli ndiye aliyekuwa mwana matengenezo wa huko Uswissi katika nyakati ambazo Martini Luther alikuwa akifanya matengenezo. Zwingli alikuwa Mchungaji wa kanisa Kuu la Zurich. Uswissi pakawa ndiyo mahali penye amani na kutengamaa kama kituo cha Taifa la Kiprotestanti. Huko Scandnavia pia matengenezo yalishamiri. Wachungaji wa Kipetri walitafsiri Biblia kwenda katika lugha ya Kiswidish na hivyo kuifanya Swideni kuwa nchi ya Kiprotestanti” John Tausen alihubiri habari za matengenezo huko Denmark. Pedornsen ndiye aliyeitafsiri Biblia kuwa lugha ya Kidenish na kwa kupitia kazi yao hiyo ya kutafsiri Maandiko na kuhubiri basi Denmark ikawa nchi ambayo Uprotestanti umeshamiri na kuota mizizi sana.

Kanisa la matengenezo liliendelea na kazi na kusaidiwa zaidi kwa tafsiri zaidi ya Biblia katika lugha mbali mbali. William Tydnale kwa kushirikiana na kiwanda kimoja cha Uchapishaji walifanikiwa kuchapa Biblia huko Uingereza kwa lugha ya asili ya watu hao ambayo ilitumika na watu wa kawaida na hivyo neno la Mungu likawaweka huru watu wengi katika nchi mbali mbali za huko. Giza lililokuwa likitawala likaondoshwa kwa njia ya Neno la Mungu, badala ya ujinga Maandiko yakachukua nafasi, watengenezaji waliofuata baadaye kama John Wesley waliweza kuieneza Injili ya kweli kwa mataifa kwa njia ya kuaminika na iliyo bora zaidi.

**e) Kanisa la Mahujaji wenye Imani kali ya Kidini:**

Mnamo Septemba 16, 1620 kadiri ya Mahujaji 100 waume kwa wake walikuwa na msimamo mkali wa kidini walitweka jahazi lao baharini kuelekea nchi ya Maua ambayo katika siku zetu inajulikana kama marekani. Safari yao ya Imani iliwezekana tu kwa sababu walikuwa wanataka uhuru wa kidini, kudiriki kwao kutenda hivyo kulifungua njia na kuwaongoza wapende Uhuru

walioishi baadaye kama Roger Williams, ambaye alikuwa ndiye mwanzilishi wa Koloni la Kisiwa cha Rhode, ambayo yalikuwa ndiyo makazi ya kwanza huko marekani kuwa na mfumo wa utawala wa Jamhuri huku kukiwa na uhuru kamili wa kidini.

**f) Kanisa la Wamishonari wa Kwanza:**
Mwanzilishi wa Misheni za kisasa tunazoziona siku hizi ni William Carey, aliyekuwa akiishi nchini Uingereza mnamo miaka ya (1761) -1834). Katika umri wake wa ujana alifanya kazi ya kushona viatu, wakati alipokuwa akiendelea na kazi hiyo siku zote alizoea kuweka ramani kubwa ya ulimwengu mbele ya ukuta uliokuwa mbele ya meza aliyokuwa akifanyia kazi. Mshona viatu huyu alihamasishwa kusafiri baharini mpaka nchi za kigeni na nahodha mmoja aliyeitwa Cook ambaye maelezo yake kuhusu safari zake yalimvutia sana. Hubiri lake alilolitoa katika kundi la ambaye maelezo yake kuhusu safari zake yalimvutia sana. Hubiri lake alilolitoa katika kundi la Wachungaji ndilo lililokuwa chimbuko la kuanzishwa kwa kazi ya Umishonari na hivyo jamii ya kwanza ya Kimishonari iliundwa na Carey mwenyewe akawa ndiye Mmishonari mwanzilishi kwa kusafiri hadi India. Pamoja na vipingamizi vyote alivyopata, lakini bado alifanikiwa kutafsiri ya kadhaa za Maandiko Matakatifu na hivyo akawa ameweka Msingi kwa Umishonari wa Kisasa.

Mwanzoni mwa karne ya 19 (kumi na tisa) Makanisa ya Kiprotestanti yalikuwa na mwamko zaidi wa kazi ya Umishonari. Vyama mbali mbali vilianzishwa kila mahali kusaidia kazi ya Umishonari katika nchi mbali mbali. Zaidi ya vyama 7 vilianzishwa huko Uingereza na Marekani. Katika robo ya kwanza ya karne hiyo kufuatia kuanzishwa kwa chama cha Kimishonari cha Kanisa mnamo mwaka 1799, ambapo ndiyo kwanza Zama za Umishonari wa Kisasa zilikuwa zimeanza. Miongoni mwa watu ambao walipata mateso makali na kupata hasara kubwa kwa ajili ya kupanuka mipaka ya kuendea kwa Injili ni hawa wafuatao:

| | |
|---|---|
| William Carey | Mmishonari wa kwanza huko India |
| Robert Morrison | Aliitayarisha Kamusi ya maneno ya Kiingereza kwenda Kichina pamoja na kuchapisha Biblia |
| Adoniram Judson | Alitafsiri Biblia kwa lugha ya watu wa Bama na pia alifanya kazi huko India |
| David Livingstone | Alikuwa mwasisi wa Ukristo katika Bara la Afrika |
| Robert Moffat | Alikuwa mtangulizi wa kazi katika Afrika |
| John Williams | Aliwaongoza wajumbe wa amani kusafiri Kusini mwa bahari ya Pacific |
| John G. Paton | Alitishiwa kuuawa na Wakanibalia mara 53 katika visiwa vilivyo Kusini mwa bahari ya Pacific. |

**g) Kanisa la Wanamarejeo:**
Kanisa katika pindi hiki lilikuwa likitilia mkazo mafundisho ya Utume wa Kristo wa Kurudi mara ya pili, uvuvio huo na mwamko wa watengenezaji juu ya tukio hili, dalili zilizokuwa zikionyesha ukaribu wa tukio hilo ndiyo vilivyotawala mahubiri kwamba Yesu angerudi tena mapema katika karma ya kumi na tisa (19) Kazi aliyoifanya William Miller ilichukua umuhimu wa kwanza katika kazi iliyofanywa katika siku zile; katika nchi mbali mbali watu waliibuka na kuhubiri ujumbe wa kurudi mara ya pili kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Wakati ambapo angekuja katika dunia mara ya pili kama Mfalme wa Wafalme, kama ilivyotabiriwa na Manabii waliotangulia, walioishi katika zama za Kanisa la Wakati wa Agano la

Kale. Ambayo pia ilikuwa ndiyo mada kuu, katika zama za Kanisa la Agano Jipya. Kwa karne nyingi katika zama za giza. Mateso makali kwa watu wa Mungu pamoja na watu kuuawa tumaini lao kuu na nguvu lilijengwa juu ya ahali ya kurudi kwa Kristo mara ya pili.

Watengenezaji hawa waliamini kabisa Unabii, kuhusu tukio la kuja kwa Kristo mara ya pili, kwa vielelezo dhahiri walidhihirisha imani yao kwa jambo hili na kwamba muda mrefu usingepita kabla ya Kristo kurudi, hivyo tunaona kuja kwake mara ya pili ikawa ndiyo mada iliyotawala katika siku hizo katika sehemu mbali mbali za kanisa la Kikristo na ilihusu sana katika kuleta uamsho wa kidini. Kipengele hiki cha historia ya Kanisa chenye kusisimua kitazungumziawa kwa undani katika sehemu inayofuata ya kitabu hiki.

**h) Kanisa la Masalio:**

Msamiati huu Masalio ni neno lililotumika katika Biblia kuelezea kanisa la wakati wa mwisho katika kipindi cha kufungwa kwa historia ya ulimwengu. Kama ilivyo kwa Masalio au masazo ya kipande cha kitambaa kutoka katika jora zima, ndivyo ilivyo kwa Kanisa. Kanisa la Masalio ni lile ambao litasalia hadi mwisho wa wakati.

Masalio ya kipande cha kitambaa haina tofauti yoyote na ile ya jora zima, hivyo basi kanisa la masalio ni sawa kabisa na kanisa la kweli kama lilivyoanzishwa na Mungu mwenyewe na kuendelea katika vizazi vyote.

**Katika kitabu cha Ufunuo, Yohana huzitaja tabia kadhaa zinazolitambulisha Kanisa la Masalio** (Kariri mafungu yafuatayo na kufahamu mahali yanapopatikana)

- Kushika amri Kumi za Mungu (Ufunuo 12:17)
- Kuwa na Ushuhuda wa Yesu au Roho ya Unabii (Ufunuo 12:17,19:10)
- Kutangaza ujumbe wa Malaika watatu kwa kila Taifa, na Kabila na Lugha na Jamaa (Ufunuo 14:6)
- Kutangaza angako la Babeli ya Kiroho (Ufunuo 14:8)
- Kuwaonya watu juu ya kupokea alama ya Mnyama (Ufunuo 14:10)
- Kuwa na subira ya Watakatifu (Ufunuo 14:12)
- Kuwa na imani ya Yesu (Ufunuo 14:12)

**Kanisa la Masalio ni lile litakalo " ishindania imani waliyokabidhiwa Watakatifu mara moja tu" (Yuda 3).** Kwa maneo mengine Kanisa ni lazima liendeleze kazi ya matengenezo iliyo kuwa ikifanywa na Waprotestanti. Ni lazima lipinge mafundisho ya Kiprotestanti yaliyo kinyume na kweli ya Biblia, pia litawaongoza wake kwa waume katika kupinga mafundisho yaliyochanganywa na mila na desturi za watu badala ya kweli ya Neno la Mungu.

Kazi ya matengenezo katika Kanisa la Masalio itajengwa katika misingi ya Neno la Mungu liyodhahiri kabisa ili kuwawezesha watu kutembea katika nuru ya Neno la Mungu badala ya kufuata mapokeo ambayo ni mafundisho ya wanadamu.

Katika mpango wa Mungu ameliweka wakfu Kanisa la Masalio ili kwamba liweze kuhubiri Injili ya milele pamoja na Ujumbe wa malaika watatu katika ulimwengu wote kabla ya kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo mara ya Pili.

Kama Yohana Mbatizaji alivyokuwa mchukuzi wa ujumbe wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza, kadhalika kanisa la Masalio litachukua ujumbe wa kurudi wa Kristo mara ya pili kwa ulimwengu

wote. Maandiko hunena wazi wazi kwamba "Alikuwako mtu ametumwa kutokea kwa Mungu, jina lake aliitwa Yohana. "Biblia pia hueleza kwamba litakuwako Kanisa la masalio ambalo pia litakuwa limetumwa na Mungu.

**Mafundisho ya Kanisa la Waadventista wa Sabato hupatana kabisa na mafundisho ya Kanisa la Kikristo katika vizazi vyote**: Kadiri utakavyokuwa ukijifunza Biblia utagundua kwamba mafundisho juu ya ukweli kuhusu mada kama haki kwa neema kwa njia ya imani, hukumu. Sabato ya siku ya Saba, ubatizo kwa kuzamishwa majini, zaka, karama ya unabii, kuja mara ya pili kwa Kristo, hali ya wafu, kutengwa kutoka katika ulimwengu, yamekuwa ndiyo mafundisho ya kanisa katika zama zote. Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe ambaye ndiye kielelezo chetu alibatizwa kwa ubatizo wa kuzamishwa majini, aliitunza Sabato ya siku ya saba, alifundisha juu ya Utakatifu wa Ndoa pamoja na wajibu wa kila mtu kurudisha Zaka ya Bwana, pia aliwaonya wanadamu juu ya hukumu itakayokuja, na haya ndiyo mafundisho ya Kanisa la Waadventista wa Sabato katika siku tunazoishi.

**Watu wa Mungu hupatikana katika madhehebu zenye imani mbalimbali, watu wa Mungu** ni wale wote ambao wanatembea katika nuru ya neno lake kwa kadri walivyofunuliwa, watu ambao ni waaminifu kweli kweli katika mioyo yao watakapofahamu ujumbe wa Malaika watatu uliopo katika kitabu cha Ufunuo 14:6-12 watautii.

Yohana hueleza kwamba wale wote ambao wako katika Babeli ya Kiroho watatoka humo na kujiunga na kanisa la masalio. Mungu anawataka wote watoke na kujiunga na Kanisa la Masalio ili waweze kuwa mashahidi wa ile kweli na kuwa tayari huku wakingoja kuja kwa Yesu mara ya pili.

**Kuwa Mshiriki wa Kanisa la masalio ni upendeleo wa Pekee**. Umepewa nuru kubwa na hivyo Mungu amekupa wajibu wa kufanya ambao ni kuishi kutokana na nuru ambayo Mungu amekufunulia.

Katika sura chache zinazofuata za kitabu hiki utajifunza historia ya Kanisa la Masalio; kadri utakavyokuwa unaendelea kujifunza utagundua kwamba Mungu mwenyewe amekuwa akiongoza katika mfumo mzima na shughuli za Kanisa la masalio.

Hebu leo na uweke dhamira kwamba kwa Neema ya Bwana Yesu nitakuwa Mkweli na Mwakilishi Mwaminifu wa Kanisa ili uweze kupaza sauti na kuimba "Imani iliyo hai ya Baba zetu…..tutadumu kuwa waaminifu hata kifo".

## SEHEMU YA PILI
## WACHUKUZI WA UJUMBE WA MAREJEO – 1755 – 1843

### a) Dalili ya matukio Matakatifu katika Nchi

Dalili ya matukio haya matatu katika ulimwengu yaliyotokea katika miaka ya 1755, 1780 na 1833 yalilenga dhahiri kwa kuja kwa Kristo mara ya pili. Tukio la kwanza katika matukio hayo matatu ni lile tetemeko la Lisbon (Ureno) Tetemeko ambalo lilienea pia katika sehemu kubwa ya Ulaya na Afrika. Mtikisiko wake uliwafikia watu katika nchi za mbali Kaskazini kama Norway na Sweden, na magharibi mwa Greenland, Kaskazini mwa Marekani na West Indies. Eneo zima kwa ujumla ambalo liliathiriwa na tetemeko hili ni zaidi ya maili millioni 4 za mraba. Ambapo watu wengi walikimbia

huku na huko wakilia kwa hofu kwamba mwisho wa dunia umefika" Tetemeko hilo la mwaka 1755 lilitimiza Unabii wa kufunguliwa kwa Muhuri ya sita, ambayo habari zake zipo katika Ufunuo wa Yohana 6:12,13.

Miaka 25 baada ya tetemeko hilo, jua nalo likatiwa giza. Jambo ambalo Yesu alikuwa amelitabiri pale katika Mlima wa Mizeituni, wakati aliwaambia wanafunzi wake "Lakini siku zile baada ya dhiki, hiyo Jua litatiwa giza na mwezi hautatoa mwanga wake". Marko 13:24) "Siku zile zilizotajwa katika fungu hili hueleza juu ya kipindi cha miaka 1260 ambacho kilimalizika mwaka 1798; katika mpango wa Mungu mateso ya watu wa Mungu yaliyopinzwa, jambo ambalo lilileta kufupizwa kwa kipindi hicho ni kwa sababu ya matengenezo ya Kiprotestant. Hivyo ni dhahiri kutokana na Unabii kwamba Jua kutiwa giza kungetokea kabla ya mwaka 1798. Jambo ambalo lilitimia sawasawa kama maneno ya Unabii yalivyosema, mnamo Mei, 19, 1780, ndipo jua lilipotiwa giza.

Daktari mmoja ambaye wakati tukio hili lilipotokea alikuwa katika zamu ya kutembelea wagonjwa katika hospitali moja alitoa ushuhuda kwamba giza lilikuwa zito mno kiasi kwamba hakuweza kuona leso yake nyeupe iliyokuwa karibu kabisa na macho yake. Lilikuwa ni giza totoro. Ukimya huu ulioambatana na giza ulikuwa na msukumo wa namna ya pekee kwa watu wa kila rika wa kutoa ibada ya unyenyekevu kwa Mungu; Makanisa yalifunguliwa, Mikutano ya sala ikaendeshwa na watu waliamini kabisa kwamba siku ya hukumu ya Mungu ilikuwa imekwisha wadia.

Baada ya giza nene neno la usiku wa manane, ndipo giza lile likatoweka, na baada ya giza lile kutoweka mwezi ulionekana ukiwa mwekundu kama damu.

Yesu alitabiri pia kwamba nyota nazo zitanguka kutoka mbinguni. Hii ilikuwa ni moja ya dalili ambazo zingeonekana katika mbingu ili watu wote wapate kushuhudia, kutokana na maelezo ya Unabii wa Yohana, nyota zingeanguka kutoka mbinguni katika pande zote. "Kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake" (Ufunuo 6:13). Tukio hili lilitokea tarehe 13 Novemba, 1833, miaka miwili tu baada ya William Miller kuanza kuhubiri ujumbe wa kurudi mara ya pili kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

Mambo haya matatu yaliyotokea katika ulimwengu yalipangwa na Mungu mwenyewe ili kuwatanabahisha waume kwa wake kwa ukweli kwamba mwisho wa ulimwengu umekaribia. Dalili hizi zimeleta msukumo mkuu wa kuhubiri na kutoa mafundisho juu ya marejeo.

b) **Ujumbe wa malaika watatu**

Wakati ambapo utimilifu wa wakati katika mpango wa Mungu wa kutoa ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu unaopotea, ulipotimia, tukio hilo alilileta kwa njia ya mfano wa malaika watatu wenye nguvu. Mungu angeweza kutuma viumbe watakatifu toka mbinguni wenye umbo la mwanadamu ili waje katika dunia kwa utukufu mwingi na kupiga mbiu kutangaza ujumbe huu kutoka katika vilele vya milima, lakini huu haukuwa mpango wa Mungu; washiriki wa kanisa katika zama tunazoishi ndio waliokabidhiwa jukumu la kutangaza ujumbe huu, ni washiriki wa kanisa la Mungu walio na Roho Mtakatifu huwapa nguvu za kutangaza ujumbe huu kwa ulimwengu.

Yapo mafundisho mengi yaliyomo katika ujumbe wa malaika watatu, lakini ujumbe huu unaweza kuelezwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Ujumbe wa malaika wa kwanza: hutoa wito kwa wanadamu kumcha Mungu na kumtukuza. Yeye aliyezifanya mbingu na nchi na pia hutoa tahadhari kwamba saa ya hukumu yake imekuja.

Ujumbe wa malaika wa pili: hutangaza anguko la Babeli ya Kiroho

Ujumbe wa malaika wa tatu: hutoa onyo kwa watu wanaoishi katika kipindi cha Kanisa la Masalio dhidi ya kupokea alama ya mnyama.

Vitabu vya Danieli na Ufunuo hubeba ujumbe maalumu wenye manufaa makubwa kwa watu wanaoishi katika kipindi cha kufungwa kwa historia ya ulimwengu; hivyo ni lazima ujifunzwe na wote wanaoishi katika nyakati hizi.

Ujumbe wa malaika wa tatu wa sura ya 14 ni muhtasari wa mafundisho maalum yanayopatikana katika vitabu vya Danieli na Ufunuo, ambavyo ni lazima yafundishwe kwa watu na wale wote ambao ni washiriki wa kanisa la masalio, ili kwamba watu wanaoishi katika siku hizi za mwisho waweze kufanya uamuzi wa kufuata ukweli badala ya kupotezwa kwa kufuata udanganyifu na mapokeo.

**c) Mabalozi wa Marejeo Huko Marekani**

**1. William Miller, 1782 - 1849**

Katika nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa (19) Mhubiri wa Kimarekani aliyevuviwa aliyeitwa William Miller alihubiri kwa nguvu ujumbe wa marejeo ya Kristo. William alikuwa ndiye kijana mkubwa katika familia yenye watoto kumi na sita, hata hivyo Miller hakuweza kupata kile kinachojulikana kama elimu bora lakini kutokana na hamu kubwa ya kupata elimu aliyokuwa nayo aliweza kujisomea mwenyewe. Baadaye kwa sababu ya kuhusiana kwake na wanasiasa pamoja na wasioamini, akawa shabiki wa siasa, pamoja na kwamba alivutiwa na mambo hayo, lakini ukweli wa Biblia ulikuwa bado umetunzwa moyoni mwake.

Kwa namna ya ajabu, mabadiliko yalitokea katika maisha yake kutoka kuwa shabiki wa siasa hadi kuwa mtu wa Mungu mwenye imani, hata hivyo alipata upinzani toka kwa marafiki zake wa zamani ambao walikuwa wakishirikiana katika mambo ya siasa. Walifahamu hali yake ya kukosa msimamo thabiti katika imani ya Biblia. Ili kudhihirisha imani yake ilimbidi ajifunze kwa miaka kadhaa, ni katika muda huu ndipo alipobaini ukaribu wa kuja mara ya pili kwa Kristo ulivyokuwa.

Alijifunza kwa bidii tangu mwaka 1816 hadi 1631 na akaridhika kabisa na yale aliyojifunza hivyo akakereketwa na kuona kwamba asingeweza kunyamaza na kwamba ilikuwa ni lazima awaambie wengine juu ya ugunduzi muhimu aliokuwa amefunuliwa.

Akiwa na umri wa kadri ya miaka 50 (hamsini) hivi mtu ambaye hakupata kujifunza maishani mwake namna ya kutoa hotuba hadharani alijaribu kujizuia asieleze wazi mambo aliyokuwa amejifunza. Hatimaye aliweka nadhiri mbele za Mungu kwamba atahubiri habari hizo iwapo tu jafasi ingepatikana, katika asubuhi moja ya Sabato mwezi Agosti, 1831, alipokuwa akiendelea kujifunza katika nyumba alipewa taarifa na mpwa wake aliyeitwa Irving Guilfred kwamba

Mchungaji wa Kanisa la Kibaptisti alikuwa amesafiri na hivyo baba wa Irving alimwomba Miller aje kutoa somo Jumapili ile juu ya habari za kuja kwa Kristo mara ya pili.

Tokeo wakati huo Miller aliendelea kuhubiri katika sehemu za mashambani zilizokuwa karibu na nyumbani kwake. Watu wengi walimjia toka sehemu mbali mbali zilizomzunguka ili kusikiliza hotuba alizokuwa akizitoa, ambapo wengine walileta mialiko toka pande zote ya kumtaka aje kutoa hotuba.

Katika hotuba zake alizungumza juu ya dalili za kurudi kwa Kristo na alirejea kwa zile ambazo tayari zilikuwa zimetimia. Mfano siku ambapo jua lilitiwa giza Mei 19, 1780. Mafundisho yake yalikaziwa kwa tukio la kuanguka kwa nyota Novemba 13, 1833. Ushirikiano baina yake na Joshua V. Himes wa Boston kulisababisha apate mialiko zaidi ya kuhubiri katika miji. Alianza kuhubiri katika jiji la New York mwaka 1840 na inakadiriwa watu wapatao elfu hamsini waliupokea ujumbe wake.

Miller alijifunza zaidi juu ya Unabii wa siku 2300 wa sura ya 8 na 9 ya kitabu cha Daniel na baadaye akaridhika kabisa kwamba kutakaswa kwa Hekalu kulikuwa ndiyo kutakaswa kwa dunia kwa moto wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili. Japokuwa alihubiri sana kuhusu marejeo ya Kristo, lakini hadi mwaka 1844 hakuweza kubaini tarehe maalumu ya kuja kwa Kristo. Ingawaje mnamo mwezi Januari 1843 alisema Yesu angerudi tena kati ya Machi 1843 na Machi 1844.

Wakati William Miller na wenzake walipoanza kufundisha kuhusu unabii, viongozi wa kanisa hawakupendezwa: mwishoni mwa mwaka 1843 hadi 1844 washiriki wengi wa kanisa walioamini ujumbe wa marejeo walitengwa na makanisa yao ambayo bado waliyapenda na kupenda kusaidia; miongoni mwa watu hao alikuwa Robert Harmon pamoja na jamaa yake. Upinzani uliendelea kuwa na nguvu na katika mwaka 1844 ilikuwa dhahiri kwamba makanisa yale yaliyopendeka yalikuwa yamekataa ujumbe wa malaika wa kwanza ulioletwa kwao na Wana amarejeo.

Baada ya mwaka 1843 na 1844 kupita bila Yesu kutokea, imani ya William Miller haikutetereka, aliendelea kuhubiri habari za kurudi kwa Kristo mara ya pili.

Kazi yake ya kutoa mahubiri ya hadhara ilikoma mwaka 1845 na mika 4 baadaye yaani 1849 ndipo akafa.

Katika maisha yake yote alikuwa ni Kiongozi katika kazi ya Mungu na mwanafunzi makini wa Biblia; hata hivyo katika kujifunza kwake hakupata kubaini kuhusu Sabato ya kweli.

Katika muda miaka kumi, William Miller alitoa mahubiri zaidi ya 3,000 katika sehemu tofauti tofauti zaidi ya 1,000. Mnamo mwaka 1848 mtendakazi huyu mkongwe alipata upofu na mwaka uliofuata akafa akiwa na tumaini thabiti la kumwona Mwokozi akirudi. Alipokea ujira kidogo kwa kazi zote lakini kamwe jina lake lisingeweza kutenganishwa na ujumbe wa marejeo. Alikuwa mtangulizi wa ujumbe wa Marejeo ambao hata sisi leo tunautangaza.

Karibu na mwisho wa mwaka 1842 Miller alitoa maoni yake kwa ulimwengu ambayo kwa sehemu kubwa huwakilisha imani ya wana marejeo wote.

**Maoni yake yalikuwa kama ifuatavyo:**

1) Ninaamini kwamba Yesu Kristo atarudi tena katika ulimwengu huu
2) Ninaamini kwamba atakuja na Utukufu wote wa Baba yake
3) Ninaamini kwamba atakuja katika mawingu kutoka mbinguni
4) Ninaamini kwamba atatawazwa kuwa Mfalme wa Ufalme wake utakuwa ni wa milele
5) Ninaamini kwamba hatimaye wateule watapewa Ufalme wa milele
6) Ninaamini kwamba wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili miili ya watakatifu waliokufa itafufuliwa kwa utukufu kama Kristo naye alivyofufuka
7) Ninaamini kwamba watakatifu watakaokuwa hai hapo atakapokuja Yesu watabadilishwa miili yao ya kufa na ndipo watanyakuliwa hewani pamoja na wale waliofufuka ili kumlaki Bwana nao watakuwa na Bwana milele.
8) Ninaamini kwamba wateule watakwenda mbele za Mungu wakiwa hawana hatia wala doa au kunyanzi katika upendo
9) Ninaamini Yesu atakapokuja mara ya pili atamaliza vita vya Sayuni na kuwakomboa kutoka nguvu za yule mjaribu ambaye ni shetani.
10) Ninaamini kwamba Yesu atakaporudi atawateketeza watenda dhambi wote kwa moto kama alivyotenda kwa ulimwengu wa zamani ambapo aliwateketeza kwa maji na kuzika roho zao kuzimu hadi hapo utakapowadia wakati wa kufufuka kwao ili wapate kuangamizwa.
11) Ninaamini kwamba baada ya dunia hii kutakaswa kwa moto, Kristo pamoja na wale waliokombolewa wataimiliki nchi hiyo mpya na kuishi humo milele na ndipo wateule watakapomilikishwa ufalme.
12) Ninaamini kwamba wakati umewekwa na Mungu mwenyewe ambapo mambo haya yote yatatendeka.
13) Ninaamini kwamba Mungu ameudhihirisha wakati huo maalumu.
14) Ninaamini kwamba wengi wa wahubiri na wale wanaomkiri Kristo hawataamini wala kuujua wakati hadi hapo wakati utakapowajia ghafla.

15) Ninaamini kwamba wenye hekima watang'aa kama mwangaza wa anga (Daniel 12:3) na wataufahamu wakati

16) Ninaamini kwamba wakati unaweza kufahamika kwa wale wote wenye nia ya kufahamu na kujitayarisha wawe tayari kumlaki. Na nina imani thabiti kwamba wakati fulani kati ya Machi 21, 1843 na Machi 21, 1844, kufuatana na namna amabavyo Wayahudi huzihesabu nyakati, Kristo atarudi na kuwaleta pamoja naye wateule wote na kwamba hapo ndipo atakapomlipa kila mtu ujira wake kwa kadri ya matendo yake….. "Life of William Miller pp. 170-173. Kwa hakika, William Miller anaitwa" Nyota ya Asubuhi ya Ujumbe wa marejeo kwa sababu:
    a) Alianzisha kazi ya kuhubiri Ujumbe wa Malaika wa Kwanza
    b) Alitangaza Injili kwa nguvu na kujitoa kiasi kwamba kazi aliyoifanya siku za mwanzo ilijulikana sana na hivyo ikaitwa kwa jila lake na wafuasi wake nao wakaitwa hivyo.

**2. Joshua V. Himes 1805 - 1895**

**Joshua V. Himes, ndiye Mhubiri wa pili aliyejulikana huko Marekani baada ya William Miller.** Huyu alizaliwa katika Kisiwa cha Rhode, na baba yake alipenda sana kijana huyu awe mhubiri katika kanisa la Episkopo, hata hivyo matamanio yake hayakuweza kutekelezeka kwa sababu ya ukosefu wa fedha na hivyo ikawa ni lazima kwa Joshua kuwa kibarua katika karakana moja ya useremala, lakini hilo halikukidhi hamu yake. Mvuto wa kupenda shughuli za kanisa ulizidi kuongezeka hatimaye katika umri wa miaka 22 alianza kazi ya uhubiri katika mji wa

Boston. **Miller na mwenzake Himes** walikutana kule Hempshire, mwaka 1839, na Himes akavutiwa sana na hotuba za Miller na hivyo akamwalika katika kanisa lake huko Boston. Hivyo hawa wawili wakawa wakitenda kazi pamoja ya kuhubiri juu ya ujumbe wa marejeo huko Marekani.

Baada ya Himes kusikiliza mahubiri ya Miller alimsonga kwa maswali kama alikuwa akiyaamini mafundishi "<u>Yale yeye mwenyewe</u>" Naye alijibu kwamba "Ndiyo" Himes akamwuliza tena kwamba kwa kuwa anaamini hivyo alikuwa anafanya nini kuhakikisha kwamba ujumbe huu umeenea ulimwenguni mwote. Miller alimhakikishia kwamba alifanya yote aliyoweza kwa uwezo mdogo aliokuwa nao. Lakini Himes aliendelea kulalama na kusisitiza kwamba ujumbe huu haujafahamika kabisa au umefahamika kidogo sana kwa watu; kwa maelezo haya Miller, alijibu "Je, unafikiri mkulima mzee angeweza kufanya nini zaidi? "Sikuwa na uzoefu wowote wa kutoa hotuba hadharani, sina mtu wa kunisaidia, Japokuwa nimefanya kazi kwa juhudi na kuongoa wengi kumgeukia Mungu, lakini hakuna yeyote aliyeonyesha nia yakujiunga na kazi hii ya kuhubiri Injili na kunipatia msaada ninaouhitaji. Hupenda kuniona nikihubiri mwenyewe na kuwajengea makanisa, na huo huwa ndiyo mwisho wa mambo yote. Nimekuwa nikitafuta msaada na bado ninauhitaji.
Himes ambaye naye sasa alikuwa ameyakubali mawazo ya Miller alikuwa na jambo moja tu la kufanya, aliazimia kuacha mambo yake mwenyewe, familia, jamii, heshima na yote yenye kumpendeza nakuamua kuyaweka katika madhahabu kama sadaka ili aweze kumsaidia Miller kwa uwezo wake wote hadi mwisho.

Joshua Himes alianza kuchapisha gazeti la Dalili za Mwisho wa Wakati "Signs of the Times" huko Boston mwaka 1840. Makala nyingine nyingi kuhusu marejeo zilizidi kuchapishwa ikiwa ni pamoja na lile la Kilio cha Usiku wa Manane "The Midnight Cry" ambalo mwanzo lilitolewa kila siku nakala 1,000. Hii iliendelea kutolewa huko New Yorkkwa majuma 4 tu na baadaye likaendelea kutolewa mara moja kila juma. Mikutano ya Makambi iliyohudhuriwa na maelfu ya watu ilisaidia sana katika kueneza ujumbe huu.

Himes alikuwa ni mtu mwenye tabia ya pekee sana, alikuwa kiongozi mwenye nguvu, shupavu, mwenye kuhamasisha na kufanyiza nakutekeleza mipango iliyoanzishwa na Miller kuhusu ujumbe wa marejeo. Mchango wake katika kuanzisha uchapaji wa kijarida cha mwanzo kuhusu kuja kwa Kristo mara ya pili kama dalili za mwisho wa wakati. "Signs of the Times" ulitoa msukumo mkubwa kwa ueneaji wa ujumbe wa Marejeo huko Marekani. Kazi yake baada ya mwaka 1850 haina mwito mkubwa, kwa kuwa hakujiunga na kundi la Waadventista wa Sabato baada ya kukatishwa tamaa na tukio la kutomwonaYesu akirudi mwaka 1844 kama walivyoamini. Pamoja na hayo yote, hakupoteza mvuto wa ujumbe wa marejeo hadi kufa kwake hapo mwaka 1895.

### 3. Josia Litch

Huyu ni miongoni mwa wahubiri wa Kiprotestanti wa kwanza kuamini ujumbe wa Marejeo na kuuhubiri kwa wengine. Alianza kuwa Mkristo akiwa na umri wa miaka kumi na saba tu, alijiunga na kanisa la Kimethodisti na kuwa Mhubiri wao. Mnamo mwaka 1838, alisoma kitabu kilichokuwa kimeandikwa na William Miller; hakuwa na uhakika na mafundisho hayo na hivyo aliazimu kuyakosoa baada ya muda mfupi. Hata hivyo kabla ya kukimaliza kitabu kile alikiri kwamba alikuwa ameridhishwa na hoja zote zilizotolewa na kwamba mambo yote yaliyoandikwa yalikuwa ya kiroho na dhahiri na hivyo isingewezekana kukanusha ukweli ambao Miller alikuwa ameuanzisha.

Joshua Litch alifanya kila juhudi kutenda kila jambo alilobaini kuwa ni la kweli, hata hivyo katika muda mfupi alijiunga na Wahubiri wa ujumbe wa marejeo. Baadaye Litch alichapisha kijarida chenye kurasa 48 kuhusu kurudi kwa Kristo mara ya pili. Alijiunga na William Miller na Joshua Himes katika mikakati ya kuhubiri injili na alikuwa mmoja wa wahariri wa gazeti la ujumbe wa marejeo "Signs of the Times".

**4. Charles Titch**

Wakati aliposoma makala mbali mbali za William Miller na kuanza kuhubiri ujumbe wa marejeo, alikuwa mchungaji wa kanisa la makutano huko Boston.

Yeye alichangia kwa njia nne kuu katika kuhubiri ujumbe wa marejeo huko Marekani.

a) Mhubiri alikuwa ni mhubiri aliyependwa sana na kiini cha mahubiri yake kilikuwa "Jitayarishe kukutana na Mungu wako" Inasemekena kwamba miongoni mwa wote katika Marekani waliohubiri na kufundisha habari za kuja kwa Kristo mara ya pili, hakuna aliyependwa kama yeye.

b) Mwandishi alichapisha waraka kuja kwa Kristo mara ya Pili (the second advent of Christi) ambao ulisambazwa mahala pengi sana na hivyo wengi wakaupata ukweli yumkini hata wale ambao wasingeweza kuhudhuria mikutano yake.

c) Mtunzi wa nyimbo, Hamu yake kubwa na mapenzi kwa ujumbe wa marejeo ulidhihirishwa katika nyimbo zake. Mmoja wa nyimbo hizo ni ule wimbo namba 338 CH "One Precious Boon, O Lord, I seek"

> "To that Bright Blest, Immortal Morn,
> By Holy Prophets long Foretold,
> My eagar linging eyes I turn,
> And soon its grories shall behold".

d) Msanii: Mwaka 1842 Fitch na wenzake waliweze kubuni jedwali maarufu la unabii la mwaka 1843 – Matukio mawili katika maisha ya Fitch huonyesha uelekevu wake na msukumo katika kuhubiri ujumbe unaoonyesha kuwa mwokozi anarudi upesi.

Katika mkutano wake mmoja watu wengi walikuwa wakijitoa kumpokea Bwana na mmoja wao kwa bahati mbaya alipokuwa akitembea kwenda mbele alijikwaa na kuanguka hatua kadhaa mbele. Kicheko cha chinichini cha wasikizaji kilinyamazishwa kwa maneno ya Fitch "Usijali ndugu! Ni vema kujikwaa kwa kuingia mbinguni kuliko kutembea salama kuelekea jehanamu".

Mnamo mwezi Oktoba 1844 hali ya hewa ilipobadilika na kuwa baridi Fitch alikuwa amemaliza tu kubatiza kundi la watu ndipo makundi mengine yalifuata kwa mfululizo kwa nyakati tofauti ambao pia aliwabatiza. Hali hii ya kukaa na nguo mbichi kwa muda mrefu katika baridi hatimaye iliathiri afya yake akapta vichomi. Oktoba 14 siku chache tu kabla ya Oktoba 22 ambayo alihubiri kwa msukumo mkubwa habari zake akalala mauti.

5. George Storrs, Sylvester Bliss na S.S. Snow George na Sylvester walikuwa viongozi wa kutegemewa walio simamia mafundisho ya Miller. Bliss anakumbukwa kwa historia fupi ya maisha yake aliyoshirikiana na William Miller na Joshua Himes, yeye

pia alikuwa mhariri wa gazeti lile la Dalili za mwisho wa Nyakati “Signs of the Times”.

S.S. Snow alikuwa ni kiongozi mwingine mfuasi wa Miller ambaye alisema kwamba unabii wa miaka 2300 wa Danieli 8:14 ungemalizika katika kiangazi cha mwaka 1844 badala ya wakati wa masika.

**Mabalozi wa Marejeo katika nchi zingine**

Ujumbe wa marejeo ulianza katika wakati ule ule mmoja katika Ulaya na Marekani kadiri watu wa Mungu walivyoongozwa kujifunza Unabii wa Biblia. Ni dhahiri kwamba wakristo katika nchi mbali mbali walijifunza maandiko na kufikia muafaka wa kuamini kwamba Yesu angekuja upesi, katika sura hii tutawaangalia wahubiri wa marejeo huko Ulaya na katika nchi zingine.

**1. Joseph Wolff**

Wakati ule ule ambao William Miller alipokuwa akijifunza na kujisikia kuanza kuhubiri ujumbe wa malaika wa kwanza kaskazini mwa marekani, kadhalika Wolff alianza kazi ya kuhubiri huko Ulaya. Tangu mwaka 1821 hadi 1845 Wolff alisafiri kwenda Afrika, Syria, Uajemi, India, Visiwa vya St. Helena na shirikisho la nchi za Marekani. Alihuhiri huko New York na katika miji mingine mikubwa.

Miongoni mwa wamishonari waliojulikana sana ulimwenguni kufanya safari za kimishonari na kujifunza lugha mbali mbali ni Joseph Wolff na ambaye hatimaye alijulikana kama “Mmishonari wa Ulimwengu”.

Joseph ambaye alizaliwa huko Bovania, alikuwa ni mtoto wa mwalimu wa dini wa Kiyahudi alipokuwa na umri wa miaka kumi na mmoja aliondoka nyumbani kwao ili kutafuta elimu kwa lengo la kuwa mmishonari siku za baadaye. Akabatizwa katika kanisa Katoliki lakini kipindi cha muda mfupi alikosoa mamlaka ya Kanisa katika mafundisho yake hususani yale yaliyo maagizo ya wanadamu na yasiyo na msingi wowote katika Maandiko (dogma). Wolff aliweza kuzungumza lugha mbali mbali zipatazo 14. Na aliwatemebelea wakuu wa nchi katika nchi mbalimbali alizotembelea safari zake kati Bara la Asia na Afrika zilikuwa ni safari zilizojaa hatari ambazo zizingeweza kuepukika kwa urahisi katika safari hizo amepata kupigwa, kupata dhiki hata kuuzwa kama mtumwa. Mara tatu amewahi kupata hukumu ya kifo lakini katika dhiki hizo zote na magonjwa aliendelea kupeleka ujumbe wa onyo kwa kabila nyingi lugha na jamaa kuhusu utawala wa masihi Mkuu unaokuja. Alikuwa ni Mhubiri Mkuu wa ujumbe wa Marejeo na alitumia kila nafasi iliyopatikana kutoa ujumbe juu ya hukumu ya Mungu inayokaribia na kuwaita wengi waume kwa wake kutubu na kumrejea Bwana.

**2. Johann A Bengel**

Kabla ya Wolff na Miller ujumbe wa marejeo huko Ujerumani ulifundishwa na mhubiri wa Kilutheri aliyeitwa Bengel. Aliamini kwamba mtu anaweza kuwekwa huru kiroho na hivyo akawafundisha vijana wengi ujumbe huo. Hata hivyo mvuto mkubwa wa kufahamika kwake ulitokana na vitabu vyake kuhusu marejeo ambavyo vilisomwa sehemu nyingi hadi kule Asia.

**3. Edward Irving:**

Mhubiri wa kutegemewa ujumbe wa marejeo katika Uingereza (British Isles) alikuwa ni Edward Irving ambaye mara tu baada ya kuwa Mwinjilisti wa Kiscott alianza kujitunza Unabii wa Biblia na kutoa msisitizo wa pekee kuhusu dalili za kuja kwa Yesu mara ya pili. Mlei mmoja kutoka Paris Ufaransa aliyemsikia akihubiri aliamua kumpa nakala ya kitabu cha Lacunza kuhusu "Kuja kwa Masihi katika Utukufu na enzi" (The coming of Messiah in Glory and Majesty). Irving alivutwa na ujumbe wa marejeo na hivyo akaendelea kuuhubiri kwa nguvu.

**4. Henry Drummond:**
Huyu ni mwingereza ambaye kwanza alikuwa akifanya biashara ya Benki na pia alikuwa Mbunge ambaye baadaye alijitoa maisha yake kwa huduma za Kanisa, kwa muda wa miaka kadhaa mfululizo alikuwa akiandaa mikutano mikuu ya mwaka ya Unabii. Wahubiri wapatao ishirini kutoka madhehebu mbali mbali walihudhuria miongoni mwao akiwamo Joseph Wolff. Katika mikutano hiyo Unabii wa vitabu vya Danieli na Ufunuo wa Yohana ulijadiliwa. Mikutano hii ya kujadili Unabii iliongoza mvuto mkuu wa kuhubiriwa kwa Ujumbe wa Malaika wa Kwanza huko Uingereza na sehemu nyingine za ulimwengu.

**5. Robert Winter:**
Winter aliyasikia mafundisho haya kuhusu marejeo wakati alipotembelea nchini Marekani na kuhudhuria mikutano ya makambi. Mnamo mwaka 1842 alirejea tena Uingereza ambapo sasa alijitia katika kazi ya kuhubiri ujumbe wa marejeo kwa moyo wake wote. Katika barua zake za mara kwa mara alizoziandika kwenda Marekani alikuwa akielezea maendeleo yaliyopatikana, ambapo katika barua yake moja alisema "Ninahubiri katikia mitaa na huku jedwali langu likiwa limetundikwa katika mlingoti…. Vitabu vyetu vinapeperushwa kila mahali na kutenda kazi kubwa katika miji" Mungu alibariki juhudi zake kwa kubatizwa kwa elfu kadhaa za waumini.

**6. Horatius Bonar na George Miller:**
Miongono mwa wahubiri wa marejeo huko Uingereza ni Horatius Bonar ambaye alijulikana sana kwa utunzi wa nyimbo na mwingine ni George Miller ambaye alikuwa ni Mkurugenzi wa chama cha kutoa Huduma kwa wenye shida huko Bristol.

**7. Watoto Wahubiri:**
Ili kusaidia katika kutangaza marejeo, Mungu aliwatumia hata watoto hususani huko nchini Sweden, ambako ni wahubiri wa Kanisa Kuu lililotambulika Kiserikali ndio waliokuwa na ruhusa ya kuhubiri na hivyo wakati ambapo ujumbe wa marejeo ulipofika Sweden mapema miaka ya 1840, Walei wa Kanisa hilo walikataa kuhubiri ujumbe huu wa marejeo. Ndipo watoto na vijana ambao mingoni mwao walikuwa wale wasiojua kusoma, wakahubiri ujumbe kuhusu saa ya hukumu ya Mungu pamoja na unabii kuhusu kuja kwa Kristo mara ya pili.

Mamlaka ilitumia uwezo wake wote kuwazuia vijana hawa wasiendelee na kazi yao ya kuhubiri lakini juhudi hizo zote zilikuwa bure. Mashitaka ya kudhaniwa kuwa na wazimu pamoja na magonjwa mengine ya mwili yaliadhiri wengi walitiwa nguvuni na hata wengine kupigwa. Wahubiri wawili vijana wa miaka kumi na tatu au kuzidi kidogo akina Ole Boquist na Erick Walbon walisimama kidete kuitetea kweli ya Biblia na hatimaye waliachiwa huru baada ya Mfalme kuingilia kati. Waliendelea kuhubiri ujumbe wa marejeo hadi mwaka 1844.

**8. Manuel de Lacunza**
Lacunza alikuwa mfuasi na Kuhani wa Kristo mwenye msimamo mkali ambaye alitoa nafsi yake kwa kujifunza Unabii wa Danieli na Ufunuo. Huyu alizaliwa huko Chile, lakini baadaye aliishi uhamishoni huko Hispania na Italia. Hakuwa ameridhishwa na jinsi Wakatoliki walivyotafsiri

unabii na hivyo akaamua kusoma Biblia ili aweza kutambua yeye mwenyewe. Alikuwa ni Mwana Marejeo wa mstari wa mbele katika kanisa Katoliki. Kujifunza kwake huko kulileta matokeo ya kuandikwa kwa kitabu kuja kwa Masihi katika Utukufu na enzi "The Coming of the Messiah in Glory and Majesty). Hata hivyo hakuweza kutumia jina lake mwenyewe katika kitabu hicho na hivyo aliandika kwa jina la Rabbi Juan Ben-Ezra. Pamoja na ugumu wa kazi ya kutoa nakala kwa mkono, lakini bado maandiko hayo yalienezwa mahali pengi na zaidi sana kwa kutafsiriwa katika lugha za Kilatini na Kiitalia kando ya Kiingereza ambayo ilitafsiriwa na Irving. Hivyo kazi ya Lakunza ilienea na kufahamika katika Ulaya na pia aliwapa changamoto wale wote walioisoma na kuchunguza zaidi kuhusu Marejeo.

**9. H. Heintzpeter**

Heintzpeter ambaye alikuwa ni mwangalizi wa Makumbusho huko Uholanzi alionyeshwa katika njozi kwamba kuja kwa Kristo kulikuwa kumekaribia. Na hivyo akaitangaza habari hiyo ya furaha kwa jamaa zake akitumia mafungu mbali mbali kutoka katika Maandiko kuhakikisha mambo aliyokuwa anayasema Kati ya mwaka 1830 na 1842 aliandika vijarida kadhaa kuhusu "Matukio Makuu katika Ulimwengu" (Great World Events) ambamo alieleza nuru aliyoipata kwa kujisonea yeye mwenyewe. Miaka kumi na miwili ilipita tangu aanze kazi yake ya kuchapisha mafundishoyake kabla ya kuipata elimu ya juu ya mafundisho ya William Miller.

**10. Lovis Gaussen**

Huko Ufaransa na Uswissi ujumbe wa malaika wa kwanza ulipelekwa na Louis Gausen kutoka Geneva Uswissi. Alipoianza kazi ya uhubiri alikuwa amevutiwa sana na kujifunza unabii wa Daniel na alikariri mwenyewe kwamba unabii huu ndiyo ulikuwa ufunguo wa Historia ya ulimwengu. Kwa kujifunza historia na unabii kwa pamoja hatimaye aliridhika kwamba mwisho wa dunia ulikuwa umekaribia. Mbinu aliyotumia kueneza ujumbe huu ilikuwa ni kuanza kuwafundisha watoto. Mbinu yake ilifanikiwa na hivyo watu wazima kwa mamia walikuja kusikiliza hotuba zake, hata wengine walikuja toka nchi za bali ili kumsikiliza.

## SEHEMU YA TATU

## MWANZO WA KANISA LA MASALIO 1844 - 1852

### a) Ujumbe wa Malaika wa Pili

"Kisha mwingine malaika wa pili akafuata akisema, Umeanguka, Umeanguka, Babeli, mji ule ulio mkubwa, Maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake Ufunuo 14:8.

Ujumbe wa Malaika wa pili ambao unaunganika na ule wa malaika wa kwanza, kwa mtazamo wa haraka unaweza kuonekana kama hauhusiani kabisa. Lakini katika sehemu hii tutaona uhusiano uliopo na kwanza ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili ulitolewa katika wakati muafaka. Wakati ambapo mioyo ya watu ingeupokea. Kazi ambayo Mungu aliipanga iweze kutendeka kupitia kwa ujumbe wa malaika hawa wawili ilifanikiwa barabara.

Ujumbe wa Malaika wa Pili ulihubiriwa hasa katika kipindi kile cha "kusubiri kuja kwa Kristo kati ya mwezi Machi na Oktoba, 1844.

William Miller alianza kutoa mahubiri yake ya hadhara mwaka 1831 na sauti nyingi zilisikika toka pande mbali mbali za ulimwengu zikitangaza kuja mara kwa Kristo mara ya pili. Kitovu hasa cha ujumbe wa marejeo ilikuwa ni Uingereza na pande za kaskazini Mashariki mwa Marekani.

Miller alitenda kazi kwa miaka kadhaa akiwa bila mtu aliyemuunga mkono. Mwaka 1839 hadi 1840 watu wenye mvuto na uwezo waandishi na wahubiri walianza kuyapokea mafundisho yake na kuungana naye katika kazi ya kuhubiri ambayo alikuwa amejiwekea wakfu kwayo.

**b) Mkutano Mkuu wa Biblia kuhusu Marejeo:**
Tokea mwaka 1840 hadi 1842 mlolongo wa mikutano mikuu ya kawaida ilikuwa ikifanywa kwa ajili ya wale walioamini ujumbe wa marejeo katika miji mbali mbali ya huko Uingereza. William Miller hakuweza kuhudhuria mikutano mingi iliyopita isipokuwa mmoja ambao ulifanyika katika mji karibu na kwao, ambao ulimwezesha kukutana na kuungana na wanafunzi watiifu na wenye ujuzi ambao walikuwa wamejiunga na ujumbe wa marejeo, wengi wao waliongoka kutokana na mafundisho yake na wengine kwa njia ya kujisomea wenyewe.

Viongozi wapatao mia mbili walikutanika pamoja katika mikutano hii mikuu. Jambo ambalo liliunganisha mawazo yao pamoja na kuamsha ari ya mahubiri yao, wengi wao walikuwa ni wahubiri katika makanisa ya Kiprotestanti na hao waliwakilisha madhehebu yaliyokuwa yakipendwa.

Walihubiri ujumbe wa malaika wa kwanza katika mimbari za makanisa yao, makanisa mengine, katika majukwa hadharani na katika mikutano ya makambi. Yalikuwapo majarida mengi yaliyochapishwa kuhusu ujumbe wa marejeo, lakini lililoonyesha hali ya kuwa ni chombo cha pamoja lilikuwa ni "Signs of The Times" Dalili za mwisho wa wakati. Walianzisha chama cha wana marejeo, lakini bila kubadili hali yao ya utiifu kwa kundi zima au madhehebu yao.

Mafundisho ya kawaida yaliyojadiliwa katika mikutano hiyo na baadaye kufundishwa kwa watu yanafahamika nayo ni kama ifuatayo:
- Jinsi Yesu atakavyokuja katika mawingu ya mbinguni
- Dalili za kuja kwake kama ilivyotokea katika siku giza kuu lilipotokea, kuanguka kwa vimondo na hali ya msukosuko
- Unabii wa kitabu cha Ufunuo, mwisho wa ole zile tatu na uthibitisho wake, vilivyodhihirishwa na kupoteza uhuru kwa dola ya Ottomani mnamo mwaka 1840
- Miaka 1260 ya Utawala wa Papa iliyomalizika mwaka 1798 wakati Papa alipotekwa na kutiwa gerezani
- Unabii mwingine unaohusiana na wakati
- Miaka 2300 ya Danieli 8:14
- Kipindi kabla ya miaka elfu (premillennial)
-

**Jinsi ilivyotafsiri kuhusu kuja kwa Kristo, mnamo mwaka 1843.**

Pamoja na upinzani uliokuwa ukitolewa hasa kuhusu kuhubiriwa kwa ujumbe wa kurudi kwa Kristo, wafuasi wa Miller walifanikiwa kuhubiri na kujenga mahusiano mema miongoni mwa

madhehebu mbali mbali.  Wengi wa wasioamini walioongoka na mauzo ya Biblia yaliyoongezeka kwa ghafla.

Katika kiangazi cha mwaka 1842 Charles Fitch alichapisha hubiri lake moja ambalo alikuwa amelitoa siku zile kwa kutumia mafungu ya Ufunuo 14:8 na 18:2-4 kwa makanisa ya Kilutheri na Kiroma, alisema kwamba namna hizo zote mbili za ukristo ni babeli na wameanguka kwa kuacha kufuata ujumbe wa kurudi kwa Kristo mara ya pili.  Kulikuwa na sababu nzuri ya kutoa tafsiri hii kwa sababu mpaka wakati huu, makanisa mengi yalikuwa yamezika ujumbe wa marejeo na wahubiri wake.

Katika kiangazi hicho cha mwa ka 1843 ndipo wahubiri waliwekewa mikono na kundi la wafuasi wa William Miller ili  kuhubiri ujumbe wa marejeo.  Vile vile katika gazeti kuhusu dalili za mwisho wa wakati "Signs of the times" waumini walishauriwa kujitenga kutoka katika makundi yao, washiriki wa makanisa waliambiwa na viongozi wao kwamba wabadili imani zao katika kipindi kile cha kusubiri marejeo au sivyo wajitoe katika ushirika wa makanisa yao. Mfano halisi ni ile habari ya familia ya Harmon; Ellen White anaelezea uzoefu wa jamaa yake mwenyewe katika kitabu chake cha Life Sketches ukurasa 50 – 53.

Aya inayotoa hitimisho la habari hiyo inasomeka "Jumapili iliyofuata mwanzoni mwa sikukuu ya mapendo, Kiongozi aliyekuwa madarakani alitangaza kufuatwa kwa majina yetu, jumla ya watu saba kutoka ushirika wa kanisa".

Wakati ambapo miongoni mwa wahubiri wa ujumbe wa marejeo walipoanza kutumia neno "Babeli: waziwazi kumaanisha makanisa yale yanayokataa mafundisho juu ya hukumu ya mwisho na kuja mara ya pili kwa Kristo ndipo ujumbe wa malaika wa pili unapounganika na ule wa malaika wa akwanza.  Mada yenye kichwa "Umeanguka Babeli Mkuu"  (Bablon the Great is fallen) ilichapishwa huko Oswego, New York.  Ndipo mnamo majira ya kiangazi ya mwaka 1844, zaidi ya waumini elfu hamsini walijitenga kutoka katika makanisa yao na kuanzisha vikundi vyao.

**c)  Kilio cha usiku wa manane**

William Miller pamoja na wengine walijaribu kutafuta kujua muda halisi wa mwisho wa siku 23000 za Unabii.  Mwanzoni walisema kwamba ingekuwa ni "Mwaka 1843" lakini baadaye viwango vya muda viliwekwa ambavyo vilipenya machi 21 na baadaye aprili 18, 1844, ambao ndio mwisho wa mwaka 1843 wa Kiyahudi.  Muda huo ulipita bila tukio lolote lisilo la kawaida. Katika hali hii ya kukatisha tamaa lilikuwa ni pigo kubwa kwa waumini na lilifuatiwa na kipindi cha ukimya, wakati wa "kuchelewa mno" kama ambavyo ilitokea katika mfano wa wanawali kumi na kufafanuliwa baadaye.

Baada ya tukio la hali ya kukata tama, watafiti wa unabii wa marejeo walivirejea tena vitabu vyao na kugundua makosa waliyofanya katika kutafsiri unabii unaohusu miaka 2300, kwamba unabii huu ungepaswa kujumuisha miaka ya 457 K.K. na 1843.  Hivyo matukio yaliyotokea katika mwaka 457 yangehusianishwa katika unabii katika muda ule ule yaani 1844.  Jambo hili liligunduliwa mwaka mmoja kabla ya 1844; lakini ugunduzi huo haukuzingatiwa.  Mnamo kiangazi cha mwaka 1844 nuru mpya iliwatokea ambayo iliwaangaza wana marejeo hawa na kufikia kilele chake mwezi Oktoba.

Katika mkutano wa makambi wa mwezi Agosti huko Hampshire. Joseph Bates alihisi kwamba angeweza kupata nuru mpya. Alimkaribisha Samwel S. Snow kutoa fundisho lake kuhusu "Kilio cha Usiku wa Manane". Samweli aliendelea kutoa mafundisho kila siku mpaka mkutano ulipokoma, watu walichomwa mioyo yao kwa mfano wa Wanawali Kumi jinsi ulivyoonekana kuyahusu maisha yao. Aliendelea kueleza kwamba wanamarejeo walitarajia kwamba Bwana angerudi katika wakati wa masika ya mwaka ule lakini walilazimishwa kusubiri. Unabii wa siku 2300 ungekoma katika kipindi cha masika ya mwaka 1844 (ambao ndio mwisho wa mwaka 1843 wa Kiyahudi). Kama tangazo la Artashasta, Mfalme lingekuwa likitolewa katika siku ya kwanza ya mwaka wa Kiyahudi wa 457 K.K. Hivyo kwa vile tangazo hilo halikutolewa mwanzoni mwa mwaka na badala yake mwishoni mwa mwaka 457 K.K, basi ni dhahiri kwamba mwishoni mwa mwaka 1844.

Kujifunza kwa undani juu ya hekalu na huduma zake kulidhihirisha kwamba kutakaswa kwa Hekalu kulifanyika katika siku ya kumi ya mwezi wa saba. Jambo ambalo hupatana na wazo kwamba siku 2300 zingemalizika mwishoni mwa mwaka. Kwa kuwa siku ya kumi ya mwezi wa saba (wa Kiyahudi) katika mwaka 1844 ingetimia Oktoba 22.

Katika mfano wa wanawali kumi, kilio kilisikika usiku wa manane. Wakati kiangazi kikiwa kimeshamiri, ujumbe wa Samweli Snow ulionekana kushabihiana na "Kilio cha Usiku wa Manane". Uhalisi wa ukweli ulivuta mioyo ya watu na hivyo baada ya mkutano ule wa makambi waliondoka kwa furaha wakizitangaza habari hizi njema katika sehemu mbalimbali. "Tazameni, Bwana arusi anakuja, tokeni twende tukamlaki". "Kilio cha Usiku wa Manane" kilisikika wakati wa subira ya "Kuchelewa mno".

Wana marejeo wapatao 50,000 walivutiwa sana kwamba Bwana angerudi na hivyo wengi wao wakaacha kutayarisha mashamba yao ili kupanda mazao kwa sababu walidhani kwamba angekuja kabla msimu wa mavuno mengine kufikia.

**Waliutumia muda wao kutangaza mbiu ya kuja kwa Kristo mara ya pili.**

**d) Hali ya kukata tamaa**

Kadiri Oktoba 22, 1844 ilivyozidi kukaribia, hali ya wasiwasi ilizidi kuongezeka miongoni mwa Waadventista walikuwepo maelfu miongoni mwao ambao hawakujishughulisha kabisa. Walisimama kando kama watazamaji. Magazeti yalichapisha habari zenye kusisimua kuhusu mafundishi ya Miller. Hata hivyo, taarifa kuhusu waaminifu zilionyesha kwamba makundi ya Waadventista ndiyo waliokuwa waaminifu, wenye kujitoa, watulivu na wenye nia thabiti.

Yalikuwepo madaraja kadhaa ya watu miongoni mwa wale walioamini ujumbe wa marejeo. Wengine walijiunga kwa sababu ya woga, wengine waliikataa tarehe iliyokuwa imetajwa, kwa mfano William Miller mwenyewe ambaye hakukubali hadi majuma machache tu kabla ya Oktoba 22. Walikuwepo waumini waaminifu ambao wengi miongoni mwao waliikubali tarehe hiyo na hivyo walijitayarisha kikamilifu kukutana na Yesu.

Siku iliwadia Waadventista walikuwa katika majumba ya mikutano au nyumba zao binafsi, waliimba nyimbo za sifa na kurudia mafundisho yaliyothibitisha kwamba Kristo angekuja, siku ilipita pamoja na machweo yake, lakini tumaini bado lilikuwapo. "Kwa maana hamjui siku ajapo mwenye nyumba kwamba ni jioni au usiku au awikapo jimbi au pengine ni asubuhi". Hatimaye usiku ule ukapita. Maombi mengi yaitolewa na machozi yalijaza macho ya baadhi ya

waumini, walishikwa na simanzi huku wakiulizana. "Je Maandiko hayakuwa kweli. "Baadaye walipojifunza kwa makini zaidi waligundua kwamba muda wa unabii ulioelezwa ulikuwa sahihi, lakini tukio ambalo lingepaswa kutokea ndilo lilitafsiriwa kimakosa.

Hiram Edson alisema "Yuko Mungu wa mbinguni ambaye amejifunua kwetu kwa njia ya mibaraka katika kusamehe, kuokoa na hivyo hawezi kushindwa. Baada ya muda usiokuwa mrefu siri hii itafunuliwa.

Wengi wa wafuasi wa Miller waliiacha imani yao baada ya hali ile ya kukatisha tamaa, ijapoikuwa vikundi vidogo vidogo viliendelea kuwa na mshikamano kwa miaka kadhaa. Hatimaye William Miller alifariki mnamo mwezi Disemba 1849. Miongoni mwa washiriki wake waliendelea kupanga tarehe mpya kwa miaka kadhaa baadaye. Mwishoni walitambulika kama Wainjilisti wa Kiadventista na waliamini juu ya hali ya wafu kwamba hawana fahamu na kwamba kuna moto wa milele huko kuzimu; ambao pole pole hupungua hadi kuzimika kabisa. Kundi jingine ambalo liliamini juu ya hali ya wafu kutojua neno lolote ambalo pia waliendelea kuitunza Jumapili, walipewa jina la Wakristo wa Marejeo. Kanisa lao bado lipo hata sasa. Yalikuwapo makundi mengine kadhaa yaliyokuwa na mawazo tofauti ambayo miongoni mwao walijiingiza katika hali ya kuongozwa na misisimko. Tungependa kuelewa zaidi kuhusu makundi hayo pamoja na habari kuwahusu Hiram Edson. Joseph Bates, James White na Ellen Harmon ambao ndio waliokuwa kitovu cha Kanisa la Masalio. (James na Ellen waliunganishwa kwa ndoa Agosti 31, 1846).

Wale wote waliokuwa ndio kitovu kwa pamoja walishiriki uchungu wa kuumwa mioyo wakati ule wa kukatishwa tamaa pamoja na waumini wengine.

Wengi wa wale ambao siku ile walikuwa wamekusanyika katika nyumba ya edsom katika shamba lake walirejea makwao kwa huzuni kubwa asubuhi ile ya Oktoba 23. Edson na rafiki zake wa karibu walikwenda mahali pao walipopatenga kwa maombi ili waweze kuomba na hilo ndilo liliwatia nguvu kwamba Bwana angewaonyesha njia.

Baada ya kifungua kinywa Edson alimwambia mmoja wa waumini aliyekuwa amebakia "Hebu na twende tukawafariji wapendwa wetu kwa uhakikisho huu "Wote wawili wakatembea mle shambani ambamo nafaka zake zilikuwa bado. Walitembea kwa utulivu huku wakiwa na mioyo yenye kutafakari. Kuhusu hali ya kukata tama iliyowapata. Karibu na katikati ya shamba, Edson alisimama ghafla. Alionekana kana kwamba alikuwa analiona Hekalu la mbinguni na Kristo kama Kuhani Mkuu akiondoka patakatifu pa Hekalu la mbinguni na kuingia Patakatifu mno.

"Niliona dhahiri na waziwazi" Edson anaandika "Badala ya Kuhani wetu Mkuu kuondoka kutoka Patakatifu mno pa hekalu la mbinguni, kuja duniani katika siku ya kumi ya mwezi wa saba, mwishoni mwa siku 2300, kumbe ndio kwa mara ya kwanza alikuwa anaingia katika chumba kile cha pili cha hekalu la mbinguni yaani Patakatifu pa Patakatifu. Na kwamba alikuwa na kazi maalum ya kufanya katika kile chumba cha pili cha patakatifu Mno. Kabla ya kurejea tena katika dunia hii". Kutakaswa huku kwa hekalu kuliashiria kuanza kwa hukumu ya upelelezi.

Mwenzake alikuwa tayari ameshafika mwisho wa shamba na hivyo alipogeuka na kumwona Edson akiwa mbali alimwita na kumwuliza ni jambo gani ambalo lilimkawiza nyuma peke yake

Edson naye alijibu. "Ni Bwana ambaye alikuwa akijibu maombi yetu ya asubuhi" na hivyo akamweleza juu ya nuru mpya aliyokuwa ameipata.

Nuru ile waliyoipata pale shambani iliwaongoza wao pamoja na wenzao katika kujifunza kwa bidii juu ya huduma zilizotolewa katika hekalu kwa wana wa Israeli pamoja na umuhimu wa mafundisho juu ya siku 23000. Hivyo wakachapisha makala juu ya mambo hayo katika moja ya magazeti yaliyokuwa yakieleza kuhusu Marejeo na Hiram Edson akaitisha mkutano mkuu mwishoni mwa mwaka 1845.

Hivyo ile siri sasa ikawa imefunuliwa na muda ikawa dhahiri. Na ujumbe wa malaika wa kwanza ukaendelea kuhubiriwa kuwa ndio ukweli wa wakati huo. Yalikuwa na bado ni mafundisho yenye nguvu kuwabadili wenye dhambi kumgeukia Kristo katika saa hii ya hukumu. Umuhimu wa ujumbe wa malaika wa pili ulichukua nafasi yake mara tu baada ya kipindi kile cha "Kukata Tamaa" na umeendelea kuwa na umuhimu mkubwa katika zama zilizofuata baadaye.

**e) Kuanza kwa ujumbe wa malaika wa tatu:**

Kujifunza juu ya hekalu ulikuwa ndio ufunguo kwa ile siri ya wakati wa kukatisha tamaa. Pia ilikuwa ni ufunguo kwa mafundisho ya kiini ya ujumbe wa malaika wa tatu ambao hutuelekeza kwenye sheria ya Mungu hususani kwa matokeo ya uasi.

Upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya ujumbe huu na sabato ambayo ndiyo kiini cha sheria ya Mungu. Ni katika nuru ambayo Mungu aliwapa wale waumini wa kwanza juu ya ukweli wa Sabato ambapo alikuwa akiitayarisha dunia kwa ujumbe wa mwisho

"Wakati ule wa kilio cha usiku wa manane, mwaka 1844 Mama Rachel Oakes (ambaye baadaye aliitwa Preston) ambaye alikuwa Mbaptisti aliyetunza siku ya saba alitembelea Washington na Hampshire ambako binti yake alikuwa akiishi ambaye pia aliamini ujumbe wa marejeo. Mama Oakes alikuwa ni muumini aliyekubali Sabato kama inavyoelezwa katika Biblia na hivyo alikuwa amekuja na vijizuu vyenye ukweli huu. Hivyo mara alikubali mafundisho ya ujumbe wa marejeo na kuendelea kuitunza Sabato. Vijizuu vile alivyovigawa kimya kimya vikazaa matunda.

Asubuhi moja katika ibada za Jumapili mwanamarejeo mmoja alisimama na kusema alikuwa ameridhika kabisa kwamba siku ya saba ilikuwa ndiyo Sabato ya kweli iliyofundishwa na Biblia na kwamba yeye mweneyewe alikuwa amekata shauri kuitunza. Wengi weingine pia walionyesha kuamini hivyo na hivyo katika muda wa siku chache kundi zima la waumini arobaini wakawa ni watunzaji wa Sabato.

Hivyo huo ndio ukawa mwanzo na kwamba Washington. New Hampshire ndipo Kanisa la kwanza la Waadventista wa Sabato lilipoanza. Japokuwa kanisa hili lilikuwa limeanzishwa siku nyingi zilizopita.

Mhubiri wa kwanza kuukubali ukweli wa Sabato alikuwa ni Frederick Wheeler kutoka kundi la kule Washington. Hapo kwanza alikuwa ni mhubiri wa madhehebu ya Wamethodisti na mshiriki wa William Miller.

Si Waadventista wote ambao walikuwa wakiitunza Sabato katika mwaka 1844. Waadventista kama kundi walisukumwa kuujua ukweli wa Sabato kupitia kwa makala kuhusu mada hiyo iliyotolewa na T.M. Preble

na kuchapishwa katika gazeti huko Portland, Maine, mwanzoni mwa mwaka 1845 J.B. Cook naye pia aliandika makala yake ambayo ilitolewa muda ufupi baadaye na kuchapishwa. Katika makala hii alitoa hitimisho kwamba hakuna uthibitisho wowote kutoka katika Maandiko unaoonyesha kwamba tunapaswa kuitunza Jumapili kama Sabato ya siku ya Saba. Tangu hapo ujumbe kuhusu Sabato ulianza na kuendelea kwa nguvu na hivyo haikuwa rahisi kuunyamazisha.

Baada ya kusikia mambo yalivyokuwa yakiendelea huko Washington. New Hampshire kwamba wenzi wao walikuwa wakiitunza Sabato, Joseph Bates aliamua kuwatembelea ili aweze kujua nini hasa maana ya mambo yote aliyosikia habari zake. Akaenda mpaka New Hampshire na kujifunza juu ya mada hiyo na kutambua kwamba mawazo yao yalikuwa sahihi na hivyo akaikubali nuru ile. Alipokuwa akirejea nyumbani alikutana na rafiki yake Hall katika daraja lililokuwapo kati ya New Bedford na Fairheaven ambaye alimsalimu na kumuuliza kulikuwa na habari gani huko. Naye Bates alijibu, habari ni kwamba, siku ya Saba ndiyo Sabato ya Bwana Mungu Wetu". Bwana Hall alijibu kwamba angekwenda nyumbani kwake na kuisoma Biblia ili kuchunguza juu ya jambo hili. Naye alifanya kama alivyoahidi. Alipokutana na Bates kwa mara ya pili alikuwa tayari ameshaukubali ukweli wa Sabato na kuanza kuitunza. (The Great Adventist Movement pp. 39/40)

Japokuwa ukweli wa Sabato ya siku ya Saba ulifunuliwa tena mwaka 1844, lakini kumekuwa na watu waliotunza Sabato tangu mwanzo wa wakati. Hata katika zama za giza makundi mbali mbali ya watu waliitunza Sabato ya siku ya Saba. Wabaptisti wa siku ya Saba ambayo ndiyo Amri nne: kwa karne kadhaa kama tulivyoona kwamba hatimaye Waadventista kwa mara ya kwanza, walijifunza juu ya Sabato ya Kweli kutoka kwao.

**f) Mkutano Mkuu kuhusu Sabato**

Baada ya muda mfupi mafundisho juu ya Sabato ya siku ya Saba ikawa ndiyo kigezo kwa wote ambao wangependa kujiunga na Waadventista wanaotunza Sabato.

Kwa kusoma makala moja tu ilitosha kumshawishi Joseph Bates, Hiram Edson naye pia akaupokea ujumbe huu wa Sabato ya kweli Frederick wheeler na William Farnsworth walihitaji kupewa utangulizi tu juu ya mada hii na muda kidogo wa kujifunza, katika muda mfupi nao wakawa ni watunzaji wa Sabato. James na Ellen White kwa mara ya kwanza hawakuvutiwa wala kuona umuhimu wa mafundisho kuhusu Sabato. Baada ya James na Ellen kuona waliweza kusoma kitini kilichochapishwa na Bates, nao pia wakaikubali Sabato.

Hata hivyo, kipindi hiki kilikuwa ni kigumu sana kwa viongozi kwa kuwa hakukuwa na umoja na hali ya kukubaliana katika mafundisho. Kwa uwezo wa Mungu mikutano mikuu kadhaa iliweza kufanyika katika nyakati zile. Waumini walijifunza Maandiko kwa bidii sana na kwa kulinganisha fungu moja na jingine waliweza kutambua ukweli wa mafundisho ya Biblia. Mikutano hiyo yote kwa jumla ilikuwa sita katika mwaka 1848. Ellen White alichukua sehemu muhimu sana katika mikutano hiyo.

**g) Zawadi ya Mungu kwa Kanisa la Masalio**

Mtume Yohana katika njozi zake alipokuwa kule kisiwani patmo, alionyeshwa katika mfano vipindi vikuu vya historia ya ulimwengu. Kwa hadiri Yohana alivyoangalia kwa makini mambo yatakayokuwa, aliweza kuona watu waaminifu kwa Mungu karibu kabisa na mwisho wa wakati, na aliweza kubaini kwamba Kanisa hili lilitunza amri za Mungu. Alionyeshwa vile vile kwamba liliongozwa kwa nuru Takatifu ya pekee kwa njia ya Roho ya Unabii". Kwa maana Ushuhuda wa Yesu ndiyo Roho ya Unabii. Ufunuo 19:10 (The Story of our Church p. 186).

Tangu mwanzo kabisa, Mungu amedumisha mawasiliano yake na kanisa lake. Uongozi wake haukuwa dhahiri siku zote kama zamani za wana wa Israeli ambapo mchana walifunikwa kwa wingu na usiku waliongozwa kwa nguzo ya Moto. Bali watu wake wamejulishwa juu ya kuwako kwa Mungu. Njia kuu ya mawasiliano kati ya Mungu na watu wake imedumu kuwa kupitia kwa "Watumishi wake Manabii" Kama ilivyotabiriwa katika Ufunuo 12:17 na 19:10 kwamba Kanisa la Masalio litakuwa na Karama ya Unabii.

Mnamo January 1842 William Foy ambaye alikuwa ni Mbaptisti kutoka Boston na ambaye baadaye ndiye aliyeandaa huduma ya Kiaskofu, alipewa njozi kuhusu nchi mpya waliokombolewa wakiongozwa kwa mpangilio wenye utukufu kama ule wa mbinguni. Njozi inayofanana ilimrudia tena katika mwezi Februari, ambayo sasa ilikuwa ni maelekezo dhahiri kabisa ya jinsi ya kufanya. Siku tatu baadaye alipingana na nafsi yake juu ya kuieleza kwa watu hatimaye akaazimu kuilinganisha njozi ile na nyingine katika mkutano mkubwa kule Boston.

Baada ya kusafiri sana akiwa na ujumbe wake alipata njozi nyingine ya tatu na hii ilitokea siku chache tu kabla ya ule wakati wa kukatisha tama. Elimu mpya aliipata sasa ambapo alionyeshwa majukwaa matatu, ambayo yalionyesha awamu ya tatu ya ujumbe toka kwa Mungu kwa ajili ya nyakati zile. Katika hali ya kuchanganyikiwa, alikoma kutoa mahubiri ya hadhara na muda mfupi baadaye alikufa. Hata hivyo hakuna uhakikisho wowote kwamba alifanya dhambi kwa kutohusianisha njozi hii na zile za mwanzo.

Hazen foss, kijana mwanamarejeo mwenye kipaji cha pekee kutoka Poland Maine, alipata njozi siku chache tu kabla ya ule wakati wa kukatisha tama. Njozi hiyo ilihusisha pia majukumu matatu aliyoonyeshwa Foy katika njozi yake. Mapema Foss alikuwa ameshatahadharishwa juu ya ugumu ambao angekabiliana nao yeye binafsi kama mjumbe wa Bwana, pamoja na kuhusianisha njozi yake na mambo halisi. Kwa sababu ya kuogopa dharau za watu hakuweza kuutangaza ujumbe huu. Njozi hiyo ilirudiwa tena kwa msisitizo na maonyo kwamba kama angeendelea kukataa karana hiyo, ingepokonywa kutoka kwake. Kwa kuwa aliendelea kukataa njozi ya tatu ilimrudia tena ambayo ilimweleza kwamba Karana hiyo ilikuwa imetoka kwake na kupewa mtu aliyekuwa dhaifu sana. Japokuwa aliishi mpaka mwaka 1893, hakuweza kupata tena nguvu na mvuto kwa mambo ya dini.

Ellen Harmon alikuwa ndiye mtu wa tatu kuchaguliwa na Bwana ili kuwa mjumbe wa Masalio. Mwezi Disemba 1844, miezi miwili tu baada ya wakati wa kukatisha tama, wakati ambapo sauti ya Mungu yenye uhakika ilipohitajika kutoka mbinguni kwa ajili ya watu walioamini juu ya Marejeo. Mungu alimwonyesha njozi Ellen, binti aliyekuwa na miaka kumi na saba tu.

Kwa jumla na ufupi kwa namna ya mfano, Mungu alimwonyesha jinsi kanisa litakavyokuwa katika siku za usoni.

Alionyeshwa jinsi mambo ambayo yangetokeo kuanzia Oktoba 22, 1844. Kupitia katika zama zote hadi wateule watakapoingia katika Yerusalemu Mpya. Alionyeshwa pia kwamba kuja mara ya pili hakukuwa karibu sana kama walivyotumaini. Utukufu wa mbinguni ulionekana kuwa halisi kabisa kwa Ellen wakati alipokuwa katika njozi. Lakini mara tu baada ya kuzinduka kutoka katika hali ya njozi hakuona kitu chochote, mambo yote yalikuwa kama usiku wa giza kwake. Alilia kwa uchungu alipogundua kwamba mambo aliyoonyeshwa yalikuwa njozi tu; alikuwa na hamu ya kufika mbinguni kiasi cha kuugua.

Baada ya muda wa takribani juma moja tangu alipopata njozi ya kwanza, alipata mafunuo kwa mara ya pili, ambayo yalimwagiza kwamba ilimlazimu kwenda kila mahali na kuwaeleza watu juu ya ujumbe huu wa Mungu ambao ulikuwa umefunuliwa kwake. Vile vile alionyeshwa adha ambayo ilikuwa ikimkabili.

Katika njozi yake ya kwanza, Ellen Harmon alionyeshwa njozi ile ile ambayo ilikuwa imeonyeshwa kwa Foss na Foy. Njozi ambayo ilionyesha safari ya watu wa Mungu kuelekea katika ufalme wa mbinguni. Katika kanisa la mwanzo la Waadventista, kila mshiriki alipaswa kuamua mwenyewe binafsi kuamini au kutoamini kwamba ujumbe uliotolewa na Ellen Harmon ulitoka kwa Mungu. Kadhalika mtu yeyote anayejiunga na Kanisa la Waadventista wa Sabato leo hana budi kuamua yeye mweneyewe binafsi kwamba mambo aliyoyasema ni ya hakika au la. Hususani, pale alipoliweka bayana jambo hili kwamba Mungu alikuwa amemwita kuwa mjumbe wake.

Hata hivyo, hatujaachwa mashakani kwa sababu Biblia imeweka vigezo muhimu ambavyo kwavyo twaweza kujaribu na kuhakikisha madai yaliyotolewa katika maandiko ya Ellen White kwamba yeye ni miongoni mwa manabii wa Mungu. Vipo vigezo vine vilivyo dhahiri katika Biblia ambavyo katika vigezo hivyo vyote, Ellen White anafuzu kama Nabii kwa kuzingatia maisha na kazi zake (Jifunze vigezo vinne na majaribio)

1. “Na waende kwa sheria na ushuhuda, ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi” (Isaya 8:20)
   Maneno yaliyotolewa na nabii yasipingane na yale yaliyotolewa kuwa ushuhuda kwa kanisa pamoja na mafundisho ya Biblia. Maandiko ya Ellen White, daima huiinua na kukuza Biblia kama kitabu cha pekee.

2. “Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua” (Mathayo 7:20)
   Shule ya Sabato, Elimu ya Kikristo, kuishi kiafya, kazi ya uchapaji ni machache ya matunda yaliyoletwa kanisani kutokana na kufuata mashauri yaliyotolewa na mjumbe wa Bwana-Ellen. Kwa muda wa miaka zaidi ya sabini amedumu kuwa mkristo mwaminifu, mwenye hekima na Kiongozi wa kutegemewa. Alijitoa maisha yake kwa kazi ya Mungu na kamwe hakutafuta madaraka au utajiri.

3. “Nabii atabiripo habari za amani, neno la nabii yule litakapotokea, ndipo Nabii yule atakapojulikana kuwa Bwana amemtuma kweli kweli” (Yeremia 28:9) Wapo Manabii wengi katika Biblia na pia wapo watu wengi katika maandiko waliotajwa kuwa ni Manabii ambao hawakutabiri jambo lolote. Hata hivyo nabii wa kweli abashiripo mambo ya siku zijazo ni lazima yatimie. Mnamo mwaka 1848 alitabiri kwamba kazi ya uchapaji ingeanzishwa kwa kuchapisha vijizuu na kwamba baadaye ingekua na kuwa nuru kuu itakayoenea ulimwenguni mwote. Leo Kanisa la Waadventista linamiliki zaidi ya viwanda vya uchapaji 50. Upo utabiri

mwingine mwingi ambao umetimia miongoni mwao ukiwa ni ule ulioeleza kwamba Kansa ni virusi na pia kwamba ulimwengu mzima utahusika na vita vya upotevu wa meli na vyombo vingine vya majini na mambo hayo yote yatahusisha upotevu wa mamilioni ya maisha ya watu. Mambo ambayo yanabainisha maneno yake kuwa kweli.

4. Kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu (1Yohana 4:2) Vitabu (The Desire of Ages) Tumaini la Vizazi Vyote, Thoughts from The Mount of Blessing( Mlima wa Baraka) na (Christ in Object Lessons) vielelezo vya Ushindi, ni ushahidi uliodhahiri kuonyesha kwamba Ellen White alimkiri Yesu kwamba ni Mungu.

Kwa muda wa miaka mingi maadui wamekuwa wakimpinga vikali Mama White pamoja na madai yake kuhusu ufunuo aliopewa na Mungu. Kazi zao zimejengwa katika msingi wa kijicho, kuvuruga ukweli pamoja na uongo. Ni dhahiri kwamba upinzani wa jinsi hii ungetazamiwa. Hata hivyo zaidi ya magombo sitini na maelfu ya makala katika magazeti vinaendelea kutia ushuhuda kazi takatifu ya Dada White.

Historia ya kanisa imezingwa ndani ya uongozi wa karama ya unabii. Kila wakati ambapo kanisa limefuata mashauri kutoka kwa Bwana, limepata ushindi kama ilivyo ahadi yake. Hapo chini ipo orodha ya baadhi ya ukweli kuhusu maisha na kazi zake.

1. Ellen Gould Harom alizaliwa Novemba 26, 1827 shambani kwa baba yake huko Gorham. Maine, kadiri ya maili kumi na mbili (Km. 22) magharibi mwa Portland. Akiwa na dada yake ambaye alikuwa pacha wake na hivyo yeye alikuwa ndiye mdogo katika familia ya watoto nane. Alikuwa ni motto wa kawaida tu, mwenye furaha na mwenye mvuto wa kina katika mambo ya dini, ambao aliurithi kutoka kwa wazazi wake wacha Mungu.

2. Kilele cha maendeleo ya maisha yake kilikuwa katika siku moja alipokuwa akivuka barabara alipopigwa na jiwe la uso lililokuwa limetupwa na msichana mwingine. Pua yake iliharibiwa kabisa na uso wake ulipoteza sura yake ya kawaida. Alipoteza fahamu kwa majuma matatu hivyo mshtuko huo wa mishipa ya fahamu ulimfanya kuwa dhaifu kwa muda mrefu. Juhudi za kuendelea kusoma zilififia, japo alifanikiwa kuendelea tena na masomo lakini baadaye ilimlazimu kuacha mipango yote ya masomo kutokana na afya yake kuwa mbaya.

3. Katika miaka ya 1840 na 1842, Ellen Harmon pamoja na familia yake walisikiliza hotuba za William Miller kuhusu Marejeo ya Kristo, wakayakubali mafundisho hayo huku wakiendelea kuwa wafuasi wa madhehebu ya Kimethodisti. Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa Ellen White kufanya maamuzi yoyote maana katika wakati huu Ellen White alipitia kipindi kigumu cha kiroho cha kufanya maamuzi. Katika mkutano mmoja wa makambi mwishoni mwa mwaka 1840, alitoa maisha yake kwa Mungu na hivyo moyo wake uliokuwa na simanzi ukatulia. Tangu wakati huo alianza uhusiano mpya na Bwana.

4. Familia yake ilikuwa ni miongoni mwa familia zile zilizokuwa zimepokea “Kilio cha usiku wa Manane”. Kutokana na kuyaacha makanisa yaliyoasi, walikuwa ni

miongoni mwa wale waliopata uzoefu wa uchungu wa usiku ule wa kukatisha tama lakini wakaendelea kuwa imara katika ujumbe wa marejeo.

5. Njozi yake ya kwanza aliipata kipindi kifupi baada ya kule kukata tamaa kukua na alionyeshwa maendeleo ya watu wa Mungu kuelekea mbinguni. Kadiri alivyotafakari juu ya ujana wake (alikuwa na umri wa miaka 17 (kumi na saba tu) hali yake ya aibu, afya mbaya na mambo magumu ambayo angeyakabili, alimwomba Mungu kwa unyenyekevu kwamba amuepushie jukumu lile la kumfanya mjumbe wake pamoja na maombi hayo, mwito wake haukubadilishwa hatimaye akatoa ukubali wake wa kwenda na kutenda kama Mungu atakavyomwagiza.

6. Mnamo mwezi April 1847, alipata njozi kuhusu Sabato. Alionyeshwa Hekalu la mbinguni na Yesu akafungua mlango, ndani yake aliziona Amri kumi, Amri ya nne ilikuwa imezungukwa na nuru ya pekee ya utukufu na pia akamsikia malaika akithibitisha umuhimu wake. Alionyeshwa kwamba kama Sabato ingetunzwa siku zote, basi kusingekuwa na uasi au imani kuhusu kutokuwako kwa Mungu na hivyo dunia isingejiingiza katika ibada ya sanamu. Njozi hii ilifunua uhusiano uliopo kati ya Sabato na ujumbe wa malaika wa tatu. Waumini walioona umuhimu halisi wa hekalu, mafundisho kuhusu Sabato na kuja kwa Yesu mara ya pili yalikuwa ndiyo mwongozo wa Kanisa la Waadventista. (Soma Life Sketches pp. 95,96).

7. Kwa muda wa miaka sabini iliyofuata kazi yake ilikuwa ni kupokea maelekezo toka kwa Mungu na kuwapa watu wake. Aliwahutubia watu wengi na kuandika vitabu zaidi ya 40 (ambavyo baadaye vimejulikana kama “Roho yaUnabii”) ambavyo vilitoa mchango mkubwa katika makala nyingi za Maandiko ya Waadventista wa siku ya Saba. Miongoni mwa vitabu vilivyofahamika na kupendwa sana ni kile kinachoeleza hahari za maisha ya Yesu “Tumaini la vizazi vyote” (The Desire of Ages). Alisafiri mahali pengi zaidi ya Marekani ya Kaskazini, pande za Ulaya, hadi Australia na New Zeland ambako mashauri yake yalitumika kama msingi wa kuanzisha kazi ya Mungu. Mawazo yake yalitoa mchango mkubwa wa kuanzishwa chuo cha Avondale kule Australia.

8. Ujumbe wote ambao Ellen White aliupokea toka kwa Mungu aliupata kwa njia ya maono. Wakati wa maono hayo ilionyesha dhahiri kwamba alikuwa chini ya uongozi wa Mungu. Alionekana kana kwamba alikuwa akiangalia kitu fulani kilichokuwa mbali sana, hakuweza kupumua kwa wakati wote, lakini mwili wake haukubadilika rangi na wala mapigo ya kuonyesha msukumo wa damu hayakushindwa. Ushuhuda kutoka kwa watu mbali mbali waliomwona wakiwamo madaktari. Walihakikisha kwamba jambo hilona yote yaliyotendeka yalikuwa si mambo ya dunia tu. F.C. Castle ambaye alishuhudia uchunguzi wa madaktari alisema “Mshumaa unaowaka uliwemwa karibu na macho yake ambayo yalikuwa hayakufumbwa na hakuna hata msuli mmoja uliotokisika, kasha alifanyiwa uchunguzi kuhusiana na mapigo ya moyo na pumzi, ilihakikishwa kwamba hakupumua kabisa.

Matokeo yake ni kwamba kila mtu aliridhika kwamba wasingeweza kuwajibika kwa mambo ya kanuni ya sayansi ya asili.

Mwanamke huyo dhaifu wa afya alionekana kuwa mwenye nguvu na imara akiwa katika maono, wakati mmoja akiwa katika maono alikuwa ameshika Biblia kubwa yenye uzito wa paundi 18 (kg. 8) katika mkono wake wa kushoto ulionyeshwa kwa muda wa nusu saa.

9. Miaka saba baada ya kupata njozi ya kwanza alichapisha kitabu chake cha kwanza, kigazeti cha kurasa 64 ambacho sasa huunda sehemu ya kwanza ya kitabu "Early Writings" Maandiko ya Ellen White huitwa "Maandiko ya Roho ya Unabii" Miongoni mwa vitabu alivyoviandika unavyopaswa kuvifahamu na kujifunza ni kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1855 - 1909 | Testimonies for the Church (9 volumes) |
| 1882 | Early Writings |
| 1888 | The Great Controversy |
| 1890 | Patriarchs and Prophets |
| 1892 | Steps to Christ |
| 1896 | Thoughts from the Mount of Blessing |
| 1898 | The Desire of Ages |
| 1900 | Christ's Object Lessons |
| 1903 | Education |
| 1905 | The Ministry of Healing |
| 1911 | The Acts of the Apostles |
| 1913 | Counsels to Parents, Teachers and Students |
| 1916 | Prophets and Kings |

10. Ellen White alilala kwa amani usingizi wa mauti katika kristo Yesu kama mtoto aliyechoka aendaye kupumzika, Nyumbani kwake Elmshaven mnamo Julai 16, 1915. alizikwa karibu na mumewe na watoto wake huko Battle Creek.

**h) Watangulizi wengine wa awali**

1. James White (1821 – 1881) alikuwa mhubiri wa ujumbe wa Marejeo. Pamoja na hali yake ya ulemavu, wa viungo aliona kwamba lilikuwa ni jukumu lake kuuonya ulimwengu juu ya mwisho ambao unakaribia sana, na hivyo aliendelea kuhubiri sehemu mbali mbali ujumbe wa malaika wa kwanza. Alikuwa ni mhubiri mwenye kusihi na mwimbaji mashuhuri lakini zaidi ya yote alikuwa kiongozi wa watu. James White alikuwa shupavu, mbunifu, mwenye kuona mbali, kiongozi mwenye shauku juu ya kanisa la Waadventista ambalo ni changa ambaye katika miaka ya mwanzo wa historia alifanya sehemu kubwa.

   Kwanza kwa kutayarisha mafundisho na kuwafunza watu wa kuyasimamia. Pili kuhamasisha na kuunda chombo cha utawala na tatu, kuanzisha na kuzimazima taasisi mbali mbali. Kanisa kama Taasisi, Uchapaji, Afya na Elimu ambavyo ndiyo nguzo ya makusudio yote.

   James White ni mtu aliyezaliwa na silka ya uongozi. Wote waliotenda kazi pamoja naye waliona uwezo wa Roho ukitenda kazi ndani yake…. "(Spaldings)

kwa miaka kadhaa alikuwa na afya mbaya, kwa sehemu ilisabishwa na kufanya kazi kupita kiasi na hivyo akafa akiwa na umri wa miaka sitini tu, lakini katika umri huo tayari alikuwa ametumiwa na Mungu vya kutosha katika uanzilishaji wa kanisala Waadventista Wasabato.

James White alitenda kazi kama Kiongozi Mkuu wa Kanisa ulimwenguni (General Conference President) kwa vipindi vitatu mfululizo vilivyopata miaka kumi kwa jumla.

2. Joseph Bates (1792-1872) aliibuka kutoka kuwa mhudumu wa meli hadi Nahodha na kustaafu kazi ya ubaharia kabla tu ya ujumbe wa malaika wa kwanza kumfikia. Mungu alikuwa akimwongoza.

Siku zote alikuwa mtu mwenye kuongozwa na kanuni bora na mpenda haki na kweli. Aliacha kabisa matumizi ya mvinyo na tumbaku wakati bado akiwa baharia. Alikuwa mshiriki wa kanisa la Kikristo, hadi alipopata mwito wa kazi ya uhubiri akiwa na umri wa miaka hamsini, alianzisha moja ya vyama vya kiasi vya kwanza kule Marekani. Fedha zake nyingi alizitumia katika kazi hii hadi kipindi kile cha kukatisha tamaa alikuwa amebakiwa na fedha kidogo sana hivyo baada ya hapo aliishi kwa imani tu.

Alikuwa kiongozi wa kwanza miongoni mwa viongozi waliokubali kuwa wahubiri wa Kanisa la Waadventista Wa Sabato, waliukubali ukweli kuhusu Sabato na kuwafundisha watendakazi wengine na waumini, pia aliandika kijarida fasaha kuhusu Sabato ambacho pia kilichapishwa.

Baadaye alitumia muda wake mwingi kusafiri hadi pande za magharibi ambako Injili ilikuwa bado kufika. Alisafiri hata wakati wa baridi kali na barafu huko Canada na pande zote za mashariki mwa Marekani.

Aliendelea kufanya kazi hiyo katika hali ngumu bila kukata tama. Alikuwa na umri mkubwa zaidi kuliko watendakazi wenzake vijana na hivyo walijifunza kutoka kwa mashauri ya utu uzima katika kuendeleza kazi ya Mungu. Alikuwa mchangamfu na mwenye nguvu hadi mwisho wa maisha yake. Alifariki mwaka 1872 na kuzikwa karibu na nyumbani kwake huko Michigan.

3. John Nevins Andrew (1829 – 1883) alikuwa na umri wa miaka kumi na mitano tu katika wakati ule wa kukata tamaa, alianza kazi ya kuhubiri akiwa na umri wa miaka ishirini na moja. Alikuwa miongoni mwa viongozi wa kwanza kukubali ukweli wa Sabato na pia alikuwa mwanafunzi mwenye bidii, Mwandishi bora (kitabu chake maarufu kilijulikana kama ("History of The Sabbath") na mtu wa mipango mizuri. Aliongoza katika kujifunza mpango wa Mungu wa matoleo kwa ajili ya Injili, ambao baadaye uliendelezwa na kuzaa mfumo wa urudishaji wa zaka tunaoufahamu hadi leo. Mwezi Agosti 1860 alipendekeza hadharani kwamba washiriki ni lazima wakutane na kujadili muundo wa Uongozi wa kanisa. Hatimaye matokeo yakawa kuundwa kwa Adventist Publishing Association na jina "Seventh-day Adventist" likachaguliwa kwa ajili ya Kanisa. Kutokana na

ujuzi wake wa lugha, alitumwa kwenda Ulaya mwaka 1874 kama Mmishonari wa kwanza kwa nchi za nje, na huko aliweka msingi imara wa kazi J.N. Andrews alikuwa ndiye Rais wa Tatu wa Jenero Konferensi (General Conference).

4. John Norton Laughborough (1832-1924) alihubiri habari za wanamarejeo tangu akiwa na umri wa miaka 16, japo hakuwahi kupata ukweli kuhusu Sabato hadi 1852. Ambapo J.N. Andrews alimweleza kwa ufasaha mara moja aliukubali. Aliendelea kutenda kazi pamoja na N.E. Cornell hadi miaka ya 1850 ambapo wahubiri walianza kulipwa mishahara, alifanya kazi nyingi yoyote ambayo angeweza kufanya kwa muda wa siku nne na nusu za juma na kwa muda uliobaki alihubiri.

5. John Byington (1798 – 1887) anajulikana vizuri kwa kuwa ndiye alikuwa Raisi wa kwanza wa Jenero Konferensi. Ambaye kabla ya kupata ujumbe wa malaika wa tatu alikuwa mhubiri wa Kithodisti, moja ya Shule za Sabato za kwanza na shule ya kwanza ya Kanisa la Waadventista (zilianza mwaka 1853) zilifundishwa nyumbani mwa Byington huko Bucks Brige, New York na mwalimu wake akiwa ni binti yake Martha.

   Watunzaji wa Sabato wa mwanzo walikusanyika mahali pake ambapo baadaye alijenga Kanisa la Waadventista.

6. J.H. Waggoner (1820 – 1889) alipokea ujumbe wa Marejeo mwaka 1852 na ameorodheshwa kuwa miongoni mwa watu waliohimiza mkutano wa kujadili muundo wa uongozi wa kanisa mnamo mwaka 1860, kwa wakati huo alikuwa ni miongoni mwa viongozi wa marejeo waliokuwa wakitunza Sabato. Alitenda kazi pande za magharibu, hususani kama mhariri wa "The Signs of the Times" Baadaye alifanya kazi Ulaya na kufariki kule Switzeland.

7. Unabii (1832-1903) na Annie (1828-1855), Smith walikuwa vijana wawili kaka na dada wa kutumainiwa ambao walikuwa ni waalimu wakati Mungu alipowaita kazini mwake. Annie Smith aliitika mwisho baada ya njozi yake kuhusu Mzee Joseph Bates ambaye alikuwa amemsikia akihubiri punde siku hizo. Alikuwa ni mtenda kazi mwenye shauku ambaye anakumbukwa sana kwa mashairi yake ambayo mengi baadaye yalitumika kama nyimbo za ibada. Maisha yake yalikatizwa mnamo mwaka 1855 kutokana na ugonjwa wa Kifua Kikuu. Uriah Smith naye alipokea ujumbe huu mwishoni mwa mwaka 1852 zaidi ya mwaka mmoja tangu dada yake aupokee. Hivyo yeye aliingia katika kazi ya uchapaji. Alikuwa ni mtumishi aliyewekwa wakfu kwa ajili ya kazi ya Injili na ambaye aliutumia muda wake wa maisha kama mhariri tangu mwaka 1853 hadi 1903 wakati alipokufa. Alikuwa mhariri wa Review and Herald na pia mwandishi wa kitabu "Thoughts on Daniel and The Revelation" ndio mchango wake mkubwa atakaokumbukwa kwao. Mnamo mwaka 1888 alikuwa ni Kiongozi wa mjadala juu ya haki kwa imani. Pia alikuwa miongoni mwa wanafunzi wa Biblia wa kutegemewa.

8. Frederick wheeler (1811 – 1910) alikuwa ni mhubiri na mwanamarejeo wa Kimethodisti ambaye aliishi huko New Hempsshire ambaye alihudumia kanisa la Washington kama mchungaji. Huyu ndiye aliyekuwa mhubiri wa kwanza wa

Waadventista miongoni mwa Waadventista wa siku ya Saba. Yeye alipokea ukweli wa Sabato ulioletwa kwake na Rachel Oakes (ambaye baadaye aliitwa Rachel Preston) mwaka 1844, ambaye katika kundi lake waliopokea ujumbe wa malaika wa tatu walikuwa akina Farnsworth, William na Ahasuero (Cyrus).

**Kwa kujifunza zaidi juu ya watangulizi wa awali, soma:**

Life Sketchez of Ellen G. White uk. 105-111 Foot print of the pioneers, by Athur W. Spalding (Unaweza kupata toka maktaba ya Kanisa lako au Shule).

## SEHEMU YA NNE

## KUUNDWA KWA KANISA LA MASALIO 1853 - 1863

**a) Kutolewa kwa vitambulisho:**
Hatua muhimu ya mwanzo katika uundaji wa Uongozi wa kanisa ilikuwa ni kutolewa vitambulisho kwa wahudumu. Mpango huu ulianzishwa mnamo mwaka 1853. Wahubiri hawa wa kujitegemea walihubiri kwa msisimko na shauku kuu.

**b) Hema la kwanza la Kiinjilisti pamoja na kuanzishwa kwa matawi ya shule ya Sabato**
M.E. Cornell na J.N. Loughborough walitumia hema katika kufanya mahubiri ya hadhara mwaka 1854 na watu wengi wakajiunga na kanisa. Shule ya sabato ya kawaida ya awali ilifanyika huko Rochester na Buck's Bridge, New York miaka ya 1853 na 1854.

**c) Kuhamia Battle Creek**
Walei wanne walimpatia James White dola 200 ili aweze kujenga jengo kwa ajili ya uchapaji huko Battle Creek. Baada ya maombi mengi, msaada huo ulikubaliwa na hivyo walihama toka Rochester, New York, kwenda Battle Creek Michigan mwaka 1855. Makao makuu yaliendelea kuwa pale hadi mwaka 1903. Kwa ajili ya kuwa kumbukumbu la jinsi utendaji na Uongozi wa Mungu katika uhamishaji wa makao hayo makuu kutoka Battle Creek kwenda Washington, angalia Life Sketches of Ellen White pp. 388 -398.

Mahali hapo papya palipojengwa mtambo wauchapaji, kiwanda kilikuwa na kazi kubwa ya kuchapa Review and Heralds na Youth Instructor, vijizuu kuhusu mambo ya kiasi pamoja na Uinjilisti. Uriah Smith aliteuliwa kuwa Mhariri na mwandishi walikuwa ni pamoja na J.N. Andrew James White na J.H. Waggoner.

Joseph Bates naye akahamia Michigan na huko aliendelea kufanya mikutano ya Injili akiongoza Konference na kuendelea kusafiri kwa muda mwingi kuhudumia kondoo waliotawanyika.

**d) Machapisho ya Awali**
Mnamo mwaka 1849 KUNDI LA WANAMAREJEO WENYE KUITUNZA Sabato lilianza kuchapisha gazeti lililoitwa Ukweli wa Leo The Present Truth". Mwaka 1850 walichapisha matoleo sita ya gazeti la Adventist Review. Mwaka huo huo mwezi Novemba, magazeti hayo mawili yalichanganywa na kutolewa kwa jila la "Second

Adventist and Sabbath Herald ambalo sasa linajulikana kama Adventist Review. Hili ni gazeti la kawaida ambalo huandika habari kuhusu shughuli za Kanisa katika ulimwengu mzima zinazohusu ibada pamoja na makala zingine za mafundisho. Lipo toleo la kila juma pamoja na lile linalotolewa kila mwezi ambayo yote mawili huchapishwa katika mitambo ya uchapishaji ya Review and Herald Publishing Association huko Washington D.C.

Gazeti la Youth Instructor lilianzishwa na James White mwaka 1852 kule Rochester, ambamo mlikuwa na masomo ya Shule ya Sabato ya kila juma. Ili kutimiliza kusudi lake la awali. Kanisa leo huchapisha gazeti kama insight ambalo huchukua nafasi ya Youth Instructor, Guide Primary Treaasur, Our Little Friends, pamoja na masomo ya Shule ya Sabato ya kila robo.

e) **Upinzani Dhidi ya kuwa na jumuiya**. Hii ilitokana na ukweli kwamba wengi wao walikuwa wameondolewa ushirika wao katika makanisa yao ya awali na hivyo kuwafanya wawe kinyume na mpango wowote wa kuanzishwa kwa jumuiya ya kikanisa. Hata hivyo katika muda mfupi ilikuwa dhahiri kwa wengi kwamba jumuiya ya kikanisa ilikuwa ndiyo kinga yao dhidi ya machafuko na misisimko yenye kupotosha.

**f) Mpango wa fedha katika Kanisa la Awali**

Katika miaka ya 1850, wale wote waliokuwa wanahubiri ujumbe wa marejeo walitegemea sana ukarimu wa wasikilizaji wake hivyo walifanya kazi kidogo sana ili kujikimu. Kundi chini ya uongozi wa J.N. Andrews waliyachunguza Maandiko ile njia ambayo Mungu aliiweka ili kusaidia kazi ya Huduma. Maelezo ya mwisho yalijulikana kama utoaji kwa mpango "Systematic Benevolence". Mpango uliokubaliwa ulimtaka kila mshiriki kutoa kila mwaka angalao asilimia moja ya mali yake ukiachilia mbali pamoja madeni na sadaka za kila juma.

Hadi kufikia mwaka 1853, vitabu vilitolewa bure lakini katika mwaka ule James White alipendekeza kwamba wahubiri waviuze vijizuu pamoja na magazeti. Seti nzima iliyokamilika iligharimu senti thelathini na tano tu (cts 35).

**g) Uamuzi wa kuunda jumuiya**

Baada ya kujadili juu ya mfumo wa fedha wa kufaa, wengine walipendekeza kuwa na jumuiya ya kisheria ambayo itamiliki mali yote ya kanisa. Wachache walipinga. James White pamoja na wenzake walilaumiwa kwa kutaka utawala na kuunganisha dola na Kanisa. Katika miaka ya 1850, Mungu alizungumza kupitia kwa mtumishi wake "Mbinguni upo utaratibu na Mungu anapendezwa sana na juhudi za watu wake, katika kazi hapa duniani. Nilionyeshwa kwamba ni lazima kuwe na utaratibu katika Kanisa la Mungu, na kwamba mfumo huo unahitajika katika kusukuma mbele kwa mafanikio ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu." (Testimonies Vol. 1, p. 191)

Mnamo mwaka 1860 mjadala ulifikia kilele na washiriki wakaamua kuanzisha jumuiya ambayo kisheria ndiyo itakayokuwa mmiliki wa ofisi za Uchapaji pamoja na nyumba za Ibada.

**h) Kuchaguliwa kwa jina**

Mwaka huo huo 1860 jina "Seventh-Day Adventist" lilianzishwa. Baadaye Ellen White akapitisha uamuzi huo. "Jina Seventh-Day Adventist hubeba mwonekano halisi wa Imani yetu mbele na utabaini kila moyo wenye utafiti. Kama mshale kutoka katika upinzani wa Bwana. Utamjeruhi kila mwenye kuiasi Sheria ya Mungu na utawaongoza watubuo kwake na imani katika Bwana wetu Yesu Kristo". (Ibid. p. 224).

Chama cha kisheria kilihusishwa Mei 13, mwaka 1861 na kikaitwa The Seventh Day Adventist Publishing Association. Katika mwaka huo huo, Makanisa katika jimbo la Michigan waliungana na kuunda Konferensi ya kwanza. Konferensi zingine saba zilianzishwa mwaka 1862.

**i) Mkutano Mkuu wa Kwanza: (General Conference Session)**

Kusanyiko la kwanza maalumu la Waadventista wa Sabato lilifanyika Battle Creek mwaka 1863. Katiba yenye kanuni tisa ilikubaliwa, kanuni ambazo ziliendelea kuongezwa katika sesheni zilizofuata, lakini hakuna mabadiliko makubwa ambayo yamefanywa.

Maofisa wa chombo hiki kipya kilichoundwa walichaguliwa. Kiongozi Mkuu (President) John Byington, Katibu Mkuu Uriah Smith, Mhazini E.S. Walker, James White alichaguliwa bila kupingwa lakini alipinga kwa msingi kwamba utetezi wake madhubuti wa jumuiya hii ungehafifishwa kwa madaraka hayo mapya.

Wajumbe wa Kamati Kuu walikuwa John Byington, J.N. Loughborough na James White.

**j) Washiriki na Wahudumu**

Hadi wakati huo, kulikuwa na washiriki 3,500 katika makanisa 125. Kulikuwa na wahudumu 22 waliowekwa wakfu na wengine 8 walikuwa na vyeti.

## SEHEMU YA TANO
## KUPANUKA NA MATENGENEZO
## 1864-1873

**a) Kushinda vikwazo:**

Vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Wamarekani (1861 – 1865) vilikuwa kikwazo kwa ukuaji wa Kanisa la Waadventista wa Sabato. Hata hivyo, mwishoni mwa vita hivyo, maendeleo yalifanywa kwa upya. Mwaka 1865 James White alichaguliwa kuwa Kiongozi Mkuu wa Kanisa Ulimwenguni (President of the General Conference)

Katika kipindi hicho cha vita mwaka 1864, Kanisa lilipewa hadhi na Serikali ya Marekani ya kutohusika katika mapigano.

**b) Wito kwenda magharibi:**

Katika Mkutano Mkuu wa Kanisa wa mwaka 1868, J.N. Loughborough na D.T. Bourdoau walichaguliwa kwenda kutenda kazi katika Pwani ya magharibi. Huko kulikuwako Waadventista 14 (kumi na nne) ambao walisihi wapelekewe watendakazi. Hema lililonunuliwa ikiwa na matokeo ya ombi lililotolewa na James White katika gazeti la Review and Herald. Hivyo kazi ilikuwa kwa upesi na kuenea mpaka magharibu mwa Canada.

Mnamo mwaka 1872 familia ya White ilitembelea pwani ya Pacific na hivyo waliuza nyumba yao ya Battle Creek na kuzitoa fedha zile kama msaada kwa maendeleo ya kazi katika Pwani ya magharibi. Gazeti la kwanza la dalili za Nyakati "Signs of the Times" lilitarajiwa kuchapishwa June 4, 1874 kule Califonia.

Leo Magharibi ya Marekani kuna idadi kubwa ya washiriki Waadventista wa Sabato ambao hufanya kadiri ya theluthi moja ya washiriki wote wa Divisheni ya Marekani ya Kaskazini (North American Division).

**c) Kukua kwa kazi ya uchapaji:**

Mnamo mwaka 1865 vijizuu sita vya Ellen White juu ya Afya ya juu ya maisha vilitolewa. Maandiko hayo yalikuwa na msingi katika maeneo ya mwezi June, 1863 juu ya matengenezo ya afya na bila kusita washiriki wakayakubali mashauri hayo. Kulikuwa na kukata tama juu ya hitaji la maagizo hayo, kwani wengi wa viongozi watangulizi wa mwanzo walikuwa na afya mbaya kwa sababu ya ujinga. Waumini walipenda kazi hii ya kiasi lakini hawakujua mambo muhimu kuhusiana na kuishi kiafya.

Mwaka 1866 gazeti la mtengenezaji wa afya "Health Reformer" ambalo lilikuwa gazeti la kwanza kuhusu afya kuanzishwa na kanisa.

**d) Kuanzishwa kwa Taasisi za Afya:**

Kama matokeo ya njozi yake ya pili kuhusu afya, taasisi ya afya ilianzishwa mwaka 1866, ilijulikana kwa jina la "Taasisi ya matengenezo ya Afya ya magharibi" "Western Health Reform Institute", na baadaye kama Battle Creek Sanitarium: ilikuwa ikilipiwa ada ya uanachama. James White pamoja na J.P. Kellogg walitoa kila mmoja dola mia tano $ 500). Ulikuwa ndio mwanzo wa mwendelezo wa mnyororo wa taasisi ulimwenguni pote. Dr. Kate Lindsay alisaidia uanzishaji wa shule ya Wauguzi kule Battle Creek mwaka 1883.

**e) Kuanzishwa kwa shule:**

Juhudi za mtawanyiko zilifanywa katika uanzishaji wa shule za kanisa mwanzoni mwa 1853 chini ya Martha Byington kule Buck's Bridge, New York. (aliyedhaminiwa na baba yake John Byngton)

Shule ya kwanza rasmi ya Kanisa la Waadventista wa Sabato popote ulimwenguni ilianzishwa mwaka 1872 kule Battle Creek na Goodloe H. Bell, ambayo awali alikuwa mgonjwa aliyehudumiwa katika taasisi ya afya ya Battle Creek (Battle Creek Sanitarium) Jengo lenyewe lilikuwa la ghorofa mbili lenye eneo la futi ishirini kwa thelathini (20"x30") ambalo awali lilikuwa kwa ajili ya shughuli za uchapaji. Leo Kanisa linaendesha shule kuliko dhehebu jingine lolote la Kiprotestant.

f) **Kuanzishwa kwa mikutano ya makambi:**
Wana marejeo wa awali walioishi kabla ya 1844 waliendesha mikutano ya makambi, wengine waliendesha mikutano hiyo katika mahema makubwa mno, ambayo mpaka wakati huo yalikuwa hayajapata kusimamishwa katika nchi ya marekani, hata hivyo walidharauliwa kwa tendo lao la kufanya ibada katika hema.

Wazo la mikutano ya makambi liliamshwa miaka mitano baada ya kuundwa kwa Jenero Konferensi na ilipofika mwaka 1868, mkutano wa kwanza wa makambi kwa Waadventista wa Sabato ulifanyika kule Michigan ukiwa na washiriki wapatao 2,000. Mwaka 1876 kukawa na washiriki 20,000 katika mkutano wa makambi ya karibu na Boston.

Siku hizi, mikutano ya makambi hufanyika katika pande mbali mbali za ulimwengu na miongoni mwa mikutano mikubwa ni ile inayofanyika katika nchi ndogo ya Afrika ya Rwanda.

g) **Kuanzishwa kwa Shule ya Sabato:**
Lesoni ya kwanza ya Shule ya Sabato ilitayarishwa na kutolewa katika gazeti la "Youth's Instructor's mwaka 1852 ambayo ilitayarishwa na James White G.H. Bell, mtu mwenye karama ya ualimu ya kuzaliwa nayo ambaye alipata uzoefu katika Shule ya Jumapili, mwaka 1869 alitayarisha mfululizo wa masomo mawili kwa ajili ya Shule ya Sabato. Mwaka uliofuata jumuiya ndogo iliongezwa na hivyo ilitayarisha njia kwa Shule ya Sabato.

Zawadi ya kwanza ya Shule ya Sabato kwa misheni mwaka 1885 ingalipelekwa Australia na 1887 Afrika. Baadaye Shule ya sabato ya Marekani ya kaskazini ikatuma meli kwenda Pacific ya Kusini; "Pitcarn" iliwachukua wamishonari katika visiwa mbali mbali vya bahari hiyo, kisiwa cha Pitcairn leo wakati wake karibu wote ni Waadventista wa Sabato.

Mwishoni mwa mwaka 1978 kulikuwa na washiriki wa Shule ya sabato wapatao 3,817,459 ulimwenguni pote.

h) **Kuundwa kwa chama cha Umishonari wa vijizuu:**
Chama cha Wamishonari wenye kuwajibika, kilichoundwa mwaka 1869, ambacho kilifanya mradi wake mkuu kuwa usambazaji wa Maandiko, Stephen N. Haskell aliona uwezekano wa mafanikio katika kazi hii hivyo akaunda mkakati wa kuipanua zaidi; Familia ya White nayo ilizihimiza Konfrensi zingine kuanzisha vyama vya namna hii ambavyo baadaye vilijulikana kama vyama vya umishonari navijizuu. Hivi leo tuna Idara ya Uchapaji pamoja na maduka ya vitabu.

Mnano mwaka 1873, katika Jenero Konferensi, chama cha wamishonari kiliundwa. Matokeo yake yalikuwa ni kuongezeka kwa kazi ya Umishonari miongoni mwa washiriki. Chama hiki kiliendelea hadi ilipoanzishwa Idara ya Umishonari wa nyumbani 1913, ambayo kwa sasa inajulikana kama Idara ya shughuli za Walei.

## SEHEMU YA SITA

## NJOZI KWA AJILI YA ULIMWENGU MZIMA 1874 – 1878

a) **Mmishonari wa kwanza nchi za Ng'ambo:**
Kwa miaka kadhaa mwito wa Kimakedonia umekuwa ukiletwa Jenero Konferensi toka "Switzerland". Watu wamekuwa wakiandika kuomba mafundisho kuhusu Sabato, wakati huo huo Mungu amekuwa akiwaandaa watu wake kwa ajili ya kazi yake ulimwenguni kwa kuleta ujumbe kupitia kwa mtumishi wake Ellen White.

Katika mkutano mkuu wa Jenero Konferensi (General Conference) mwaka 1874, hatua za kuridhisha za maendeleo zilichukuliwa. John Nevins Andrews aliteuliwa kuwa mmishonari wa kwanza katika nchi za Ng'ambo na akapelekwa Switzerland.

Mwanae wa kiume Charles akiwa na umri wa miaka 17 na binti yake Maria akiwa na umri wa miaka 13 walitweka baharini pamoja naye, kwani mkewe alikuwa ameshafariki mwaka 1872.

Mwanzoni kabisa M.B. Czechowski Mchungaji wa Kikatoliki aliyekuwa ameongoka, alirejea tena Ulaya na kuwashawishi watu kadhaa juu ya ukweli wa Sabato japokuwa hakuwa ametumwa na kanisa.

Mara tu baada ya Andrews kuwasili, misheni ya Ulaya ilianzishwa. Alikwenda Prussia na kuwasiliana na watunzaji wa Sabato zaidi ya 46 (arobaini na sita).

**b) Kazi ya uchapaji katika Swizland:**
Kiwanda cha uchapaji kilianzishwa kule Basel mwaka 1876 na makala ya kwanza ya Waadventista wa Sabato wa Ulaya iliyohusu dalili za nyakati kwa lugha ya Kifaransa ilitolewa.

c) Kuenea kwa kazi huko Ulaya:
Ujumbe uliingia katika nchi za Scandnavia mwaka 1877 kupitia kwa John G. Matteson na hivyo kiwanda cha uchapaji kilianzishwa miaka miwili baadaye. D.T. Bourdeau alipewa jukumu la kusimamia kazi kule Ufaransa, Ndugu yake A.C. Bourdeau alifanya kazi Italia, Ujerumani, Ufaransa, Switzerland na Romania. Philipp Reiswig aliupeleka ukweli huu hadi Urusi, alikuwa ni mtu asiye na elimu na mwenye kigugumizi lakini Mungu alimfanya kuwa mtenda kazi wake aliye bora.

**d) Kuanzishwa kwa kazi katika uingereza**
Uingereza ilikuwa ni moja ya sehemu za mwanzo kabisa kuanzishwa kwa kazi katika Ulaya. Mwaka 1878 William Ings alikwenda huko na katika kipindi cha muda wa majuma 16 (kumi na sita) watu 10 (kumi) walikuwa tayari wanatunza Sabato. Loughborough naye alikuja baadaye katika mwaka huo huo na kuendelea kusimamia kazi ya Mungu. Baada ya muda mfupi mtambo wa uchapaji wa Stanborough na chuo cha New Bold kilianzishwa na hivyo Uingereza ikawa ndiyo hazina ya kupeleka wamishonari katika nchi zingine.

## SEHEMU YA SABA

## MAENDELEO MUHIMU PAMOJA NA MAPUNGUFU 1879-1904

## MAENDELEO MUHIMU

**a) Kuanzishwa kwa Chama cha Vijana:**

Chama cha Vijana cha kwanza kilianzishwa huko Hezelton, Michigan, mwaka 1879 na vijana wawili, Harry Fenner aliyekuwa na umri wa miaka 17 na Luther Warren aliyekuwa na umri wa miaka 14.

Mwaka 1889 Konferensi ya Ohio ilikuwa ndiyo ya kwanza kukifanya Chama cha Vijana kuwa jumuiya ya kuwaunganisha vijana wake wote katika Konferensi. Chama hicho kilijulikana kama wamishonari wa kujitolea (Missionary Volunteer-MV). Mwaka 1901 Chama cha Vijana kiliwekwa chini ya uangalizi wa Idara ya Shule ya Sabato. Mwaka 1907 Idara ya Vijana katika Jenero Konferensi ilianzishwa rasmi kama Jumuiya.

**b) Kuanzishwa kwa kazi ya Uinjilisti wa vitabu:**

Kupitia kwa mtumishi wake Ellen White mwaka 1879, Mungu alielekeza juu ya hitaji la kusambaza vitabu miongoni mwa watu. Miaka miwili baadaye, George King aliona umuhimu wa kukiuza kitabu cha Danieli na Ufunuo "Daniel and Revelation". Mpango huu ulikuwa wa mafanikio makubwa na kwa njia hiyo kazi ya Uinjilisti wa vitabu ilianzishwa.

Mwaka 1978 kulikuwa na Wainjilisti wapatao 6,459 ambao walifanya mauzo ya vitabu na maandiko mbali mbali ya Kanisa kufikia kadiri ya $ 111,000,000 (Dola Million mia moja na kumi na moja)

c) Urudishaji wa Zaka:

Mfumo wa urudishaji zaka ulichukua nafasi ya mpango wa utoaji kwa mpango wa mwaka 1878. Kama matokeo ya Mapato kutoka katika zaka na mauzo ya vitabu, awamu zote za Kazi ya Mungu ziliimarika zaidi. Mpango wa Zaka na Utoaji kwa Mpango umeliwezesha Kanisa kugharimia mpango wa Injili katika Ulimwengu mzima.

**d) Kuongezeka kwa washiriki wapya:**

Mnamo mwaka 1883, yaani miaka 20 (ishirini) tangu kuundwa kwa Jenero Konferensi, kulikuwa tayari kuna makanisa 680 na Washiriki 17,436, zaka iliyotolewa na washiriki hawa ilifikia dola 96,500 (dola tisini na sita elfu na mia tano)

**e) Kuanzishwa kwa Mpango wa Usomaji wa Biblia:**

Dhoruba katika mkutano wa makambi ilimlazimisha Stephen Huskell kuacha kuendelea na mahubiri na badala yake alikusanya kundi la waumini kumzunguka, kisha aliwapa mafungu na kuanza kuwauliza maswali. Ellen White alikuwepo na aliunga mkono mpango huo, ambao sasa ndio mpango muhimu wa Uinjilisti.

**f) Kuanzishwa kwa kazi Ulaya:**

Rais wa Jenero Konferensi aliyeitwa George I. Butler alitembelea Ulaya mwaka 1844 na kuanzisha Konferensi. Mwaka uliofuata Ellen White naye alikwenda Ulaya na kutoa mashauri zaidi kwa viongozi.

g) Kuenea ujumbe hadi Pacific ya Kusini:
Kwa mara ya kwanza ujumbe uliingia Australia mwaka 1885 kwa njia ya chama kilichoongozwa na S.N. Haskell, M.C. Israel na J.O. Corliss, walipata upinzani mkali lakini kanisa na mitambo ya uchapaji vilianzishwa katika Melbourne, New Zealand ilifuatia katika kupokea ujumbe wa marejeo wakati Haskell alipokwenda huko mwaka 1885 na A.G. Daniells aliyesafiri kwenda huko mwaka 1886.

Hali iligeuka na kuwa kama ilivyokuwa katika kisiwa cha Pitcairn mara tu baada ya John I. Tay kuwasili mnamo mwaka 1886.

Mmishonari wa mwanzo kwenda katika visiwa vya Fiji alikuwa J.E. Fulton na hata sasa kuna chuo ambacho kinaitwa kwa jina lake. Hivi leo Waadventista wa Sabato katika Fiji wanajulikana kama "Watu Safi".

**h) Wakati wa kufanya mapitio:**

Mnamo mwaka 1860 na 1870 Wainjilisti wa Kiadventista walikuwa wakifanya juhudi kubwa kuonyesha kwamba Sheria ya Mungu haikuishia pale msalabani na hivyo walitilia mkazo kidogo tu kwa "imani ya Yesu" na kusisitiza sana juu ya "Amri za Mungu". Bado walikuwepo watu waliokuwa wakishikilia mawazo ya Waaria kumhusu Kristo na ambao hawakuamini juu ya Utatu Mtakatifu au juu ya Roho Mtakatifu kama Nafsi.

Mkutano Mkuu wa Jenero Konferensi wa mwaka 1888 ulifanyika kule Minneapolis, ulikuwa ni mkutano muhimu mno katika historia ya Kanisa. Kwa sababu wengi walikuwa wamepoteza maana ya "Haki kwa imani" na hivyo kilele kilikuwa kimefikiwa. Miaka 10 yaani kati ya 1888 na 1898 ilikuwa ni miaka iliyoambatana na uamsho ambapo somo la Haki kwa Imani lilijadiliwa kwa nguvu sana na wengi walilikubali. Ujumbe mwingine uliletwa kwa kanisa kupitia kwa maandiko ya ellen White, mfano vitabu vya "The Desire of Ages" na "Steps to Christ" ambavyo vilisahihisha makosa katika mafundisho juu ya asili ya Kristo na kuthibitisha ujumbe wa ukweli juu ya haki kwa imani.

**i) Wito wa Makodonia " kutoka Afrika ya Kusini, 1886**
Bara la Afrika ndio lilifuatia kusikia ujumbe wa Malaika watatu na historia juu ya mwanzo wa kazi katika bara hili kubwa ni wa kusisimua sana. Kitabu cha kuvutia chenye habari juu ya mwanzo wa kazi kusini mwa Afrika ni kile kiitwacho Track and Jungle Trail kilichoandikwa na Virgil Robinson.

**j) Misheni za kwanza barani Afrika:**
Mnamo mwaka 1894, Peter Wessels na wenzake walikuwa na mazungumzo na Cecil Rhodes ambaye alikuwa Waziri Mkuu wa Koloni la Cape na Mwenyekiti wa kampuni ya Kiingereze ya Afrika ya Kusini, katika mazungumzo hayo,

waliomba sehemu ya ardhi ambapo wangeweza kuanzisha Misheni kwa ajili ya Waafrika katika Rhodesia. Hivyo Rhodes alimwagiza Dr. L.S. Jameston ambaye alikuwa mtawala katika Bulawayo kutoa kibali kwa wawakilishi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato kuchagua sehemu yoyote ya ardhi ambayo wangeihitaji.

**k) Kuzinduliwa kwa kazi katika Uchina:**

Mnamo mwaka 1888 mshiriki mmoja mlei aliyejulikana kwa Jina la Abraham La Rue alikwenda Hongkong kama Mwinjilisti wa Kujitegemea, aliizuru china na hivyo kutayarisha njia kwa Wamishonari wa kudumu ambao ni Edwin H. Wilbur na J.N. Anderson ambao waliingia China nakuanza kazi miaka 14 (kumi na nne) baadaye.

l) **Kuundwa kwa Taasisi mbalimbali**

Chuo cha kwanza cha Waadventista wa Sabato nje ya Marekani kilianzishwa mwaka 1893. Kilianzishwa karibu na mji wa Cape Town ambacho baadaye kilijulikana kama Helderberg.

**Taasisi nyingine zilizoanzishwa katika nchi za kigeni ni:-**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Signs Publishing Company | - | Australia | - | 1886 |
| Stanborough Press | - | England | - | 1889 |
| Hamburg Publishing House | - | Germany | - | 1889 |
| Avondale College | - | Australia | - | 1894 |

<u>**(Madarasa ya Msimamizi hayapaswi kujifunza matukio ya mwaka 1893)**</u>

**m) Ziara ya Ellen White huko Australia:**

Ellen White alitweka kuelekea Australia mwaka 1891 ambako alikaa kwa muda wa miaka 9 (tisa) ukijumlisha miezi kadhaa aliyokaa New Zealand) na ziara hiyo ilionyesha dhahiri kwamba ulikuwa ni mbaraka wa pekee. Alizindua (Avondale College) ambayo kama ilivyotarajiwa ilitayarisha Wamishonari wengi ambao hatimaye walitumwa pande mbali mbali za ulimwengu.

Ellen White pia alihamasisha uanzishaji wa viwanda vya chakula bora. Kitengo hiki cha usindikaji wa chakula bora (Sanitarium Health Food Company) kimekuwa na mafanikio makubwa na kimekuwa ndio msambazaji mkuu wa chakula bora katika Australia na New Zealand. Zaidi ya hayo, kutokana na mapato ya fedha kutoka kitengo hicho cha chakula bora, Divisheni ya Australia imekuwa na uwezo wa kujiendesha kwa kujitegemea.

n) **Union ya kwanza kuwa Konferensi**:

Union ya kwanza kuwa Konferensi ulimwenguni iliundwa huko Australia mwaka 1894, Ellen White mwenyewe alihimiza mipango ya ukuaji wa haraka wa Kanisa, katika mwaka 1978 kulikuwa tayari na Union Konferensi 83 na Konferensi/Misheni/Field zipatazo 378 ulimwenguni pote.

**o) Kuboresha na kuimarisha:**

Jenero Konferensi katika mwaka 1901 ilikuwa ni jumuiya bora zaidi kwa kufanya mabadiliko ya kimuundo na kusukuma mbele kazi ya Injili. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:

1) Kamati ya Jenero Konferensi iliongezwa ukubwakwa kuongeza wawakilishi.
2) Union, Konferensi, Misheni pamoja na Konferensi/Misheni zikawa ni sehemu ya Jenero Konferensi.
3) Konferensi zikaanza kushirikiana katika mambo ya zaka na sadaka na Misheni/Field.
4) Jumuiya mbali mbali zinazojitegemea ambazo huwakilisha maslahi ya kanisa zikafanywa kuwa Idara za Jenero Konferensi.

Jenero Konferensi katika mwaka 1901 imeelezwa kama ndio upeo kuelekea umoja, matengenezo. Uwezo wa kifedha na shauku kubwa ya uinjilisti.

**p) Mapungufu yaliyojitokeza:**

Kulala kwa watangulizi

1) James White alifariki mwaka 1881. Kifo chake kilikuwa mwanzo wa mwisho wa zama za watangulizi katika Marekani.
2) John N. Andrews alilala mwaka 1883; hadi wakati huo yeye pamoja na wenzake walikuwa wamekwisha weka msingi wa kudumu wa kazi kule Ulaya. J.H. Waggoner alilala mwaka 1889. Wote wawili walizikwa Basel, Switzerland.

3) Uriah Smith Mhariri wa muda mrefu wa Review and Herald alilala mwaka 1903. Kitabu chake cha Thoughts on Daniel and Revelation bado kinathaminiwa sana hadi leo katika kipindi cha kufa kwake zama za umaarufu wa battle Creek zilikoma.

**q) Kuzimika kwa nyota zenye kung'aa:**

1) D.M. Canright aliliacha kanisa. Alikuwa ni mhubiri aliyekuwa mstari wa mbele katika kazi lakini baadaye aligeuka na kuwa mpinzani na kanisa na kazi ya Ellen White hatimaye alikufa akiwa hana tumaini.

2) Dr. J.H. Kellog aliyekuwa mkuu wa kitengo cha Afya cha Battle Creek naye pia akajitenga na kanisa, yeye naye pia alishindwa kuyakubali maonyo ya mjumbe wa Bwana, alionywa juu ya kuchanganya mawazo ya upagani wa kuamini kwamba Mungu ni kitu chochote na dini ya Kristo, pamoja na kundi la wenzake waliamua kupokonywa kitengo kile cha afya cha Battle Creek kutoka kwa uongozi wa kanisa.

3) **Moto kuteketeza Taasisi:** Mungu kwa kupitia kwa mtumishi wake, aliwashauri Waadventista waliokuwa wakiishi kule Battle Creek kwa mamia kuondoka na kwamba taasisizile zingeharibiwa kama wasingekubali kutawanyika. Mwaka 1902 mwezi wa Februari, jengo kuu la Taasisi ile ya Afya likaungua moto. Disemba 1902 kiwanda ambapo gazeti maarufu la Review and Herald lilikuwa likichapishwa nacho kikaungua. Katika mwaka 1903 ushauri wa Ellen White wa kuhamisha Makao Makuu kwenda upande

wa Mashariki ulizingatiwa, hivyo kukanunuliwa sehemu kule Takoma Park, Washington, D.C.

## SEHEMU YA NANE

## KUKUA NA KUPANUKA KWA INJILI 1905 – 1923

**a) Katika Ulimwengu wote:**
Hadi kufikia mwaka 1905, mipango ya Injili katika nchi za kigeni ilikuwa imepamba moto. Katika mabara yote, Roho wa Mungu alikuwa akiwaongoza waume kwa wake katika nuru.

*R.A. Caldwell (1905) na J.L. McElhany (1906) waliingia Ufilipino
*W.E. Howell alikwenda Ugiriki (1907)
*C.H. Parker akaenda New Habrides (1912)
*G.F. Jones alielekea katika visiwa vya Solomons (1914)
*F.A. Stahl akafungua kazi kwa ajili ya inca Indians katika Marekani ya Kusini 1909

b) Kuanzishwa kwa mpango wa sadaka ya mavuno:
Mwaka 1903 mshiriki mmoja Mlei aliyeitwa Jasper Wayne aliligawa gazeti la "Signs of the Times" na kukusanya fedha kwa ajili ya kazi ya Mungu. Ellen White alionyesha ukubali wake juu ya mpango huo na kuendelea kuunga mkono tangu ulipopendekezwa kwa mara ya kwanza. Hivi sasa wazo hilo limeendelezwa na kufanya mpango wa mavuno ambao hufanyika ulimwenguni kote kila mwaka. Pamoja na mpango huu wa mavuno, kukusanya fedha kwa ajili ya Injili pia hutoa nafasi kwa washiriki wa kanisa kuutangazia ulimwengu juu ya ujumbe wa malaika watatu.

c) Kuanzishwa kwa shule ya uinjilisti kwa njia ya Uuguzi:
Shule ya Uuguzi kwa mara ya kwanza ilianzishwa kule Battle Creek ambayo baadaye kiliporwa na Dr. Kellogg kutoka mikononi mwa Kanisa na baadaye kufungwa. Mnamo mwaka 1910 Chuo cha Uinjilisti kwa njia ya Uuguzi kilianzishwa rasmi huko Loma Linda, Calfonia.

Taasisi hii ilifanikiwa sana na mwaka 1913 ilianzishwa Kliniki huko Los Angeles (ambaye baadaye ilijulikana kama hospitali ya kumbukumbu ya White). Chuo hiki cha Uinjilisti kwa njia ya Uuguzi kimebadilishwa jina na kuitwa Loma Linda University. Hiki ni chuo chenye kiwango cha hali ya juu cha mafundisho ya taaluma ya Uganga, wahitimu wengi wa chuo hiki cha Loma Linda wametapakaa katika nchi nyingi ulimwenguni kutoa huduma na kwa kiasi kikubwa wamesaidia kutangaza ujumbe wa Injili.

**e) Kugawanywa kwa Kanda za Ulimwengu:**
Mwaka 1913, Field mbali mbali zilipangwa katika makundi na kujulikana kama Divisheni, ambapo kila mkuu wa Divisheni ni Makamu wa Mkuu wa Jenero Konferensi (Raisi wa Jenero Konferensi). Maofisa wa Divisheni na Wakurugenzi wa

idara pamoja na wale wote ambao wako katika Ofisi ya Makao Makuu huchaguliwa na Jenero Konferensi katika mkutano Mkuu wa Uchaguzi.

Kwa sababu ya kupanuka kwa kazi na kuongezeka kwa gharama za kusafirisha wajumbe, muda kati ya mkutano mmoja na mwingine wa Jenero Konferensi, ulirefushwa katika mwaka 1905 kutoka miaka 2 hadi 4, hatimaye katika mwaka 1970 ulirefushwa zaidi hadi kufikia miaka 5. (Kila baada ya miaka mitano)

*Kiongozi Mkuu anapaswa kufahamu majina ya wafuatao:
Viongozi wa Jenero Konferensi, divisheni na Union. Msimamizi anapaswa kufahamu Mkuu (Rais) wa Jenero Konferensi na katibu wake pamoja na mkuu (Rais wa Divisheni yake na Wakurugenzi 5 wa Divisheni).

(Kwa msaada wa mwalimu wako au kutoka katika kitabu cha matukio cha kanisa cha wakati huo "SDA Year Book" Mwanafunzi ajaze nafasi zilizoachwa wazi kwa maofisa wa sehemu yake)

| **Maofisa:** | **General Conference** | **Division** | **Union** |
|---|---|---|---|
| Rais | …………………… | ………………… | ……………… |
| Katibu | …………………… | ………………… | ……………… |
| Mhazini | …………………... | ………………… | ……………… |
| | | | |
| Wakurugenzi wa Idara | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Mawasiliano | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Elimu | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Afya | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Huduma za Walei | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Huduma | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Uhusiano na Uhuru | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Wa kuabudu | …………………….. | …………………. | ……………… |
| Uchapaji | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Shule ya Sabato | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Uwakili | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Kiasi | ……………………. | …………………. | ……………… |
| Vijana | ……………………. | …………………. | ……………… |

Kitabu kinachoelezwa habari za Kanisa SDA Year Book huchapishwa kila mwaka na hutoa orodha ya maofisa na viongozi wote wa idara mbali mbali, lakini uweze kufaulu mtihani unapaswa kuwaelewa walioorodheshwa hapo juu tu.

*Kiongozi mkuu na msimamizo wote wanapaswa kuwafahamu viongozi wao katika ngazi ya Union. Konferensi/Misheni/Field, Wakuu (Marais) na Wakurugenzi wa Vijana.

Kufariki kwa mjumbe wa Masalio:
Mwaka 1915 una umuhimu wa pekee katika historia ya Kanisa la Waadventista kwa kuwa ndio mwaka ambao Mjumbe maalumu wa Masalio alipofariki.

Katika miaka yake 70 ya kutenda kazi, Ellen White aliandika zaidi ya kurasa 100,000 (laki moja) zilikuwamo makala zaidi ya 4,000 katika magazeti na angalao nyaraka na barua 8,000. Jumla ya vitabu alivyoviandika hadi hii leo vinakadiriwa kufikia 65. Orodha ambayo miongoni mwa vitabu maarifu alivyoviandika imetolewa katika sehemu ya 3 (9).

Japokuwa kifo chake kiliashiria mwisho wa zama zake, lakini mvuto wa roho ya Unabii kama ilivyotabiriwa umeendelea, kuliongoza Kanisa. Mwaka 1907 Ellen White "Haidhuru kama maisha yangu yatakoma au kuachwa kuendelea, maandiko yangu daima yataendelea kusema na kazi yake itaendelea na kutimia kadiri muda utakavyomalizika.

Maandiko yangu yametunzwa katika majalada ofisini na hata kama sitaendelea kuishi, maneno haya ambayo Bwana wangu amenipa yatakuwa bado hai na kuendelea kusema na watu. Selected Messages Vol. 1. p. 55)

Mkutano wake wa mwisho wa Jenero Konferensi aliohudhuria mwaka 1909 aliinyanyua juu Biblia kwa mkono wake na kusema:
"Ndugu zangu, ninakithibitisha kitabu hiki kwenu" kwa Mwadventista huyu wa pekee aliyewekwa wakfu pia kama shahidi, kitabu hiki cha Biblia kilikuwa ndiyo "Kanuni ya pekee ya imani na mwenendo"

"Biblia imepewa umuhimu kidogo tu" alisema, na Mungu ametoa nuru ndogo kuwaongoza waume kwa wake kwenye ruru kuu" (Review and Herald Jan. 20, 1903)
Ellen White alilala Julai 16, 1915 akiwa na umri wa miaka 87. maneno ya mwisho aliyomwambia mwanae yalikuwa "Ninamjua ambaye nimemwamini".

f) Kanisa katika ulimwengu wote:

Kutoka katika hali ya kazi kufanyika katika nchi moja kwa takribani nusu karne hivi ya kuenea kwa ujumbe wa marejeo, mwanzoni mwa karne ya 20 kazi iliendelea kwa upesi hatimaye kanisa likaenea katika ulimwengu wote. Ni katika kipindi hiki ndipo ambapo kanisa lililindwa katika vita kuu ya kwanza ya dunia (1914-1918). Wakati ambapo A.G. Daniells alipoacha majukumu ya kuwa mkuu wa kanisa ulimwenguni (Rais) mwaka 1922, ilikuwepo haja ya kupata kiongozi mwenye mtazamo wa kimataifa ambaye angekuwa na upeo wa kuelewa kazi hii katika ulimwengu wote. Mtu huyo hakuwa mwingine bali W.A. Spicer ambaye aliwahi kuwa Katibu mkuu wa Jenero Konferensi kwa miaka 20 ambaye pia alikuwa ametembelea nchi mbali mbali.

*Msimamizi anapaswa kuwafahamu angalau watangulizi watatu waliofanya kazi katika Union yake.

## SEHEMU YA TISA

## MAFUNDISHO DHIDI YA VIKWAZO (1924 – 1946)

a) Kufa kwa mwanzilishi wa mwisho

Kifo cha J.N. Laughborough, mnamo mwaka 1924 kilifanya zama za watangulizi kukoma. Hata hivyo moyo wa uanzishaji haukukoma. Katika mkutano mkuu wa Jenero Konferensi wa mwaka 1926, watendakazi 150 walipelekwa katika nchi mbali

mbali za kigeni. Mara tu baada ya Hospitali/Shule kuanzishwa huko Ethiopia, Japan, Poland, Angola na katika Visiwa vya Ufilipino.

Misheni Mpya zilianzishwa katika bahari za Kusini, mashariki ya kati, Cameroon, Brazil na huko West Indies.

Shule/Viwanda vya Uchapaji vilianzishwa katika Uchina, Himalaya, Java, Trinidad na India

Kwa muda wa miaka 10 kazi ilishamiri sana. Mbegu zilizokuwa zimekwisha pandwa na waanzilishi zilizaa matunda kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu.

b) Miaka ya Ukata:
Hali mbaya ya ukata iliyoukumba ulimwengu katika mwaka 1929 na miaka iliyofuata kwa kiasi fulani ilipunguza kazi ya maendeleo ya Kanisa.

Mwaka 1930 (C.H. Watson, Rais wa Divisheni ya Australia aliitwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi. Alifahamika kwa uwezo wake mkubwa na upeo wa kuona na kupanga mipango ya kifedha. Kama matokeo ya ukata uliokumba ulimwengu miaka ya 1931 hadi 1934, mapato ya kanisa yalipungua kwa Dola 54,000,000 (milioni hamsini na nne). Hata hivyo, inashangaza kuona kwamba idadi ya washiriki iliongezeka kwa jumla ya watu 90,000. Misheni 48 zilianzishwa na watendakazi 654 zaidi waliajiriwa. Kwa hakika Bwana alizawadisha imani na kazi ya watu wake.

c) Uinjilisti wa kiganga wa mwanzo:
Mwaka 1931 wauguzi wawili Leo B. Halliwell na Mkewe Jessie walipeleka vikosi vya kwanza vya Umishonari kwa njia ya Uganga ambavyo vilifanya kazi kwa nguvu kule Amazon na katika mito mingine ya Marekani ya Kusini. Kituo cha kwanza kilinunuliwa kwa vile hakukuwa na fedha za kutosha kuanzisha hospitali. Njia hii kama zingine ilikuwa na Mungu kuanzisha mafanikio mapya ya Uinjilisti.

d) Chama cha Kiasi:
Chama cha kiasi cha Marekani kilianzishwa na Jenero Konferensi mwaka 1932, wakati ambapo bajeti iliyobanwa sana na kuzuia uwekezaji wa kiasi kikubwa cha fedha; kuhamasishwa kwa kazi ya kiasi kuliendelea kufanikiwa pamoja na ugumu uliojitokeza, hivyo chama cha kiasi cha kimataifa “International Temperance Association mwaka 1947 yalikuwa ni matokeo dhahiri ya ukuaji wake. American Temperance society (ATS) kilitokana na chama kilichokuwa na madhumuni yanayofanana, kilichoanzishwa kule Boston mwaka 1826 kabla ya kuanza kwa ujumbe wa marejeo.

e) Kuanzishwa kwa Seminari ya Kithioloji:
Ili kukabiliana na ukuaji wa kiwango cha elimu, seminari ya Thiolojia ya Waadventista wa sabato “Seventh-day Adventist Theological Seminary” ilianzishwa kule Washington D.C. mwaka 1936. Mwanzoni shahada za juu za fani ya sanaa tu ndizo zilizotolewa, lakini baadaye zimeendelea kuongezwa shahada zingine za juu katika fani zingine.

Mwaka 1960 Seminari hii ikafanywa kuwa Chuo kishiriki cha Andrews University ambayo ilipewa jina hilo kwa kumbukumbu ya mmishonari wa kwanza J.N. Andrews.

f) Kupanuka kwa mpango wa chakula bora:
Viwanda vya chakula bora vilijengwa mapema mwaka 1897. Viwanda hivyo katika nchi za U.S.A. Australia. New Zealand, Denmark, England, Ujerumani na nchi zingine vimedhihirika kuwa na msaada mkubwa kwa kazi ya kanisa kwa njia kadhaa.

Taasisi hizi zimekuwa za muhimu sana kwa namna tatu:
1) Kutoa chakula bora kwa taifa
2) Kutoa ajira kwa washiriki wa kanisa
3) Kutoa fedha kwa ajili ya Misheni na Elimu

g) Vita Kuu ya Pili ya dunia 1939 -1945)
Ilikuwa kabla ya muda kupita na hali ya uchumi kudhurika kutokana na ukata uliokuwa umeikumba dunia siku zile ndipo vita kuu ya pili ilipoanza kupiganwa, kuanza kwa vita kulisababisha kukabili vikwazo vingine vipya:
- Uhaba wa vifaa kama karatasi
- Shida ya usafiri
- Kuharibiwa kwa majengo na vifaa vingine
- Watendakazi wengine walizuiliwa, kulazimishwa kujiunga na jeshi au walitakiwa kuacha kazi zao za taaluma

Pamoja na hayo yote, mkono wa Bwana ulikuwa bado pamoja nao katika kazi yake na mafanikio ambayo hayakutarajiwa yalipatikana.

h) Miaka 10 ya Umoja na Maendeleo:
Hatua kadhaa muhimu zilizochukuwa kati ya mwaka 1931 -1941 zilikionyesha kipindi hiki kuwa ni cha kufikiwa kwa umoja wa hali ya juu na maendeleo, kwa mfano:
- Misingi ya imani yetu ilitayarishwa mwaka 1931
- Vyeti vya ubatizo vyenye muhtasari wa Misingi ya Imani Yetu, Agano na Kiapo vilitayarishwa mwaka 1941 (yapo maswali 13 ambayo wanafunzi wa ubatizo wanapaswa kuyajibu)
- Kuleta msisitizo wa pekee juu ya mafundisho yanayomfanya Kristo kuwa ndiye kiini cha ujumbe wetu.

h) Kupanuka kwa huduma ya Radio
Mtangulizi mwanzilishi wa kurusha matangazo kwa njia ya Radio alikuwa H.M.S. Richards. Wazo hili alilipata katika mwaka 1920 na kurusha matangazo yake ya kwanza mwaka 1926. Alianza kwa unyenyekevu mkubwa na kujidhili, ofisi yake ya kwanza ilikuwa banda la kuku lililofanyiwa ukarabati. Hadi ilipofika mwaka 1941, ndipo Sauti ya Unabii ilipokubaliwa kuwa ni mradi wa Kanisa. Hivi leo matangazo yanarushwa toka pwani hadi pwani nyingine katika divisheni ya marekani ya kaskazini kwa kutumia vituo takribani 800.

Vipindi vilivyohusishwa na Sauti ya Unabii vinasikika katika vituo zaidi ya 1,000 nje ya Marekani. Mtoto wa H.M.S. Richards alifuata nyayo za Baba yake na kuwa mtangazaji wa Sauti ya Unabii (VOP).

Masomo ya Biblia kwa njia ya Posta yamedhihirisha wazi kwamba ni bora na huleta mvuto kwa njia hiyo maelfu wameongozwa kuujua ukweli wa leo. Matangazo kwa njia ya radio yamefanikiwa sana katika nchi zingine pia na hivi sasa ni mojawapo ya njia muhimu ya Uinjilisti.

## SEHEMU YA KUMI

## KUKUA NA MSHIKAMANO 1947 – 1959

**a) Kukabili ulimwengu uliobadilika:**

Kanisa lilikabiliwa na kazi ya ukarabati mkubwa na ujenzi mpya wa miradi katika mwaka 1946. Pia ilikuwa dhahiri kwamba vita ilikuwa imebadilisha kabisa mwonekano wa watu katika mabara mbalimbali. Viongozi wa kanisa nao walilazimika kukabili ukweli kwamba matatizo yaliyosababisha kubadilika kwa mipaka yangesababisha pia uundaji upya wa baadhi ya Divisheni. Katika muda mfupi watendakazi wote wa kigeni walilazimika kuondoka kule China hata nchi nyingine nazo zikawa na msimamo mpya kuhusu makanisa ya kikristo na wamishonari.

Ilikuwa vigumu kupata taarifa za kuridhisha na zenye ufafanuzi wa kutosha kutoka katika nchi mbali mbali, kufanya safari likawa ni jambo gumu kwa sababu ya vitu kama vibali vya kuingia na kuishi.

**b) Kuendelezwa kwa Umishonari:**

Pamoja na matatizo hayo yote, moyo wa umishonari haukufa, viongozi wakajenga dhamira mpya ya kupanua mipaka ya Injili. Mara tu baada ya vita, Wamishonari walirejea tena katika maeneo waliyokuwa wameyahama na pia walifungua kazi katika maeneo mapya. Watendakazi wengi wa kutumainiwa walitweka kwenda nchi za kigeni kuwakusanya na kuwavuvia kondoo waliotawanyika.

- Chuo kilianzishwa kule Iceland mwaka 1950
- Hospitali ilifunguliwa kule Pakistani mwaka 1951
- Kituo cha yatima kilianzishwa nchini Korea mwaka 1951
- Huduma ya matangazo ya Redio ilianzishwa katika marekani ya Kusini

**c) Mmishonari wa zamani alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi:**

Tangu mwaka 1950 hadi 1954, Mmishonari aliyewahi kufanya kazi kule China na Afrika W.H. Brainson alichaguliwa kufanya kazi kama Rais wa Jenero Konferensi. Baadaye aliugua na hivyo mwaka 1954 R.R. Figuhr alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi katika mkutano mkuu uliofanyika mwaka huo. Figuhr alikuwa ameshawahi kufanya kazi kwa miaka mingi kule Ufilipino na marekani ya Kusini.

**d) Njia Mpya za Uinjilisti:**

Tangu mwaka 1950 mamilioni ya watu katika Marekani ya Kaskazini walipata ujumbe wa Injili wakiwa majumbani mwao kwa njia ya televisheni.

Kipindi cha televisheni cha imani ya leo, kilichoendeshwa na Mchungaji W.A. Fagal kilianzishwa kule New York, mwaka 1952. Shule ya Biblia iliyojulikana kama imani ya

leo ikaanzishwa. Kipindi kingine cha Televisheni kilichoitwa imeandikwa kichoandaliwa na George Vandeman kilianzishwa mwaka 1955, na hivi sasa vipindi vya televisheni vimekuwa njia muhimu ya Uinjilisti katika nchi mbali mbali zikiwemo Australia na Canada.

Kabla ya kufika katikati ya karne, viongozi wa Jenero Konferensi pamoja na watu wengine walibuni mikakati mipya ya kuhubiri katika makundi makubwa ya watu katika miji mikubwa ya dunia zana mbali mbali za thamani kwa ajili ya kutolea matangazo pamoja na mikakati kabambe ulifanyika. Vilinunuliwa viwanja kule London na New York na pia vituo 2 vya Uinjilisti vilifunguliwa. The New Gallery katika mtaa wa Regent, London na The New York Centre, karibu na Off Times, New York zilikuwa ni nyenzo muhimu zilizotumika kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu katika miji hii miwili muhimu.

Miaka mingi kabla mtumishi wa Mungu hajatamka kwamba kanisa ni lazima lifanye kazi ya kuhubiri kwa watu katika miji mikubwa, kazi muhimu ilikuwa imeshafanyika kwa ajili ya Wayahudi. Chama cha Maandiko ya Kiebrania. "The Hebrews Scripture Association", kilianzishwa mwaka 1955 na Gazeti la Isralite likawa likichapishwa kila robo.

**e) Hoja juu ya mafundisho:**

Baada ya Kanisa kufikia umoja na mwelekeo wa namna moja katika mafundisho ya namna fulani fulani ambayo yalizua malumbano kwa miaka mingi, wasomi wa Biblia waliojulikana kimataifa walianza kuuliza maswali juu ya imani ya Waadventista wa Sabato. Maendeleo hayo ya kupendeza yalianza mwishoni mwa miaka ya 1930 lakini yalishamiri katika miaka ya 1955 na 1956. Katika miaka hii viongozi wengi wa kanisa na wasomi wa Biblia walipata nafasi ya kujadili imani yetu sambamba na wanathiolojia kutoka katika nchi mbalimbali. Mijadala hii ilileta matokeo ya kuchapishwa kwa kitabu mwaka 1957 kilichojulikana kama "Seventh-day Adventist Answer Questions on Doctrine".

**f) Ukweli ulioambatana na takwimu:**

| | | |
|---|---|---|
| 1955 | - | Goli la utoaji wa Dola 100,000,000 kama matoleo ya sadaka ya shule ya Sabato lilitolewa kwa misheni kwa miaka kadhaa lilifikiwa na kuvukwa. |
| 1956 | - | Fungu lililotengwa kwa ajili ya kazi katika nchi za kigeni lilikuwa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 21. |
| 1957 | - | Kanisa lilikuwa linarusha matangazo katika vituo zaidi ya 961 vya redio kwa lugha 27. |
| 1958 | - | Kulikuwa na taasisi kubwa za Afya 102 na Kliniki 85 pamoja na Zahanati. Kule Marekani ya Kusini kulikuwa na vituo 10 vya Umishonari wa Kiganga. |
| 1959 | - | Washiriki wa kanisa ulimwenguni walifikia, 1,194,030 na matoleo ya zaka katika mwaka huo yalikuwa zaidi ya Dola milioni 53.5 |

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

## KUMALIZA KAZI YA INJILI 1960-----

**a) Kuongezeka kwa hali ngumu:**

Mjumbe wa Bwana alikuwa amelionya kanisa kwamba karibu na mwisho wa wakati kazi itabidi ifanywe katika hali ya ugumu zaidi. Hivi leo pamoja na matatizo mengine mengi hapa chini, ni baadhi ya mtihani wanaoupitia wale wote wanaoupeleka ujumbe wa malaika watatu "Kwa kila Taifa na Kabila na Lugha na Jamaa".

1) Dhoruba. Vita na kuchukiwa na mataifa
2) Kukosa uhakika na usalama katika ulimwengu
3) Ajali za nchi kavu, baharini na angani
4) Majanga katika ulimwengu kama mafuriko, Ukame, matetemeko na kimbunga
5) Dhiki na ukiwa
6) Hali ya kutengwa Utaifa
7) Dhoruba za Kisiasa na machukizo
8) Mabadiliko katika nyanja zote za maisha, mfano nyumbani kunakotawaliwa na talaka nyingi, katika mashule hakuna nidhamu, n.k.

Baadhi ya matatizo haya hayawagusi watu wa Mungu kwa kiasi kikubwa kwa sababu hayawahusu na hawana sehemu katika hayo. Wengine watajulikana kama askari wema wa msalaba hadi Kristo atakapokuja kuwachukua na kuwapeleka nyumbani.

Kutakuwepo Roho ya Upendo wa kindugu miongoni mwa watu wa Mungu, japokuwa tumetawanyika kati ya mataifa tunapaswa kuwa wamoja. Jukumu letu ni moja tu kuwapelekea watu ujumbe wa kumcha Mungu na kumtukuza na kuwatayarisha watu kumlaki Yesu ambaye atakuja punde. <u>Watendakazi pamoja na Mungu wanapaswa kuifanya kazi ya kuhubiri injili kuwa ndilo jambo lenye kuwapendeza</u> na kuachilia mbali ubinafsi na faida za kitambo tu na kwamba wautazamie mji ambao msanifu na mjenzi ni Mungu. <u>Katika kila kizazi na wakati wa matatizo, Mungu anao watu wake</u> wa kupeleka ujumbe, hebu kila mmoja wetu na awe tayari kuitikia wakati anapoitwa.

**b) Sauti ya kuwaamsha Mataifa:**

Tunaishi katika kipindi cha historia ya kanisa ambapo sauti inapaswa kusikika ikiwaamsha mataifa. Kama Yohana Mbatizaji alivyokuwa mtangulizi wa kuja kwa Kristo mara ya kwanza na sauti ilivyolihamasisha taifa la siku zile ndivyo ambavyo kanisa la Masalio linavyopaswa kutangulia na kutayaarisha njia kwa kuja mara ya pili kwa Bwana wetu Yesu Kristo na Sauti ya ujumbe wa malaika watatu ndiyo itakayoyaamsha mataifa leo. Katika kizazi hiki, Kanisa limeingia katika udhamini wa Uinjilisti wa aina mbali mbali. Ni vigumu kuandika kwa maneno katika kurasa hizi chache maendeleo mengi muhimu yaliyofanywa na Kanisa la Masalio.

Hapa chini yameorodheshwa baadhi ya maendeleo kuwa kama uthibitisho. Maendeleo yaliyofanyika ni katika kutangaza ujumbe wa Malaika watatu.

- Sauti ya Unabii, imani ya leo, Pumzi ya Uhai na Imeandikwa, vimezidi kuongeza wasikilizaji na watazamaji wake. Vipindi vingine mbali mbali vya radio na Televisheni. Pia vimewafikia watu wengi zaidi. Masomo ya Biblia kwa njia ya posta yanafanya kazi kwa ushirikiano na matangazo ya Redio na TV na vimeendelea kuwatayarisha makumi ya maelfu ya masomo kila mwaka.

- Makanisa mengi yamekuwa yakianzishwa. Hadi mwishoni mwa mwaka 1978 kulikuwa na Makanisa 20,446 duniani kote.

- Ili kuendeleza kazi ya Injili kwa haraka, ndege nyingi zilinunuliwa kwa ajili ya kutoa huduma katika maendeleo mbali mbali ya Misheni. Ndege hizi zilitumika kuwasafirisha wamishonari na zaidi sana kutoa huduma ya madaktari wanaosafiri.

- Idara ya vijana katika kanisa ilianzisha mpango wa "shiriki imani yako" "Share your Faith" katika miaka ya 1950. Matokeo yake, vijana wengi wa kanisa walijiunga katika shughuli za Kiinjilisti za aina mbali mbali. Mikutano ya Sauti ya vijana bado inaendeshwa kila mwaka katika Divisheni mbali mbali za ulimwengu. Katika mwaka 1964 msukumo wa pekee wa uinjilisti wa ulimwengu mzima kwa vijana wa MV (Missionary Volunteer) uliitishwa, vijana wa MV walijiwekea lengo la kuvuna roho 30,000.

- Katika kipindi hiki cha historia ya kanisa, kulikuwa na msisitizo wa kuendelea katika divisheni zote za ulimwengu juu ya Uinjilisti wa hadhara. Si jambo geni kusikia kwamba watu kati ya elfu kumi na elfu ishirini walihudhuria katika kampeni za mikutano ya namna hii, katika Divisheni mbali mbali za ulimwengu kumewekwa mpango kabambe wa kuhubiri katika kumbi za mikutano katika miji mingi mikubwa na midogo.

- Mpango wa siku tano wa kuzuia uvutaji ulianzishwa rasmi na Jenero Konferensi mwaka 1962. Mpango huu pamoja na mpango uliotayarishwa na idara ya kiasi, umetoa nafasi kwa maelfu ya watu kujua habari juu ya kanisa Masalio (siyo muhimu kufahamu tarehe za mwaka 1962).

- Kampeni za Mavuno huleta ghalani mamilioni ya fedha kila mwaka ambazo hutumika kwa ajili ya ustawi wa jamii, Utabibu na shughuli nyinginezo muhimu.

- Kuongezeka kwa Wamishonari wenye kuacha nyumba zao na kwenda nchi za kigeni kila mwaka. Na nchi nyingi zikawa chanzo cha kupeleka Wamishonari sehemu nyingine.

- Katika mwaka 1966, R.R. Figuhr alistaafu kuwa Rais wa Jenero Konferensi na R.H. Pierson alichaguliwa kuchukua nafasi yake.

| |
|---|
| Pierson ambaye alikuwa na uzoefu mkubwa wa kazi za huduma ambazo alizifanya katika sehemu mbali mbali ikiwa ni pamoja na Marekani, Asia ya Kusini, Trans-Afrika na Divisheni ya Marekani ya Kaskazini. Mwito wake kwa kanisa ulielekezwa katika "Toba Matengenezo na Uamsho". |

Mnamo mwaka 1978 katika mkutano mkuu wa mwaka, Pierson alitangaza rasmi kustaafu na Neal C. Wilson akachaguliwa kuchukua nafasi yake. Alichukua madaraka ya uongozi Januari 3, 1979 baada ya kufanya kazi Asia ya Kusini, Mashariki ya Kati na Marekani ya Kaskazini.

- Ili kuhamasisha zaidi kutangazwa kwa ujumbe wa malaika watatu, idara mpya kadhaa na huduma zikaanzishwa, ikiwa ni pamoja na idara ya uwakili na Maendeleo, Huduma ya vyakula, Huduma za Kutegemewa (Trust Services) na huduma za ukarimu kwa taasisi mbalimbali (Philanthropic services).

- Shule ya Sabato imeendelea kuwahimiza washiriki wa kanisa kushuhudia juu ya injili kwa majirani namarafiki. Matawi ya shule ya sabato, Masomo ya Biblia wakati wa likizo (Vocational Bible School) na sabato ya wageni vimewavuta watu wengi kwa ufalme wa mbinguni.

- Kanisa limehusika kwa sehemu kubwa kutoa msaada wakati kunapotokea dharura za kitaifa. Sadaka ya ulimwengu ya maafa na njaa sasa hutolewa kila mwaka.

- Mkutano mkuu wa 51 wa Jenero Konferensi ulifanyika katika mji wa Atlantic, New Jersey, mwezi June, mwaka 1970. Katika miaka ya 1970 hadi 1975 mfululizo, kanisa liliingia katika mpango mkubwa wa uinjilisti unaojulikana katika historia yake, mpango ulipoanza ulijulikana kama "Dhamira ya 1972" Idara zote za kanisa, washiriki, Walei pamoja na wahudumu waliungana pamoja ili kuwaleta watu kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

- “Matokeo ya Ushuhuda” kuendelea kuleta msisitizo mpya miongoni mwa makanisa ulimwenguni pote juu ya Roho ya Unabii.

- Vitabu na magazeti kutolewa kwa wingi sana kutoka katika mitambo ya uchapaji na kutawanywa kwa ulimwengu mzima kama miti idondoshayo majani wakati wa kiangazi.

- Ufinyu wa mapato kuongezeka, sababu kubwa kwa wakati ule ni kushuka thamani kwa dola ya Kimarekani. Lakini kwa ukarimu, watu wa Mungu waliendelea kujitoa na kuongeza matoleo.

- Jengo la ghorofa 10 sehemu ya Kaskazini ya Jenero Konferensi lilimalizika kujengwa mwaka 1972 na kuanza kutumika kwa ajili ya idara mbali mbali. Kadhalika ghorofa ya 10 ilitumika kama Bwalo la chakula.

- Mkutano ulifanyika katika kiangazi cha mwaka 1972 katika jiji la Mexico mwezi Oktoba na tangu wakati huo ndipo likaanzishwa jina Mkutano Mkuu wa kila mwaka.

- Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Jenero Konferensi kufanyika nje ya Marekani ulifanyika mwaka 1975 kule Vienna, Australia.

- Mkutano wa Jenero Konferensi wa mwaka 1980 ulifanyika Dallas Taxas katika mwezi April. Taratibu mtindo wa kufanya mikutano hiyo katika majira ya joto ukaepukwa.

- Kipindi kati ya mwaka 1975 hadi 1980, msisitizo uliwekwa katika kumaliza kazi ambayo goli la kubatiza watu 1,000 kwa siku moja liliwekwa. Ni katika kipindi hiki ambapo Divisheni ya Inter-American ikawa ndiyo Divisheni kubwa kuliko zote ulimwenguni kwa upande wa idadi kubwa ya washiriki.

c) **Mambo muhimu ya kukumbukwa:-**

Washiriki wa kanisa wa kuanzia mwaka 1960 na kuendelea wamekuwa na mambo mbali mbali ya kukumbukwa, ambayo huwakumbusha ambavyo Mungu amekuwa akiongoza katika siku zilizopita. Tunahakikishiwa kwamba, hatuna jambo lolote liwezalo kututisha isipokuwa kama tutasahau jinsi Bwana alivyotuongoza na mafundisho aliyotupatia kupitia katika historia.

Yaliyo orodheshwa hapa chini ni baadhi ya mambo muhimu ya kukumbukwa tangu miaka ya 1960 ilipoanza:

| | | |
|---|---|---|
| 1960 | - | Miaka 100 tangu jina Seventh-day Adventist lianze kutumika Rasmi. |
| 1961 | - | Miaka 100 tangu kuanzishwa kwa Konferensi ya kwanza |
| 1963 | - | Mwaka wa 100 tangu kuundwa kwa Jumuiya hii ya Jenero Konferensi (General Conference) |

| | | |
|---|---|---|
| 1966 | - | Miaka 100 tangu kuanzishwa kwa Kituo cha kwanza cha utabibu (Hospitali) |
| 1968 | - | Miaka 100 tangu kufanyika kwa mkutano wa makambi wa kwanza |
| 1972 | - | Mwaka wa 100 tangu kuanzishwa kwa mfumo wa Elimu wa Waadventista |
| 1974 | - | Miaka 125 tangu jarida la kwanza kutolewa pamoja na kazi ya uchapaji (The Review and Heralds dates from 1849). Miaka 100 tangu kutumwa kwa mmishonari wa kwanza.<br>Miaka 100 tangu kuanzishwa kwa "Signs of the Times"<br>Miaka 100 ya chuo Kikuu cha Andrews (chuo kilichochukua nafasi ya Battle Creek College) |
| 1975 | - | Miaka 25 ya chama cha Watafuta Njia |
| 1976 | - | Miaka 50 ya Ukambikaji wa Kiadventista |
| 1979 | - | Miaka 100 ya chama cha vijana cha Kwanza kule Hezelton, Michigan. |

**d) Idadi ya washiri kuvuka milioni tatu:**

Mwanzoni mwa mwaka 1978, washiriki wa kanisa waliobatizwa ulimwenguni pote walikuwa wameshazidi zaidi ya milioni tatu. Washiriki wa Shule ya Sabato walikuwa kadiri ya 3,700,000. Washiriki hawa wa Kanisa na Shule ya Sabato walipatikana katika nchi 190 za ulimwengu. Umoja wa mataifa unaorodha ya nchi 220 ambazo zipo katika ulimwengu. Kanisa lilikuwa likitoa huduma yake kwa kutumia lugha 590. vielelezo hivyo husaidia kuonyesha kwamba Kanisa la Waadventista wa Sabato linatimiza maneno yanayopatikana katika Ufunuo 14:6 kwamba ujumbe wa malaika watatu ungekwenda kwa kila taifa, na lugha na jamaa. Vielelezo vingine muhimu na takwimu kuhusu Kanisa vilivyopo vilivyopatikana hivi karibuni ni kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Washiriki wa Kanisa waliobatizwa | 3,117,535 |
| Idadi ya Makanisa | 20,446 |
| Washiriki wa Shule ya Sabato | 3,817,459 |
| Matawi ya Shule ya Sabato | 38,220 |
| Wachungaji waliowekewa mikono (wanaotenda kazi) | 8,976 |
| Shule zilizoendeshwa na Kanisa | 4,601 |
| Idadi ya Wanafunzi katika Shule hizo | 482,397 |
| Shule kando ya zile za watoto wadogo | 715 |
| Vyuo huko Marekani ya Kaskazini | 10 |
| Vyuo Vikuu | 3 |
| Shule za Kimataifa (kwa njia ya Posta) | 1 |
| Nchi ambazo Kanisa lilikuwa likitenda kazi (kati ya nchi 220 kwa Mujibu wa Umoja wa mataifa) | 190 |
| Lugha zilizotumiwa na kanisa katika kazi | 567 |
| Nyumba za Uchapaji | 50 |
| Lugha zilizokuwa zikichapishwa | 203 |
| Sadaka ya Misheni iliyopokelewa | $ 9,544,606 |
| Matoleo ya Kanisa kwa jumla | $ 516,629,624 |
| Zaka | $ 313,334,263 |

| | |
|---|---|
| Vituo vya Utabibu na Hospitali | 142 |
| Zahanati na Kliniki | 257 |
| Wauguzi wenye shahada (mnamo mwaka 1978) | 9,375 |
| Madaktari wa fani mbali mbali | 1,686 |

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## IDARA MBALI MBALI ZA KANISA

**Mambo muhimu kuhusu Idara**:

1) Zimeundwa ili kugawa majukumu na kutoa uongozi maalumu kila inapohitajika.
2) Dhumuni la kila idara ni kuongoa roho za watu kwa ajili ya Bwana wetu Yesi Kristo
3) Kazi za Idara ni kutoa ushauri na wala siyo utawala
4) Kuna Wakurugenzi wa idara katika ngazi zote. Makanisa, Konferensi/Misheni/Field/Union/Divisheni na Jenero Konferensi.
5) Viongozi wa Idara mbali mbali hushirikiana ili kutunza umoja na uwiano mzuri wa kazi katika ulimwengu wote.
6) Zipo baadhi ya idara ambazo zimepewa majina maalumu kama vile byuro (Bureau), Kamisheni, Chama au Huduma
7) Zipo pia baadhi ya Idara ambazo hutenda kazi katika sehemu fulani tu za ulimwengu, utendaji wake haujaenezwa mahali pote.
8) Nyingi ya idara zifuatazo hupatikana katika divisheni zote ulimwenguni.

**a) Idara ya Mawasiliano:**

Idara ya mawasiliano ilianzishwa na Jenero Konferensi mwaka 1972, ambayo ilihusisha kitengo kilichojulikana kama idara ya Uhusiano, Redio na Televisheni. Gazeti la idara hii linaitwa Tell. Miongoni mwa shughuli za Idara hii ya Mawasiliano ni pamoja na zile zilizokuwa zikifanywa na iliyokuwa idara ya Uhusiano Redio na Televisheni.

Uinjilisti kwa njia ya uhusiano wa jamii unalengo lile lile la kumtangaza Yesu Kristo, kuleta uhusiano bora kwa ajili ya Kanisa lake kupunguza mtazamo mbaya, kuzuia mwonekano mbaya na kuweka msingi kwa ajili ya Uinjilisti. Mchungaji wa Kanisa ni Afisa Uhusiano kwa ajili ya Kanisa. Lakini kila kanisa linapaswa kuwa na katibu wa mawasiliano ambaye atawasiliana na vyombo vya habari.

Vipindi vya Redio na Televisheni kama kile cha sauti ya Unabii (Voice of Prophecy). Imeandikwa (It is Written), Imani ya Leo (Faith for Today) na Pumzi ya Uhai (Breath of Life) vimekuwa vikitayarishwa na Idara hii ya mawasiliano. Kanisa la

Waadventista wa Sabato lilikuwa ndilo Kanisa la kwanza kudhamini vipindi vya dini redioni na katika Televisheni.

Bila shaka kipindi kinachofahamika zaidi ni kile cha "Sauti ya Unabii". Ni kipindi ambacho kimekuwa kikirushwa hewani na stesheni za redio zaidi ya 800 katika Marekani ya Kaskazini. Divisheni zingine nazo zina vipindi vyake vya redio na Televisheni katika nchi mbali mbali, Wachungaji hutoa ujumbe kwa njia ya redio kwa kutumia redio za nchi hizo.

**b) Idara ya elimu**

Wakurugenzi wa Elimu wanawajibika kuhusu mipango ya elimu kwa ulimwengu mzima kuanzia shule za awali hadi vyuo vikuu. Mfumo wa elimu wa kanisa la Waadventista wa Sabato ni wa aina yake, kwa sababu unatilia mkazo nyanja kuu nne za maendeleo ya mwanadamu, yaani Kiakili, Kimwili, Kiroho na Kijamii.

Waanzilishi wa Kanisa walianzisha shule ndogo ya mwaka 1872 kule Battle Creek na mwalimu wa kanisa wa kwanza alikuwa G.H. Bell. Hivi leo Kanisa la Waadventista wa Sabato linaendesha mpango mkubwa wa shule kuliko kanisa lingine lolote la Kiprotestanti.

Taasisi ya masomo ya nyumbani ni shule ya masomo kwa njia ya Posta ambayo hutoa nafasi ya masomo kwa wale ambao hawana nafasi ya kuhudhuria katika shule za Kanisa

**Machapisho ya Idara ya Elimu ndiyo makala za Elimu ya Waadventista.**

**c) Idara ya Afya:**

Madhumuni ya Idara ya Afya ni kutoa ushauri juu ya uanzilishi wa Taasisi za Afya kuwasaidia wahudumu wa Afya katika kazi zao na kuzisaidia Field na Konferensi kuanzisha mipango madhubuti ya Afya. Majarida kama "Life and Health na vitabu husaidia kueneza ujumbe wa Afya.

**d) Idara ya shughuli za Walei**

Idara hii inao wajibu wa kutoa mwongozo na mipango ya kulifanya kanaisa liingie katika huduma kwa ajili ya Yesu.

Idara hii ya huduma za Walei, hutilia mkazo Uinjilisti, hususani kwa kutumia njia zifuatazo:-

- Kusambaza vitabu, kujifunza Biblia, kampeni mbali mbali kama mavuno, huduma kwa jamii, uinjilisti wa Biblia kwa njia ya zawadi na masomo ya Biblia kwa njia ya Posta.

  Jarida la "The Adventist Layman" hutolewa kila robo na idara ya shughuli za Walei ya Jenero Konferensi .

e) **Idara ya Huduma -** Chama cha Huduma huwasaidia Wainjilisti, Wachungaji na Waalimu wa Biblia pamoja na kazi zao na husaidia kuiboresha kazi ya huduma. Chama cha huduma husaidia kazi ya uinjilisti wa hadhara katika kanisa. "The Ministry Magazine" ni gazeti maalumu linalotolewa na chama cha huduma. Zaidi ya hayo, gazeti hutoa nakala ya kila mwezi ya watendakazi na kanisa. Mafunzo kuhusu huduma hufanyika kila mara katika Divisheni zote za ulimwengu.

**f) Idara ya mambo ya Jamii na uhuru wa Dini:**

Idara hii ina kusudi moja tu, nalo ni kuhifadhi haki ya kila mtu bila kujali madhehebu au hali yake, haki hizo ni kuabudu, kuishi na uhuru ambao mwanadamu amepewa na muumbaji wake. Idara hii ya mambo ya jamii na uhuru wa dini imekuwa ikifafanua mawazo yanayohusu kanuni za kutenganisha kanisa na dola kwa viongozi mbali mbali wa Serikali kupitia katika magazeti ya "Uhuru wa dini".

**g) Idara ya uchapaji:**

Idara ya uchapaji inawajibu wa kuhimiza uchapaji na usambazaji wa maandiko ya Waadventista pamoja na kuwaingiza kazini, kuwapatia mafunzo na kuwasaidia Wainjilisti wa Vitabu katika kazi yao.

Hii ndiyo idara kongwe kuliko zote, kwani kazi ya uchapaji ilianzishwa miaka mingi iliyopita yaani 1849. Mtambo wa kwanza wa uchapaji ambao ulikuwa unatumia anguvu ya mvuke ulinunuliwa na mkulima mmoja kwa kumwuuza maksai wake. George A. King ndiye Mwinjilist wa vitabu wa kwanza, ambaye alianza kazi mwaka 1878. Hivi leo vitabu vinavyouzwa na wainjilisti kila mwaka vina thamani ya zaidi ya dola milioni 30.

**h) Idara ya Shule ya Sabato:**

Idara ya shule ya sabato imelihudumia kanisa kwa zaidi ya miaka 100 na inaendelea kuzingatia malengo yafuatayo:

1. Kuwawezesha washiriki wake wote kusoma neno la Mungu kwa mpango, Shule ya Sabato imekuwa ikijulikana kama Kanisa linalojifunza.
2. Kupeleka ujumbe kwa wale wote ambao bado hawajaufahamu
3. Kufanya fedha zinazotolewa kwa ukarimu kupatikana kwa ajili ya kupeleka Injili katika nchi za mbali.

Idara hii hutayarisha lesoni ya Shule ya Sabato ya kila robo, katika matoleo yake mbalimbali pamoja na jarida la "Mtenda kazi la mipango ya Shule ya Sabato na Jarida la kila mwezi kwa ajili ya Maofisa na Waalimu.

**i) Idara ya uwakili na maendeleo:**

Idara hii ya uwakili na maendeleo inaonekana kuwa mpya ikilinganishwa na idara nyingine. Kazi ya Mkurugenzi wake ni kuwaelimisha watu kuhusu wajibu wao kwa Mungu kama mawakili wake. Hii inajumuisha wajibu wao wa kurudisha zaka kwa uaminifu na kutoa sadaka zao kwa ukarimu. Wachungaji hulipwa mishahara kutokana na zaka na hawapaswi kujiingiza katika shughuli nyingine yoyote ili kujiongezea kipato chao.

Sehemu ya pili ya idara hii inayojulikana kama maendeleo, inalengo la kuliendeleza kanisa pamoja na taasisi zake. Japokuwa idara hii ilianzishwa siku za karibuni, yaani mwaka 1967, Divisheni zilizo nyingi katika ulimwengu zinao Wakurugenzi wake wa Uwakili na kumekuwa na ongezeko la kufaa katika urudishaji wa zaka na utoaji wa sadaka kama matokeo ya kuwapo kwa idara hii.

**j) Idara ya Kiasi**

Madhumuni ya idara hii ni kuhamasisha watu kujiepusha na vitu vyote vinavyodhuru kama tumbaku, mihadarati, pombe, pamoja na madawa yote yenye madhara. Watangulizi wa Kanisa la Wadventista wa Sabato waliweka msimamo madhubuti juu ya kiasi na kwa kipindi cha miaka mingi msimamo huo haukubadilika.

Gazeti kuu ambalo limekuwa likitolewa na idara hii ni lile la Sikiliza (Listen)

**k) Idara ya huduma za udhamini:**

Idara ya huduma za udhamini nayo pia mpya, ilianzishwa mwaka 1968, ikiwa na dhumuni la kutoa huduma kwa washiriki wa kanisa kuhusiana na uwekezaji wa fedha pamoja na ugawaji wa mali pindi kitokeapo kifo. Divisheni nyingi hivi sasa zinatoa huduma hii ya udhamini na mamilioni ya fedha yawezekana katika kanisa, kutolewa na kuwekewa wosia kwa kanisa. Mapato yanayaotokana na shughuli hii yamesaidia sana katika kutangaza ujumbe wa malaika watatu.

m) **Idara ya vijana:**

Kwa miaka mingi, "Idara ya Vijana wa kujitolea (Missionary Volunteer) lilikuwa ndio jina rasmi la Chama cha Vijana kanisani, lakini jina hilo lilibadilishwa mwaka 1978 na kuwa Idara ya Vijana wa Kiadventista (Seventh-day Adventist Youth Department) ambayo kifupisho chake sasa ni Adventist Youth Department. Idara hii inafanya kazi kwa njia ya vijana ambao wamegawanyika katika madaraja matatu kwa kuzingatia umri wao.

-Madarasa ya Wavumbuzi (Adventurers Classes), Kuanzia miaka 6 hadi 9. (Nyuki wa Shughuli Miali ya Jua, Mjenzi na Mkono wa Msaada)
Madarasa ya vijana wadogo (Adventist Youth) kuanzia miaka 16 hadi 30 - Kiongozi Mkuu na Kiongozi Mwadventista.

-Madarasa ya vijana wadogo (Adventist Junior Youth) kuanzia, miaka 10 – 15 Rafiki, Mwenzi, Mgunduzi, Msimamizi, Msafiri na Kiongozi.

Chama cha Watafuta Njia kilitambuliwa na Jenero Konferensi mwaka 1950. Madhumuni ya Idara ya Vijana ni kusaidia uwiano katika ukuaji wa kimwili, kiakili, kijamii na maisha ya kiroho ya kijana pamoja na kujifunza kujiandaa kwa ajili ya huduma ya Kikristo.

Shughuli za idara ya vijana zimeelezwa katika vitabu kama mwongozo kwa viongozi wa vijana (Youth Leaders Handbook), mafunzo ya huduma ya vijana (Youth Ministry Training). Mwongozo wa mafunzo (Course Manual). Mwongozo kwa Wakurugenzi kuhusu kukambika (Camp Directors Manual) na mwongozo kwa maofisa wa chama cha Watafuta Njia (Pathfinder Staff Manual). Jenero Konferensi huchapisha kila robo makala inayozihusisha idara mbali mbali ambayo huitwa "Youth Ministry Accent" Maalumu kwa ajili ya viongozi wa vijana katika makanisa "Kit Church School Focus" ambayo huwa na mipango na msaada kwa vijana wadogo. Hutumwa kwa waalimu wa shule zote za kanisa.

**l) Huduma ya chakula ulimwenguni:**

Idara hii ilianzishwa mwaka 1968 ili kusimami mipango ya kazi katika viwanda vya kutengeneza chakula bora katika ulimwengu mzima. Sekta hii ya chakula bora imeshuhudiwa kwamba ni mbaraka mkubwa kwa Kanisa na ilianzishwa kwa ushauri wa moja kwa moja wa Roho ya Unabii.

Mpango wa Wamishonari wanafunzi na ule mkakati maalumu kwa Vijana wa Kiadventista husimamiwa na Idara ya Vijana.

Mwaka 1978 sherehe za "Imani" pamoja na "Neno" zilianzishwa na idara ya vijana. Hii ilikuwa ni mikutano mikubwa sana ya vijana, ambapo washiriki wake ambao walikuwa wameshapata mafunzo awali walikutana pamoja ili kushuhudia katika mji au jamii ili kuwaandaa watu kwa ajili ya Uinjilisti wa mikutano ya ufuatiliaji. Aina nyingi za shughuli za kushuhudia zilitendeka huku washa zikiendeshwa ili kuwatayarisha vijana kuhusu njia mbali mbali za kuongoa roho. Tangu sherehe hizi kuanzishwa katika Amerika ya Kaskazini, hivi sasa zimekuwa zikifanyika katika sehemu mbali mbali za ulimwengu.

Mwanzo mpya wa mpango wa kujifunza Biblia kwa vijana ukihusisha miongozo ya usomaji dondoo za masomo, masomo yenyewe, pamoja na mawazo ya mahusiano katika kundi ulianzishwa katika mwaka 1979. Miongozo hiyo ya mafunzo ilihusisha mada zenye umuhimu mkubwa kwa vijana na zenye msaada kwa uhusiano wao na Yesu. Kanisa na familia pamoja na uchaguzi wa kazi.

Kanda iliyorekodiwa ilihusishwa katika kila mwanzo mpya ili kusaidia kwa namna sita mbali mbali.

Wakurugenzi wa vijana katika Jenero Konferensi tangu Idara ilipoanzishwa mwaka 1907 ni hawa wafuatao:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| M.E. Kern | 1907 | - | 1930 |
| H.T. Elliott | 1930 | - | 1933 |
| A.W. Peterson | 1934 | - | 1946 |
| E.W. Dunbar | 1946 | - | 1955 |
| Theodore Lucas | 1955 | - | 1970 |
| John Hancock | 1970 | - | 1980 |
| Leo Ranzolin | 1980 | | |

**n) Idara mbali mbali katika Amerika ya Kaskazini:**

Yapo mashirika ambayo hutenda kazi katika Divisheni ya Amerika ya Kaskazini tu, ambayo hayapo katika sehemu nyingine za ulimwengu; mfano mmojawapo ni ofisi ya mahusiano ya watu.

o) Hifadhi ya maandiko ya mama White:

Zaidi ya kuhifadhi maandiko ya Roho ya Unabii, wadhamini wa maandiko haya huyapanga kwa makundi, hutunza vitabu na kuvichapa vitabu kwa lugha mbali mbali.

Wapo wadhamini11 (kumi na moja) wa hifadhi ya maandiko ya mama Ellen G.White, lakini kwa hakika hii si Idara katika kanisa, haina makatibu wa idara katika Divisheni, Union au katika ngazi ya Konferensi. Arthur L. White ambaye ni mjukuu wa Ellen White alihudumu kama katibu wa hifadhi hiyo tangu mwaka 1937 hadi 1978. Baba yake aliyeitwa Wiliam C.White aliifanya kazi hiyo hiyo tokeo mama yake alipokufa mwaka 1915 na 1937. Robert Olson amekuwa katibu wa hifadhi hiyo tangu mwaka 1978.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

## DIVISHENI MBALI MBALI ZA KANISA ULIMWENGUNI

## INJILI KWA ULIMWENGU WOTE:

Kama tulivyoona katika kipindi cha miaka ya maendeleo katika Kanisa, kazi ya Uinjilisti kwa ulimwengu haikuweza kusahaulika. Katika siku za mwanzo kukiwa na watendakazi wachache pamoja na nyenzo hafifu. Marekani peke yake ilionekana ni eneo kubwa mno kuweza kufikiwa na ujumbe. Lakini Mungu alikuwa na mipango mikubwa kwa ajili ya watu wake. Kadiri Kanisa lilivyoweza kukubali, alifungua mlango mmoja baada ya mwingine.

Mwanzoni mwa miaka 1900, sehemu kubwa ya nchi za mbali zilikuwa zimefikiwa na Injili na kanisa lilikuwa limejitoa wakfu kwa kazi ya Uinjilisti.

Wamishonari watangulizi walikwenda katika mahali papya na kuanzisha Misheni, vituo, na katika muda mfupi kulikuwa na Fildi, Konferensi na Union. Mapema mwaka 1916 Divisheni zilianzishwa. Tangu wakati huo hadi sasa kumekuwa na divisheni kati ya 10 hadi 13 katika ulimwengu mzima. Kuanzishwa kwa nchi mbali mbali pamoja na hali ya kisiasa ambayo imekuwa ikijitokeza kadiri muda unavyoendelea imesababisha uanzishwaji wa Union na Divisheni zingine. Katika kipindi cha miaka mitano 1975 - 1980 Divisheni za ulimwengu zilikuwa kama ifuatavyo:-

a) **Divisheni ya Afro-Mideast EAD**
Divisheni hii ilianzishwa mwaka 1970. Ilipofika mwaka 1978 Jumuiya hii ilikuwa na makanisa 1060 yenye jumla ya washiriki 196,870. Zipo Union 4 katika Divisheni hii ambazo ni pamoja na zile za Afrika mashariki (Kenya) Ethiopia, Mashariki ya Kati na Tanzania. Makao makuu yake yalikuwa Beirut, Lebanon. Lakini ilipofika mwaka 1978 yalihamishiwa Nicosia, Cyprus. Divisheni hii inazo hospitali kubwa, Vituo vya Afya na shule, zaidi ya hayo inaendesha nyumba 3 za uchapaji, nyumba ya kuwatunza wazee pamoja na vituo 4 vya Uinjilisti.

b) **Divisheni ya Australasian**
Hii inajumuisha jumuiya ya Madola ya Australia, Muungano wa utawala wa New Zealand pamoja na visiwa vya Kusini mwa Pacific. Zipo Union Conferensi 2 ambazo huunda divisheni hii ambazo ni Trans-Tasmania na Australia pamoja na Union, Misheni zingine 3 katika visiwa ambazo ni Papua New Guinea, Central Pacific na Western Pacific. Washiriki wa kanisa katika divisheni hii hadi mwaka 1978 walikuwa 127,197 ambao waliabudu katika makanisa 108. Kulikuwa na shule za msingi na Sekondari zipatazo 300, pamoja na chuo cha Avondale. Taasisi ambazo husaidia vijana katika Divisheni hii ni pamoja na hospitali kadhaa, vituo vya afya, kliniki, vituo vya misaada, nyumba za kutunzia wazee pamoja na wajane.

Kampuni kubwa ya uchapaji ijulikanayo kama “Signs” ipo katika jimbo la Victoria, na kituo cha kampuni ya chakula bora chenye viwanda vya usindikaji 12 na vituo vya mauzo ya jumla pamoja na maduka ya rejareja yapatayo 70 katika sehemu yote ya Australia na New Zeland. Makao Makuu ya kanisa katika Divisheni hii yapo kule Wahroonga, Kitongoji kimojawapo cha Sydney, katika mtaa wa Fox Valley ndipo kuna makao makuu

ya Divisheni. Hospitali ya Waadventista ya Sydney, Kanisa la Wahroonga, Kituo cha Redio na Televisheni cha Waadventista, nyumba ya wageni ya Misheni, Shule ya Msingi na nyumba nyinginezo nyingi.

Eneo kubwa lenye thamani ambamo majengo haya yalijengwa lilinunuliwa kutokana na ushauri wa EllenG. White ambaye alikuwa akiishi Australia katika siku hizo.

**c) Divisheni ya China:**
Kutokana na jinsi hali ilivyo huko China hakuna habari za karibuni zinazoeleza jinsi kazi inavyoendelea huko. Wamishonari walioko nchini humo walipoondoka kulikuwa na taasisi za Afya, Shule, Mitambo ya Uchapaji na makanisa mengi. Kutokana na mabadiliko ya uhusiano wa Kimataifa kati ya China na Marekani, mwaka 1979 ilitarajiwa kwamba mabadiliko makubwa yataonekana katika maendeleo ya kazi ya kanisa.

d) **Makundi ya Waadventista** wa Sabato katika Jamhuri za Muungano wa Kisoshalisti za Urusi (USSR). Hakuna takwimu sahihi zilizopatikana karibuni kuhusu makundi ya Waadventista wa Sabato katika Jamhuri za Muungano wa Kisoshalisti za Urusi. Lakini Union, Konferensi ilianzishwa huko mwaka 1978. Tarakimu za mwisho zilionyesha kwamba kulikuwa na makanisa 834 yenye washiriki 40,000 katika tawala hizo kubwa za Muungano wa Jamhuri za Kisoshalisti za Urusi (USSR)

**e) Divisheni ya Euro-Afrika**

Divisheni hii iliundwa upya mwaka 1971 na hufanywa na tawala ambazo zamani zilikuwa chini ya iliyokuwa Divisheni ya Ulaya ya Kati (Central European Division). Hii inajumuisha Ujerumani, Kusini mwa Ulaya, sehemu kubwa ya mashariki mwa Ulaya, Sehemu ya Afrika hususani kaskazini Magharibi pamoja na sehemu ya Ikweta na Israeli.

Makao Makuu ya Divisheni hii yapo Berne, Switzerland. Miongoni mwa taasisi nyingi zinazoendeshwa na Divisheni hii ni nyumba ya Uchapaji ya Hamburg, Kituo cha Afya cha lake Geneva pamoja na Seminari ya Waadventista ya Kifaransa. Katika Divisheni hii kuna Union zipatazo 16 zenye Makanisa yenye jumla ya washiriki 232,081 kwa takwimu za mwaka 1978.

**f) Divisheni ya mashariki ya Mbali**

Makao yake Makuu yako Singapore. Divisheni hii huundwa na Union, Misheni zifuatazo: Korea, Japan, Visiwa vya Kusini mwa China, Ufilipino Kaskazini, Ufilipino Kati, Ufilipino Kusini, Asia Kusini mashariki, Indonesia, Mashariki pamoja na Indonesia Magharibi. Hadi mwaka 1978 katika eneo hili kulikuwa na Makanisa 2892 yenye jumla ya washiriki 349,148. Katika kitabu cha kumbukumbu za matukio ya kanisa cha mwaka huo kilionyesha kwamba kadiri ya shule 60 zilikuwa zimeorodheshwa katika orodha ya Shule za kanisa katika Divisheni hii pamoja na Hospitali, vituo vya Afya, Zahanati na Kliniki nyingi. Pia zipo nyumba za Uchapishaji zipatazo 7 na Hospitali ya Waadventista ya Seoul ambayo pia huhudumia wajane inayojulikana sana.

Divisheni hii ya mashariki ya mbali iliundwa mwaka 1919 na ujumbe umeenea kwa haraka sana katika nchi hizi Mashariki mwa bahari ya Mediteranean.

g) **Divisheni ya Inter-Amerika;**

Mnamo mwaka 1978, Divisheni hii ilikuwa na makanisa yapatayo 2472 yaliyokuwa na jumla ya washriki 519,908; Tangu wakati huo, Divisheni hii imekuwa ndiyo kubwa kuliko zote ulimwenguni. Eneo hili ambalo kazi imekua kwa kasi ilibatiza watu zaidi ya 1000 kwa juma katika kipindi cha miaka ya 1977 na 1978. Makao yake Makuu ni Miami, Florida. Divisheni hii huendesha Hospitali nyingi, Kliniki na Shule ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Montemorelos, Mexico na mtambo wa Uchapaji wa Pacific Press. Lugha 4 kuu hutumika katika eneo hili ambazo ni Kihispania, Kidachi, Kifaransa na Kiingereza.

h) **Divisheni ya Amerika ya kaskazini:**

Kanisa katika Divisheni hii linahusisha Marekani, Canada na Bermuda. Divisheni hii kubwa zenye Washiriki 551,884 waliomo katika Makanisa 3850, Kufuatana na takwimu za mwaka 1978, huundwa na Union 10, pia Divisheni hii huongozwa na Jenero Konferensi na huongozwa na Makamu wa Rais wa Jenero Konferensi ambaye huchaguliwa ili kusimamia maendeleo ya kazi katika Divisheni. Vipo Vyuo Vikuu 2 na Vyuo vingine 12 na Shule za msingi na Sekondari zipatazo 1315 zinazoendeshwa na Divisheni hii pamoja na Hospitali nyingi za kuvutia na Taasisi nyingine. Nyumba kubwa 3 za uchapaji ni Pacific Press, Review and Herald na Southern Publishing Association. Taasisi nyingi katika Divisheni hii huifanya kuwa chimbuko la vituo vya mafunzo ya ugavi wa watendakazi ulimwenguni pote. Ni nyumba iliyo muhimu sana ya msingi. Kwa kuwa karibu asilimia 70 ya fedha zote za kanisa hutoka huko, na hutuma wamishonari wengi katika nchi za kigeni kila mwaka.

i) **Divisheni ya Ulaya ya kaskazini na Afrika Magharibi** (Norther Europe-West Africa)

Katika eneo hili la ulimwengu, kadiri ya watu milioni 218 huishi eneo ambalo huundwa na Union 8 pamoja na Konferensi ya Iceland. Makao Makuu ya Divisheni hii yapo St. Albans, England, karibu na jiji la London. Union zinazounda divisheni hii ni pamoja na British, Finland. Nertherlands, Nigeria, Polish, Sedish, West-African na Est Nordic. Hadi mwaka 1978 jumuiya hizi zote zilikuwa na makanisa yapatayo 1118 yenye jumla ya washriki 113,898.

Zipi Taasisi 21 za elimu katika Divisheni hii ikiwa ni pamoja na Chuo cha New Bold, pia kuna Hospitali, Zahanati, Kliniki, Makambi ya Wastaafu, Wajane pamoja na nyumba za Uchapaji, nyumba ya uchapaji ya Stanborough Press ambayo imeunganishwa na Review and Herald. Kuna makampuni 4 ya chakula katika Divisheni hii pamoja na kituo cha Uinjilisti kinachojulikana kama New Gallery katika Mtaa wa Regent katikati ya jiji la London.

e) **Divisheni ya Amerika ya Kusini:**

Divisheni hii ilianzishwa mwaka 1916, Makao yake Makuu yakiwa kule Brasilia, Brazil. Zipo Union 6 zinazounda Divisheni hii ambazo ni Australia Chile, East Brazil, North Vrazil, South Brazil na Inca. Kulingana na takwimu za mwaka 1978, katika eneo hili kulikuwa na makanisa yapatayo 1392 yenye jumla ya Washiriki wapatao 400,876. Divisheni hii pia inazo Shule nyingi, Hospitali, Vituo vya Afya, Zahanati na Kliniki, inao Waganga Wamishonari 14 ambao huendesha Huduma ya Kliniki ya kuhamahama pamoja na huduma ya ndege. Kuna nyumba ya kutunza wazee, yatima na nyumba za uchapaji. Miongoni mwa Taasisi za Elimu inayojulikana sana katika historia ya Kanisa ni Chuo

cha Mafunzo cha Lake Titicaca cha kule Peru. Vyuo vingine vinavyotambulikana sana katika historia ya Waadventista ni vile vya Plate River cha Argentina na Brazil College.

**f) Divisheni ya Asia ya Kusini (Southern Asia)**

Katika eneo hili la ulimwengu kuna wakazi zaidi ya milioni 830 na ndio eneo lenye wakazi wengi kuliko eneo lolote la Divisheni nyingine ulimwenguni. Kulikuwa na Makanisa 766 na Washiriki wapatao 90,214 katika mwaka 1978.

Makao makuu ya uongozi wa Divisheni hii yapo kule Poona, India. Eneo hili pia linaundwa na Union 6 ambazo ni Burma, Central India, Norther Pakistan, South India na Sri Lanka na pia sehemu ya Bangladesh.

Miongoni mwa Taasisi za Elimu ni pamoja na Spicer Memorial College, Hospitali Kliniki, Zahanati pamoja na nyumba za uchapaji inazo pia na zimetapakaa katika eneo hili lote pamoja na nyumba ya uchapaji ya Oriental Watchman iliyoko Poona ambayo ni maarufu sana.

**k) Division ya Trans-Africa**

Divisheni hii inaundwa na nyingi ya nchi zilizopo barani Africa Kusini mwa Ikweta. Idadi ya washiriki imekuwa ikiongezeka kwa kasi katika Divisheni hii na hadi kufikia mwaka 1978 kulikuwa na idadi ya washiriki wapatao 306,514 katika makanisa 1941.

Zipo pia shule nyingi, mahospitali, Zahanati, Kiliniki, Nyumba za uchapaji. Miongoni mwa taasisi zinazojulikana sana katika eneo hili ni chuo cha Solusi, Helderberg, Sentinel Publishing Association na Hospitali ya Malamulo. Zipo ndege kadhaa za Misheni ambazo hutumika katika eneo hili.

Misheni nyingi zilianzishwa katika eneo hili mwanzoni mwa miaka ya 1900. Pamoja na vikwazo vingi, kazi imekuwa ikiendelea kukua kwakasi katika Divisheni hii.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## MARAIS WA JENERO KONFERENSI

**JOHN BYINGTON** Alishika madaraka hayo kati ya Mei 20, 1863 - Mei 17, 1865. Kabla ya kupokea ujumbe wa malaika wa tatu, Byington alikuwa ni muumini wa kutegemewa katika Kanisa la Kimethodisti ambapo aliwahi kuwa mchungaji wa Wesley. Halikuwa jambo rahisi kwake kukubali ukweli juu ya Sabato, Lakini alichagua kutii mambo yaliyodhahiri. "Kama asemavyo Bwana". Kanisa la kwanza la Kiadventista lilijengwa katika ardhi iliyomilikiwa na Byington Kule Buck's Bridge, New York. Kadhalika Shule ya kwanza ya Kiadventista ilifundishwa na binti yake Martha huko huko Buck's Bridge. Huyu ndiye aliyekuwa Rais wa kwanza wa Jenero Konferensi.

Alizaliwa mwaka 1798, Hinesburg, Vermont, baba yake alipata kuwa Askati wa Vita vya Mapinduzi ya Kijeshi na Mhubiri wa kuhamahama wa Kimethodisti ambaye aliishi hadi mwaka 1887.

**JAMES WHITE** Alikuwa Rais wa Pili wa Jenero Konferensi ambaye alitenda kazi katika awamu ya kwanza tangu Mei 17, 1865 hadi Mei 14, 1867. Alikuwa ni miongoni mwa watu waliofanya kazi ya kuhubiri ujumbe wa marejeo bila kuchoka. Katika kipindi chake alifanya mambo 3 makuu ambayo ni kupanga mafundisho kuhusu marejeo, kutayarisha muundo wa Kanisa na kusaidia uanzishaji wa Taasisi mbali mbali.

Mwaka 1963 alichaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Jumuiya hii mpya ya Jenero Konferensi. Hata hivyo alikataa kwa sababu alihusika katika kuhamasisha wazo la kuanzishwa kwa Jumuiya ili kuleta msukumo. Hakukubali kuchaguliwa na badala yake John Byington akachaguliwa kuwa Rais wa kwanza.

Zaidi ya kuwa kiongozi bora na Mhubiri mwenye nguvu, pia yeye na familia yake walikuwa na karama ya uimbaji. Alikuwa mwandishi mzuri na mhariri na aliweza kuanzisha gazeti la kwanza la Waadventista wa Sabato "Present Truth", vile vile yeye ndiye mwanzilishi wa Review and Herald, Youth's Instructor na Signs of the Times.

Alizaliwa Agosti 4, 1821, Palmyra, Maine; Watumishi wa mtoto mchanga aliyezaliwa katika mwezi wa Maua "Mayflower". Alikufa mwaka 1881 siku mbili tu baada ya kutimiza umri wa miaka 60 na kisha kuzikwa Battle E-reek kando ya makaburi ya nduguze.

JOHN N. ANDREWS Mei 14, 1867 hado Mei 18, 1869 akiwa na umri wa miaka 21 alianza kazi ya kuhubiri pamoja na uandishi. Akiwa mwanafunzi mwelekevu aliweza kumudu lugha za Kilatini, kiyunani, Kiebrania na Kifaransa na baadaye akajifunza Kijerumani na Kiitalia. Alikariri Agano Jipya na pia alikuwa Mwadventista wa kwanza kutumia Ufunuo 13 na kutetea utunzaji wa Sabato wa jioni hadi jioni.

Alikuwa ni Kiongozi wa kutumainiwa katika kanisa la mwanzo wakati kulipohitajika sana msukumo wa pamoja na injili na kwa utoaji wa mpango ili kusaidia kazi ya huduma.

Baada ya kutumika kama Rais wa Jenero Konferensi na kwa muda kama Mhariri wa gazeti la Review alitumwa tena Ulaya kama Mmishonari wa kwanza wa Kanisa huko. Kwa bahati mbaya aliugua ugonjwa wa Kifua Kikuu na baadaye kufa huko Switzeland mwaka 1883 akiwa na umri wa miaka 54 (alizaliwa nchini Poland, Maine mwake 1829).

Hivi leo kumbukumbu yake inaendelea kuwepo kupitia kwa jina la Chuo Kikuu cha kwanza cha Waadventista wa Sabato - Andrews University. Moja ya vitabu vyake bado vinaendelea kutumika hata leo kwa mfano kitabu cha Historia ya Sabato (History of Sabbath)

JAMES WHITE Alichaguliwa tena kuwa Rais wa Jenero Konferensi baada tu ya J. Andrews na alitumika kuanzia Mei 18,1869 hadi Disemba 29,1871.

GEORGE I. BITLER Disemba 29, 1871 – Agosti 10, 1874, George ambaye alifuata baada ya James White kama Rais wa Jenero Konferensi mwaka huo wa 1871 alikuwa ni kijana Mlei mwaminifu ambaye aliwekwa wakfu kuwa Mchungaji na kuchaguliwa kuwa Rais wa Konferensi ya Iowa kwa wakati mmoja (mwaka 1865)

Miaka iliyofuata karibu na kutokea kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe kule Amerika, ilikuwa ni miaka ya shida na hivyo viongozi walikumbana na matatizo mengi. Pamoja na hayo yote, aliendelea kuwa mtu mwenye nguvu.

Katika kipindi cha miaka 11 alichotumika kama Rais wa Jenero Konferensi, kilikuwa ni kipindi cha kukua na kupanuka kwa kasi kwa kazi. Alifanya safari nyingi katika Amerika na mara moja alipata kutumia miezi kadhaa kule Ulaya kusaidia uanzishwaji wa kazi. Mwaka 1888 ilikuwa hapana budi kwake kupumzika katika utumishi, lakini mwaka 1901 akachaguliwa kuwa Rais wa Konferensi ya Florida na mwaka 1902 akaitwa kuwa Rais wa Union ya Kusini (Southern Union). Baada ya kustaafu hotuba zake zenye mguso ulio dhahiri na makala zenye kusihi ziliendelea kutoa mchango muhimu kwa maendeleo ya kazi hadi alipokufa mwaka 1918. (Alizaliwa kule Waterburu, Vermont, mwaka 1834).

JAMES WHITE Alihudumu tena kama Rais kuanzia Agosti 10, 1874 hadi Oktoba 6, 1880.

GEORGE I. BUTLER Alihudumu tena kama Rais kuanzia Oktoba 6, 1880 hadi Oktoba 17, 1888.

OLE A. OLSEN Oktoba 17, 1888 hado Februari 19, 1897, akiwa na umri wa miaka 29 Olsen mwana wa Mhamiaji wa Kinorwey, alichaguliwa kuwa Rais wa Konferensi ya Wasconsin, wengine walimwita Rais Mvulana, lakini alifanya kazi njema na matokeo yake akachaguliwa kutumika kwa kipindi cha pili na kisha akawa Rais wa Konferensi za Dakota, Minnesota na Iowa. Mwaka 1886 alitumwa kusimamia kazi katika Scandinavia.

Akiwa na umri wa miaka 43 akachaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi na aliendelea kutenda kazi hiyo kwa miaka 9. Baadaye alikaa kwa mwaka 1 Afrika na katika mwaka 1898 alirudi Ulaya ili kuendelea kuongoza kazi. Mwaka 1901 aliombwa kusimamia kazi Uingereza. Baadaye akaenda Australia halafu katika miaka yake ya mwisho alifanya kazi Marekani. Kazi yake kubwa sana ilikuwa kuhudumia wageni katika nchi ile. Amejulikana kama mmoja wa viongozi waliopendwa sana. Janauari 29,1915 akiwa bado madhubuti na mkamilifu katika kazi ya kuongoa roho akafa ghafla akiwa kazini. (Alizaliwa Norway mwaka 1845).

GEORGE IRWIN Februari 19, 1897 hadi April 2, 1901. alizaliwa Ohio, Novemba 17,1844. mama yake alifariki yeye akiwa na umri wa miaka 9 na alipofika umri wa miaka 17 akajiunga na jeshi. Baada ya kupigana katika vita 17 alichukuliwa mateka. Ilikuwa katika kipindi hiki hali bado akiwa gerezani ndipo alipojitoa kwa Mungu. Aliipokea imani ya Waadventista wa Sabato mnamo mwaka 1885.

Mara tu baada ya kuupokea ujumbe huu alipewa kuwa msimamizi wa makanisa machache katika Ohio, na baadaye alihudumu kama mhazini na kisha Rais wa Konferensi hii. Aliwahi kuwa Mkurugenzi wa kanisa Kusini mwa Marekani na mwaka 1897 aliitwa kuwa Rais wa Jenero

Konferensi. Baada ya kuhudumu katika nafasi hiyo kwa miaka 4 aliwekwa kuwa Rais wa Union ya Australia. Mwaka 1905 alirudi Marekani na kuendelea na kazi hadi kifo chake mwaka 1913.

AURTHUR G. DANIELLS April 2, 1901 hadi Mei 11, 1922 Arthur Grosvenor Daniells Kiongozi aliyekuwa na msukumo wa hali ya juu kufanya maendeleo ukiacha James White, alikuwa ni mtoto wa Mganga na Mpasuaji. Alizaliwa Lowa mwaka 1858 na kubatizwa mwaka 1868 na mchungaji George I Butler. Baada ya miaka kadhaa ya kazi ya huduma ya Uinjilisti nchini Marekani, alitumwa kwenda New Zeland na Australia ambako alidumu kwa miaka 14. Alihudumu kama Rais wa kwanza Union Konferensi ulimwenguni ambayo ilianzishwa Australia mwaka 1894. Alipokuwa Australia alikuwa na uhusiano wa karibu na Ellen G. White ambaye bila kujua alimfundisha kazi kubwa ya kupanga na kupanua kazi na kwamba baadaye angeongoza ulimwengu wote.

Alirudi tena Amerika na kuhudhuria mkutano wa Jenero Konferensi kule Battle Creek mwaka 1901 ambapo alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi. Aliendelea kuchaguliwa mara kadhaa na hivyo alihudumu kwa miaka 21 kama Rais chini ya uongozi wa Mungu na kwa mahashauri ya Ellen G. White, mchungaji Daniells aliongoza kanisa kipindi ambacho maendeleo ya kanisa hayakutegemea uzoefu. Katika kipindi hiki, uongozi wa kanisa ulifanya mageuzi kwa kugawa majukumu, Misheni Field zilianzishwa na kuendelezwa sana kuliko ambavyo haikudhaniwa wakati uliopita.

A.G. Daniells baadaye akawa kana kwamba ni msafiri wa kudumu katika ulimwengu akitumia miezi kadhaa katika sehemu zingine mbali na Marekani Miaka 13 ya mwisho wa maisha yake aliitumia katika kusafiri, kuandika na kufanya Uinjilisti. Aliongoza katika uundaji wa chama cha Huduma pamoja ya Gazeti la huduma. Kitabu chake cha mwisho alikimalizia akiwa katika kitanda chake cha mauti mwaka 1935. Kilikuwa kinafuatilia historia ya Ofisi ya Unabii. “The Abiding Gift of Prophecy”.

WILLIAM SPICER Mei 11, 1922 - Mei 28, 1930. Mtoto wa waalimu Wabaptist Wasabato, William Abrose Spicer alizaliwa mwaka 1865 Minnesota. Familia ya Spicer ilikubali imani ya Waadventista mwaka 1874. Kazi yake ya kwanza katika Jenero Konferensi ilikuwa ni ukatibu kwa Stelhen N. Huskell kule Uingereza. Huko alisaidia uchapaji wa gazeti la ukweli wa leo “The Present Truth” pamoja na kuanzisha kazi ya mwanzo kabisa ya uinjilisti wa Kiadventista kula London. Baadaye alihudumu kama Mhariri wa Gazeti la Oriental Watchman pamoja na kufanya kazi ya kuongoza kwa muda mfupi kule India.

Kuanzia mwaka 1903 – 1922 Mchungaji Spicer alikuwa katibu wa Jenero Konferensi wakati ambapo Daniells alikuwa Rais wa Jenero Konferensi alikuwa mwenye kuwajibika katika kazi pande zote ulimwenguni. Tangu mwaka 1909 – 1911 na baadaye tena kwa kipindi kifupi mwaka 1945 alikuwa Mhariri wa Review and Herald.

Katika mkutano mkuu wa Jenero Konferensi wa mwaka 1922, alichaguliwa kuwa Rais na aliendelea kuhudumu hadi mwaka 1930 wakati ambapo kazi ilikuwa imeendelea kupanuka sana. Kumbukumbu za safari zake zilionyesha kwamba kati ya mwaka 1900 na 1940 kila mwaka alisafiri kwenda nchi za mbali isipokuwa katika miaka 4. alijulikana mahali pote katika kanisa kwamba ni Mhariri na Mwandishi mwenye kufanikiwa na pia alikuwa ni Mhubiri mweneye nguvu, uwezo mkubwa wa kufanyiza mipango na mmishonari aliyehamasika. Alikufa mwaka 1952, Takoma Park.

CHARLES. H. WATSON Mei 28, 1930 - Mei 26, 1936. katika mkutano mkuu wa Jenero Konferensi wa mwaka 1930 ndipo Watson alipochaguliwa kuwa Rais. Alikuwa ndiye mtu wa kwanza toka Australia kushika wadhifa huu wa kuwa Rais katika Divisheni ya Australian na vile vile wa Jenero Konferensi. Alizaliwa mwaka 1877 katika kijiji chenye utulivu kule Victoria. Uongozi wa Mchungaji Watson ambaye alijulikana kwa uwezo wa kifedha ulikumbwa na ukata wa dunia nzima. Hali mbaya ambayo haikuwahi kutokea nchini Marekani kama tulivyoona katika sehemu zilizotangulia katika kitabu hiki, kwamba pamoja na vikwazo vingi vilivyojitokeza lakini kazi ya Mungu ilisonga mbele. Familia ya Watson ilirejea tena kutumika katika nchi ya kwao. Alikufa mwaka 1962 kule Sydney.

J. LAMAR MCELHANY Mei 26, 1936 – Julai 10, 1950. Mmishonari Mtangulizi katika Divisheni ya Mashariki ya Mbali J.L. McElhany alihudumu kama Rais wa Jenero Konferensi kwa kipindi cha miaka 14. Alizaliwa Calofinia mwaka 1880 na kusoma katika shule za umma pamoja na Chuo cha Healdsburg (1900-1901). Na baadaye alifanya kazi ya Biblia na vijizuu kule Califonia. Utume wa kwanza kwenye nchi za mbali ulihusu Uinjilisti kule Australia (1903 - 1906) katika kipindi hicho yaani mwaka 1904 aliwekwa wakfu kuwa Mchungaji. Baada ya miaka 2 alikuwa Manila ambako alijifunza lugha pamoja na Uinjilisti. Alihamishiwa Newsland mwaka 1908 kwa ajili ya kazi ya Uinjilisti. Aliporejea marekani mwaka 1910 kwa muda mfupi alikuwa mchungaji wa wanafunzi katika kituo cha Boulder-colorado na pia kama mchungani wa kanisa. Baadaye alifanya kazi ya namna hiyo katika kituo cha Washington pamoja na Hospitali. Mwaka 1913 aliteuliwa kuwa Rais wa Konferensi kuu ya New York na huu ulikuwa ndiyo mwanzo wa mfululizo wa kuwa katika nafasi za uongozi bila jambo kuingilia kati ambao ulimfikisha katika kuwa Rais wa Jenero Konferensi kuu ya New York na huu ulikuwa ndiyo mwanzo wa mfululizo wa kuwa katika nafasi za uongozi bila jambo kuingilia kati ambao ulimfikisha katika kuwa Rais wa Jenero Konferensi. Tangu mwaka 1950 hadi kifo chake mwaka 1959 alikuwa Katibu wa mambo ya Utendaji kwa ujumla katika Jenero Konferensi.

WILLIAM H. BRANSON Julai 10, 1950 – Mei 24, 1954 alikuwa Mwinjilisti, Mtunzi, Kiongozi wa Konferensi pamoja na Jenero Konferensi. Alizaliwa Illinois mwaka 1887 na kupata elimu yake katika chuo cha Battle Creek pamoja na Chuo cha Kimishonari cha Emmanuel. Kazi yake ya utumishi Kanisani imekuwa takribani miaka 50. alianza mwaka 1906 wakati alipoingia katika kazi ya Uinjilisti wa Vitabu. Uinjilisti katika Florida ulifuatiwa na kazi ya kichungaji Kusini mwa Carolina na hatimaye kuwekwa wakfu kwa kazi ya kichungaji mwaka 1911. Aliitwa kutimika kama Rais wa Konferensi ya Kusini mwa Calofinia na kwa miaka 43 iliyofuata alishika nafasi mbali mbali za uongozi.

Mwaka 1920 aliteuliwa kuwa Rais wa Divisheni ya Afrika na akaendelea kuongoza eneo hili la ulimwengu lenye kukua kwa haraka hadi mwaka 1930, alipochaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jenero Konferensi.

Mwaka 1938 alihudumu kama Mkuu wa Divisheni ya Ulaya ya kati (sehemu ya 11) na kuanzia mwaka 1938 hadi 1940 akawa Mkuu wa Divisheni ya China. Mwaka 1946, kipindi ambapo kulikuwa na hali ngumu sana katika China alipelekwa ili kuongoza matengenezo ya kanisa na baadaye akahudumu kama Rais wa Divisheni ya China kuanzia mwaka 1946 – 1949).

Alikuwa ni Kiongozi hodari, mtu wa matendo ya kujenga kiroho na kimwili na vile vile anajulikana kuwa ndiye mwanzo wa kazi Kusini mwa Afrika, kando ya kutoa mchango mkubwa katika nyaraka mbali mbali za kanisa, aliandika vitabu kadhaa vikiwamo vile vya “The Way to Christ” “Missionary Adventures in Africa”, The Holy Spirit” “In defence of the Faith” “How

many are saved" na "The Dama of the Ages". Alistaafu mwaka 1954 kwa sababu ya hali mbaya ya kiafya na alikufa mwaka 1961.

REUBEN R. FIGUHR Mei 24, 1954 - June 16, 1966. Alizaliwa superior, Wisconsin, Oktoba 20, 1896. Figuhr alipata elimu yake ya awali katika Majimbo ya Magharibi ya Washington, Montana, Idaho na Oregon. Alifanya kazi ya Kiuchungaji. Alifundisha shule na pia aliitwa kujiunga na jeshi katika vita ya kwanza ya dunia na baadaye alijiunga na Chuo cha Pacific Union kisha Chuo cha Wakawaka ambako alihitimu mwaka 1922. Baada ya kuhitimu Elimu yake ya Chuo. Mchungaji Figuhr alifanya kazi kama Mchungaji na Mwinjilisti katika Oregon hadi alipoteuliwa kuwa mmishonari katika nchi za mbali. Kuanzia mwaka 1923 hadi 1941 alikuwa Ufilipino. Kwa miaka 10 ya mwisho alihudumu kama Rais wa Union ya Ufilipino. Alichukua madaraka ya kuwa Rais wa Divisheni ya Amerika ya Kusini ambapo pia alifanya kazi hiyo kwa miaka 9 iliyofuata. Mwaka 1950 alijiunga na maofisa wa makao makuu ya kanisa kama makamu wa Rais wa Jenero Konferensi na miaka 4 baadaye alichaguliwa kuwa Rais.

Katika wajibu wake kama Kiongozi wa Kiroho wa Washiriki Waadventista zaidi ya milion 1, Figulr alisafiri sana katika ulimwengu mzima akihutubia mikutano na kutoa mashauri kwa viongozi wa kanisa. Alizungumza lugha 3 zaidi ya Kiingereza ambazo ni pamoja na Kihispania, Kijerumani na Kitagalog.

ROBERT H. PIERSON June 16, 1966 – Januari 3, 1979. Alizaliwa Brocklyn, Iowa, Januari 3, 1911. alipata Elimu yake katika Southern Junior College (ambayo sasa inaitwa Southern Missionary). Baada ya kuhudumu kwa miaka 2 katika Konferensi ya Geirgia – Cumberland, aliitwa kwenda India na kuwekwa wakfu kama Mchungaji wa kanisa la Waaadventista wa Sabato katika Poona mwaka 1936. Mwaka 1966 alitunukiwa shahada yake ya juu ya Udaktari wa falsafa kutoka Chuo Kikuu cha Andrews.

Miaka 25 kati ya miaka yote aliyokuwa katika utumishi alitumia kufanya kazi katika nchi 6. Nyadhifa hizo zinajumuisha Mchungaji/Mkurugenzi wa shughuli za Walei/Konferensi na Urais wa Union kule India tangu mwaka 1935-1942 na baadaye kama Rais wa Union Konferensi za British West Indieas na Carribean. Jamaica na Trinidad 1944 – 1950. Rais wa Divisheni ya Kusini mwa Asia, 1950-1954, Rais wa Divisheni ya Trans-Africa, 1958 – 1966.

Nchini mwake alihudumu kama Rais wa Konferensi za Kentuky. Tennessee na Texas. Katika kipindi cha vita kuu ya pili alihudumu kama Mchungaji wa Kanisa la Takoma Park na baadaye aliendesha kipindi cha Radio katika Jiji la New York.

Mchungaji Pierson alikuwa anaendesha mikutano ya uamsho pamoja na kampeni za Uinjilisti katika nchi mbali mbali. Aliidhinisha vitabu 20 kando ya vijizuu na makala za magazetini. Mengi ya maandiko yake aliyatayarisha asubuhi mapema kabla ya saa za kazi.

NEAL C. WILSON Januari 3, 1979 alikuwa mtoto wa mmishonari. Aliishi Afrika na India na kupata elimu yake katika Shule ya Vincent Hil. Baadaye alihudumu katika Mashariki ya Kati tangu mwaka 1944 – 1958 ikiwa ni pamoja na Aden.

Alizaliwa Lodi, Calofinia July 5, 1920, na kuhitimu shahada yake ya Sanaa kutoka Pacific Union College mwaka 1942 na baadaye alipata masomo zaidi katika semina ya Thiolojia ya Kiadventista. Mchungaji Wilson alikuwa Mkurugenzi wa idara katika Konferensi ya Central Calofinia mwaka 1959 – 1960 na Union ya Columbia 1960 - 1962 na baadaye akawa Rais wa Union hiyo ya Columbia kwa miaka 4.

Mwaka 1966 alichaguliwa kuwa makamu wa Rais wa Jenero Konferensi katika Amerika ya kaskazini na kuendelea na kazi hiyo hadi alipochaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi katika Mkutano Mkuu wa mwaka 1978. Mtangulizi wake Mchungaji Pierson alistaafu rasmi Januari 3, 1979.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## MWAMKO MKUU KUHUSU MAREJEO 1975 – 19…….

Muhtasari wa historia ya kanisa kwa utaratibu wa mpangilio wa matukio kufuata miaka (mwaka baada ya mwaka)

Wale wote wanaojifunza historia ya kanisa kama sehemu yao ya kutimiza takwa katika Kozi ya Kiongozi Mkuu na Darasa la Msimamizi wanapaswa kuzingatia tarehe zote muhimu na kuzitia katika kumbukumbu zao.

Mwanzoni kabisa tulijifunza kuhusu kazi ya Mungu kwa ujumla na baadaye ikapanuka zaidi kiasi kwamba ikawa muhimu kuigwa historia hii katika awamu na sehemu mbali mbali ili tuweze kupata picha halisi ya sehemu na matukio yaliyotendeka. Japokuwa ni dhahiri kwamba kazi haikufanywa kwa awamu wala sehemu kama ilivyoonyeshwa, bali kama zege imara lililounganishwa pamoja. Ilianza kwa kuanzisha kazi katika majimbo machache na katika awamu nyingine maendeleo mpya ya kazi yalikuwa yameooneka. Kazi iliendelea taratibu hatimaye sasa ulimwengu mzima umezingirwa. Kadhalika mipango kamili na bora zaidi imetayarishwa ili kutoa huduma madhubuti na kuwaendeleza watendakazi.

**<u>SEHEMU YA 2: WACHUKUZI WA UJUMBE WA MAREJEO (1755 – 1843)</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 1755 | - | Tetemeko la Lisborn, Ureno |
| 1780 | - | Mei 19 jua lilipotiwa giza |
| 1793 | - | Zama za mwanzo wa Misheni za Uprotestanti wa Kisasa, Willian Carey akatweka kuelekea India |
| 1798 | - | Mwisho wa miaka 1260 ya Unabii |
| 1804 | - | Chama chama Biblia cha Uingereza na nchi za kigeni kiliundwa |
| 1807 | - | Mmishonari Robert Marriosn alitumwa kwenda China |
| 1813 | - | Adoniram Judson alipeleka Injili nchini Burma |
| 1816 | - | John Williams alitumwa kama Mmishonari kule Pacific ya Kusini |
| 1816 | - | Mtangulizi wa Wamishonari katika Afrika – Robert Moffat alikuja. |
| 1827 | - | Ellen Harmon (ambaye baadaye alijulikana kama Ellen G. White) alizaliwa karibu na Portland, Maine. |
| 1831 | - | William Miller alianza kuhubiri juu ya marejeo. Joseph Wolf na wenzake walikuwa wakihubiri ujumbe huo huo katika nchi zingine za mbali. |
| 1833 | - | Kuanguka kwa nyota |
| 1839 | - | Joshua V. Himes aliungana na Miller na kutoa wazo la kuhubiri katika miji mikubwa |
| 1840 | - | Himes alitoa jarida lake la mwanzo kuhusu marejeo – “Signs of the Times” mikutano ya makambi ilihudhuriwa naa maelfu ya watu. |

| | | |
|---|---|---|
| | - | Mikutano ya makambi ilihudhuriwa na maelfu ya watu |
| | - | David Livingstone alitweka kuelekea Cape Town kuanzisha kazi Afrika |
| 1842 | - | Charles Fitch alitayarisha Jedwali la Kiunabii<br>James White alianza kuhubiri ujumbe wa marejeo |
| 1843 | - | Waadventista walijiandaa kwa kuja kwa Kristo mara ya pili. Ujumbe kuhusu kilio cha usiku wa manane ulihubiriwa. |

**SEHEMU YA 3: MWANZO WA KANISA LA MASALIO (1844-1852)**

Hiki ni kipindi cha matengenezo wakati ambapo waumini walikatishwa tamaa, wale ambao walidhamiria kuwa wa kweli kwa Mungu kwa gharama yoyote walipoanza kufanya mipango ya kuhuisha matumaini ndani ya wale waliokuwa hawana tumaini na ambao walikuwa wametawanyika sehemu mbali mbali na kuwaeleza kisa juu ya mkasa ule wa kukatisha tamaa.

Wengi miongoni mwa waliokuwa wamerudi nyuma na kuugeukia ulimwengu walirejeshwa tena. Wengine walijiunga na makundi ya waumini waaminifu ambaohawakuwa na uongozi maalum. Taratibu mipango ilifanywa ya kuyakabili mahitaji yaliyotokana na kukua kwao. Sehemu mbalimbali ziliendelea kuundika kama ilivyokuwa, hatimaye muunganiko wenye nguvu ulifikiwa baadaye.

| | | |
|---|---|---|
| 1844 | - | Hali ya kukatisha tama kuu |
| | - | Ukweli kuhusu Sabato ulibadilishwa na Kanisa la kwanza la Waadventista wa Sabato liliundwa kule Washington, New Hamphshire |
| | - | Nuru ya hekalu |
| | - | Hiram Edson alitembea katika shamba lile la nafaka. Karama ya Roho ya Unabii ilitolewa kwa kanisa la masalio |
| | - | Ujumbe wa kwanza kwa uma ulitumwa kwa simu ya maandishi, ulitumwa na F.B. Morse – "Kile ambacho<br>Mungu alikifanya". |
| 1845 | - | Joseph Bates, J.N. Andrews na wenzao walipokea ujumbe kuhusu Sabato |
| 1846 | - | Familia ya White iliyakubali mafundisho kuhusu Sabato |
| 1847 | - | Njozi kuhusu Sabato alionyeshwa Ellen White ikiwa ni miezi (7) tangu familia hii ianze kutunza na kufundisha<br>juu ya Sabato. |
| 1848 | - | Mkutano wa kawaida wa kwanza wa watu wenye kuitumza Sabato mikutano 6 kuhusu Sabato |
| | - | Ellen White alipata njozi iliyomwagiza mumewe James White kuanza kuchapa kijizuu |
| 1849 | - | Gazeti la kwanza lilichapishwa: "The present Truth" |
| | - | Huu pia ndiyo ulikuwa mwanzo wa Historia ya Chama cha Uchapaji –<br>The Review and Herald Publishing Association |
| 1850 | - | Toleo la kwanza la Adventist Review na Sabbath Herald lilichapishwa |
| 1852 | - | Kitabu cha Youth's Instructor kilichapishwa kwa mara ya kwanza |
| | - | Mtambo wa kwanza wa uchapaji wa Waadventista ulinunuliwa |
| | - | Lessoni ya kwanza ya Shule ya Sabato ilitayarishwa na James White |

**<u>SEHEMU YA 4: KUUNDWA KWA KANISA LA MASALIO (1853 – 1863)</u>**

Baada ya kuongezeka kwa idadi ya washiriki, hitaji la kuwa na chombo cha kuwaunganisha lilijitokeza na hitaji hilo liliwezesha mipango kutayarishwa. Miaka 10 baada ya ule mkasa wa

kukatisha tamaa chombo kiliundwa, baada ya jambo hilo kuwekwa katika maombi na watangulizi hao na Mungu kujibu maombi hayo.

1853 - Vitambulisho vilianza kutolewa kwa Wachungaji
- Shule ya Sabato ya kawaida ilianzishwa (Rochester, New York)
- Uriah Smith alijiunga na ofisi ya Uhariri wa Review and Herald
- Shule ya kwanza ya Kanisa la Waadventista Wasabato Buck's Bridge, New York, na Martha Byington akiwa ndiye mwalimu wake.

1854 - Mkutano wa makambi wa kwanza ulifanyika katika hema ukiendeshwa na J.N. Loughborough na M.G. Cornell

1855 - Makao Makuu ya kanisa yalihamishwa toka Rochester kwenda Battle Creek, Michigan.

1859 - Mpango wa "Utoaji kwa Mpango" ulianza kutumiwa

1860 - Jina "Seventh-Day Adventist" lilianza kutumiwa rasmi

1861 - Konferensi ya kwanza iliundwa kule Michigan
- Ushuhuda wa kwanza kuhusu Afya na Kiasi ulitolewa
- Hatua za mwanzo za matengenezo kwa upande wa Afya zilifanyika

## <u>SEHEMU YA 5: KUPANUKA NA MATENGENEZO (1864 -1873)</u>

Hali ya Kanisa la Waadventista Wasabato katika muda mfupi lilianza kudhoofika.

Wamishonari walitumwa kwenda Califonia kupitia katika lango la Panama, kwa sababu ya ukweli kwamba hakukuwa na usafiri wa reli kuunganisha mabara mbali mbali hadi ilipofika mwaka 1869. Watendakazi hao pia walikuwa wakiendeleza kazi katika majimbo ya Kusini.

1864 - Waadventista walipewa hadhi ya kutohusika katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Wamarekani.

1866 - Kituo cha kwanza cha Afya kilianzishwa kule Battle Creek

1868 - Watendakazi wa kwanza walipelekwa Califonia
- Mkutano wa makambi wa kwanza ulifanyika (Wright, Michigan)

1869 - Kijizuu cha kwanza pamoja na chama cha Wamishonari vilianzishwa. James Erzeberger alikwenda Marekani kusihi juu ya mmishonari kupelekwa Ulaya.

1872 - Joseph Bate alifariki (ambaye alizaliwa mwaka 1792)
- Advent Tidende – Jarida la kidenishi lilichapishwa

Shule ya kwanza rasmi ya Kanisa la Waadventista Wasabato (ambayo baadaye ingekua na kuwa chuo cha kwanza) ilianzishwa kule Battle Creek chini ya Goodloe H. Bell.

## SEHEMU YA 6: NJOZI KWA AJILI YA ULIMWENGU MZIMA (1874 – 1878)

Ni katika kipindi hiki ambapo tumeona kazi ikianza katika nchi mbali mbali za Ulaya.
Katika Ulaya na Marekani ilihusisha lugha saba badala ya moja iliyokuwa ikitumika

1874 - Mmishonari wetu wa kwanza katika nchi za Kigeni J.N. Andrews alikwenda Switzerland.
- Chuo cha Battle Creek kilifunguliwa
- Gazeti la "Signs of the Times" lilichapwa

1875 - Chama cha uchapaji cha Pacific Press kilianzishwa

1876 - Kwa mara ya kwanza Ufaransa ilipata ujumbe wa malaika wa tatu
- Gazeti letu la kwanza kule Ulaya lilichapishwa kule Switzerland lililoitwa "Les Signes des Temps"
- Kanisa la kwanza la Waadventista wa Sabato lilianzishwa katika Ujerumani

1877 - J.G. Matteson alikuwa ndiye Mmishonari wa kwanza kule Scandnavia.
- Chama cha kwanza cha Shule ya Sabato kilianzishwa kule Califonia
1878 - Kanisa la kwanza lilianzishwa kule Scandnavia
- Mkutano wa makambi wa kwanza ambapo Shule ya Sabato iliendeshwa
- Sadaka ya kwanza ya Shule ya Sabato ilitolewa
- Shule ya Sabato iliundwa
- William Ings na J.N. Loughborough walitumwa kwenda Uingereza.

## SEHEMU YA 7: MAENDELEO MUHIMU PAMOJA NA MAPUNGUFU (1879 – 1904)

Ujumbe wa malaika watatu kwa mara ya kwanza ulihubiriwa Marekani ya Kaskazini na baadaye kule Ulaya. Mnamo mwaka 1885 kundi la watendakazi lilitweka kuelekea Australia na matokeo yake mwishoni mwa karne, watendakazi walikuwa wameingia hadi Afrika, India, Marekani ya Kusini, maeneo kuzunguka Ghuba ya Mexico, China hadi katika Visiwa vya Bahari ya Kusini.

Kazi sasa ilitendwa kwa kutumia lugha 22 ukilinganisha na zile 7 za awali. Kwa hakika kazi ya Wamishonari wetu wakuu katika nchi za kigeni ilikuwa ikienda kwisha.

Kufikia mwaka 1904 idadi ya washiriki ilikuwa imefikia 71,891 ambao kati yao 16,476 walikuwa nje ya Marekani ya Kaskazini. Katika kila nchi, watendakazi walikuwa wakirefusha kamba zao na kuziimarisha. Katika miaka ya 1900 hadi 1904, Wamishonari wapya 207 walitumwa kwenda kutoa huduma katika nchi za kigeni. Kwa sababu ya ukuaji wa kazi wa haraka, umuhimu ulijitokeza wa kubadilisha kwa namna fulani na sera za kanisa. Union Konferensi zilianzishwa na mabadiliko mengi yalifanywa ili kugawa majukumu na kuwezesha kupanuka zaidi kwa kazi, chini ya usimamizi wa moja kwa moja na ulio karibu zaidi.

1879 - Mkutano wa kwanza wa vijana (uliowahusisha vijana wa kiume tu) ulifanyika Hezelton, Michigan chini ya Harry Fenner na Luther Warren.
1880 - Ubatizo wa kwanza ulifanyika Uingereza
- Konferensi ya kwanza nje ya Marekani ya Kaskazini ilianzishwa Denmark
1881 - Kazi ya Uinjilisti wa vitabu ilianzishwa
- Kitabu cha kwanza katika mfululizo wa matoleo kiliuzwa na George A. King
- Kufa kwa mtumishi wa Mungu James White
1882 - Chama cha Kimataifa cha vijizuu kiliundwa
1883 - Mtumishi wa Mungu J.N. Andrews alikufa
- Darasa la kusomesha wauguzi lilianzishwa katika kituo cha Afya cha Battle Creek.
1885 - Mkutano wa kwanza kuzungumzia juu ya utoaji wa sadaka yote ya Shule ya Sabato kwenda Misheni ulifanywa
- Wamishonari wa kwanza walitumwa Australia
- Ellen White alifanya ziara Ulaya na Uingereza
1886 - Kazi ilianzishwa katika Patcairn
- Kazi ya kudumu ilianzishwa katika New Zealand
- Kanisa la kwanza lilianzishwa Barani Asia(Russia)
- Barua ya "Mwito wa Makedonia" kutoka Afrika ya Kusini ilisomwa katika Mkutano wa Jenero Konferensi
1887 - Wamishonari wa kwanza kuja Afrika walifika Cape Town mwezi Julai
- Mkutano wa makambi wa kwanza barani Ulaya ulifanyika kule Norway
- Kazi ya uinjilisti wa vitabu ilianza katika British Guinea
- Ellen White alirejea Marekani

1888 - Abraham La Rue alikwenda Hongkong na Uchina kama Mmishonari wa kujitegemea
- Mkutano wa kihistoria wa Jenero Konferensi ulifanyika Minneapolis, Minnesota.
1889 - Chama cha Kitaifa cha kutetea Uhuru wa Dini kilianzishwa
- Mmishonari wa kwanza alitumwa Uturuki
- Kazi ilianzishwa Barbados, East-Indes
- Chama cha Kimataifa cha vijizuu kikaanzishwa katika Hamburg, Ujerumani
1890 - Meli ya kwanza ya kimishonari ya Pitcain iliundwa
1891 - Ellen White aliondoka na kwenda kuishi Australia kwa miaka 9 (ikijumuisha miezi kadhaa aliyoishi New Zealand)
- Kazi ya kudumu ilisimikwa katika Marekani ya Kati
- Kazi ilianzishwa Mexico
1892 - Ushuhuda wa Kwanza kuwaita vijana kwa kazi maalumu ulitolewa
- Kazi ilianzishwa katika Finland na Brazil
- Konferensi ya Cape iliundwa
- Kuchapishwa kwa South Africa Sentinel
- Kazi ya elimu ikaanzishwa katika Australia
- Kitabu cha Njia Salama "Steps to Christ" kilichapishwa
- Kazi ilianzishwa kule Jamaica
1893 - Chuo cha kwanza kilianzishwa nje ya Marekani ya Kaskazini, kilichojulikana kama Claremont Union College (ambacho sasa kinajulikana kama Helderberg), Cape Town
- George James aliwasili Malawi
- Wainjilisti wa vitabu waliingia India
- Kazi ilianzishwa katika Trinidad
- Wainjilisti wa vitabu waliingia katika visiwa vya Falkland
1894 - Kazi ilianzishwa katika Chile
- Mkutano wa kwanza wa makambi ulifanyika katika Australia na vile vile Union Konferensi iliundwa
1895 - Misheni kwa ajili ya wasio wakristo ilifunguliwa katika Afrika-Solusi, Rhodesia
- Misheni ya kwanza ilianzishwa kule India – Calcuta
1896 - Shughuli za Afya zilianzishwa Australia
- Mmishonari wa kwanza alitumwa kwenda Japan
1897 - Kazi ilianzishwa Belgium
- Mmishonari wa kwanza alipelekwa Iceland
- Shule ya Avondale ilifunguliwa Cooranbong kule Australia
- Kituo cha Afya cha Claramont kilifunguliwa kule Cape Town.
1898 - Mahubiri ya kwanza ya Wamishonari yalifanyika kule Peru.
- Kitabu cha "The Desire of Ages" kilichapishwa
- Kituo cha Afya cha Skodsborg kilifunguliwa kule Denmark
- Watendakazi wa kwanza wa Kiadventista walifika Hungary
1900 - Kazi ilianzishwa katika Sumatra na pia katika Visiwa vya Virgin, British West Indes
1901 - Shughuli za vijana ziliunganishwa na zile za Idara ya Shule ya Sabato
- Kanisa la kwanza la Waadventista wa Sabato lilianzishwa katika Scotland, kadhalika na kazi ilianzishwa katika Puerto Rico.
- A.G. Daniells alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi
- Southern Publishing Association kikajumuishwa
- Kazi ya kanisa ilipangwa upya

1902 - Kituo cha Afya cha Battle Creek pamoja na nyumba ya uchapaji ya gazeti la Review and Herald viliungua moto.
- South African Conference ikafanywa kuwa Union Konferensi
- Misheni ya Malamulo ikaanzishwa kule Malawi
- Mtendakazi wa kwanza alitumwa Uchina

1903 - Makao Makuu ya Kanisa yalihamishiwa Washington D.C.
- Watendakazi wa kwanza walituma Hispania na Tanzania
- Misheni ya Panama ilianzishwa.

1904 - Kazi kwa mpango wa kudumu ilianzishwa Romania
- Kazi ilianzishwa katika Ureno
- Wainjilisti wa vitabu waliingia Ecuador
- Mkorea wa kwanza kuongoka (katika Japan)

**SEHEMU YA 8: KUKUA NA KUPANUKA KWA INJILI (1905 – 1923)**

Mwaka 1910, idadi ya washiriki wetu ilikuwa imefikia 66,294 katika sehemu ya Marekani ya Kaskazini na 38,323 kutoka pande nyingine za ulimwengu. Kwa kipindi cha kati ya mwaka 1905 hadi 1914, watendakazi 960 walitumwa kwenda katika nchi mbali mbali za kigeni ikiwa ni wastani wa watendakazi 96 kila mwaka na 2 kwa kila juma. Nyumbani na katika nchi za mbali, jeshi linalokua lilikuwa likisonga mbele kila mwaka katika kazi ya Umishonari.

1905 - Mwinjilisti wa vitabu ambaye pia ni mwananchi wa Australia R.A. Caldwell alianzisha kazi katika Ufilipino.
- W.H. Anderson alifungua kazi katika Stesheni ya Misheni ya Pemba (Misheni ya Rusangu)
- Mmishonari mkazi wa kwanza alitumwa Korea (Chosen)
- Mwinjilisti wa kwanza alikwenda Haiti
- Kanisa la kwanza lilianzishwa katika Cuba
- Kuanzishwa kwa Misheni ya Peru
- Kuanzishwa kwa idara ya Mambo ya Nchi za Kigeni (North American Missions Committee).

1906 - Ofisi za kuchapisha gazeti la Ukweli wa Leo "The Present Truth" zilihamishiwa Buenos Aires, Argentina.
- Shule na Zahanati vilianzishwa kule Hunan, China.
- Mmishonari wa kwanza wa Kiadventista aliingia Kenya.
- Misheni ya Uruguay ilianzishwa

1907 - Idara ya vijana (MV – Missionary Volunteers) iliundwa
- Shule ya Wavulana ya Kanisa ilifunguliwa kule Korea

1908 - Kalenda ya kasha la asubuhi kwa lugha ya Kiingereza ilichapishwa
- Injili iliingia katika Papua New Guinea
- Mpango wa mavuno ulipitishwa na Jenero Konferensi ili utendeke katika makanisa yote.

1909 - Chama cha vijana wadogo (JMV) kilianzishwa
- Misheni ya maranatha (Bethel College) ilifunguliwa katika Kaffirland
- Waongofu wapya wa kwanza waliojulikana walibatizwa huko Ugiriki
- Taasisi ya masomo ya nyumbani ilianzishwa

1910 - Mtendakazi wa kwanza wa kudumu katika Venezuela alifika
- Shule ya Sekondary ya Inyazura ilizinduliwa huko Rhodesia (Zimbabwe)
- Chuo cha Uinjilisti kwa Njia ya uganga kilianzishwa

1911 - Mkutano wa Mahema ulifanyika Mt. Carmel katika Palestina

1912 - Waongofu wa kwanza katika Bolivia

- Misheni mpya ya Hebrides ilianzishwa
- Idara ya Mawasiliao ilianzishwa (Press Bureau)

1913 - Ellen White alituma ujumbe wake wa mwisho katika mkutano wa Jenero Konferensi
- Sadaka zote za kawaida za Shule ya Sabato zikaanza kupelekwa Misheni.

1914 - Union Misheni ya Inca iliundwa
- Waongofu wa kwanza walipatika Borneo
- Watendakazi waliingia Manchuria, China

1915 - Kifo cha Ellen White

1918 - Tawi la huduma ya nyumbani nalo likafanywa kuwa moja ya Idara ya Jenero Konferensi

1919 - Zahanati ilifunguliwa katika mpaka kati ya China na Tibet

1921 - Misheni ya Gitwe na Songa pamoja na Hospitali ya Kenya vilianzishwa katika Afrika
- Shule ya Mafunzo ilifunguliwa katika Haita
- Shule nyingine ya mafunzo ikafunguliwa katika ukanda wa Panama.

1922 - Hekalu la Battle Creek liliungua moto
- W.A. Spicer akachaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi
- S.N. Haskell Alikufa
- Madarasa kwa ajili ya madarasa ya vijana wadogo (JMV) yalianzishwa

1923 - J.O. Carlis alikufa
- Kitabu “Testimonies to Ministers kilichapishwa

SEHEMU YA 9: MAFANIKIO DHIDI YA VIKWAZO (1924-1946)

Pamoja na vikwazo vya hali ya juu hususani ile miaka ya kudorora kwa kazi pamoja na vita kuu ya pili ya dunia, lakini bado yalikuwepo mavuno makubwa. Mbegu zilizoliwa zimepandwa na waanzilishi zilizaa matunda kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu.

Kipindi cha miaka 10 kati ya 1931 – 1941, kilikuwa ni hatua nyingine kubwa katika maendeleo ya historia ya Kanisa. Kilishuhudia zama zilizotawaliwa na kiwango cha hali ya juu ya umoja wa maendeleo.

1924 - Kufa kwa J.N. Loughborough ambaye alikuwa kiunganishi baina ya zana za waanzilishi na siku zilizofuata.

1925 - Union ya Congo (Zaire) ilianzishwa
- Kuanzishwa kwa Union ya Afrika Mashariki na Kusini

1926 - Kambi ya kwanza la vijana lilifanyika Michigan
- Nyumba ya Uchapaji ya Malamulo ulianzishwa kule Malawi (Malamulo Publishing House)

1927 - Hospitali ya Mwami ilianzishwa nchini Zambia

1930 - C.H. Watson alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi

1931 - Kuanzishwa kwa umishonari kulikamilika kaka Amazon
- Misingi ya Imani ya Kanisa letu ilitayarishwa

1932 - Kanuni ya kanisa ya kwanza rasmi ilichapishwa

1934 - Hospitali ya Haile Selassi ilikamilika kule Ethiopia

1936 - Ndege Ulaya ya kwanza kutoa huduma katika Pacific (Trans-Pacific Air Plane Service)
- J.L. McElhany alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi

1937 - Seminari ya kwanza ya Kitheolojia ilianzishwa
- Makao Makuu ya Divisheni ya mashariki ya mbali yalihamishiwa Singapore.

1939 - Chuo cha Mashariki ya kati kilianzishwa kule Beirut
- Jarida la Elimu ya Waadventista (Journal of Adventist Education) lilichapishwa kwa mara ya kwanza.

1941 - Sauti ya Unabii ilitambuliwa na Jenero Konferensi, ya Kanisa la Wasabato kama mradi wa Kanisa.
- Janauari 4, 1942, Matangazo ya radio yalisikika katika nchi nzima kwa mara ya kwanza

1944 - Kitabu cha Uriah Smith "Thoughts on Daniel and Revelation" kilifanyiwa mapitio na kuchapishwa

1946 - Kitabu cha "Evangelism cha Ellen White kiliungwa pamoja na kutolewa

SEHEMU YA 10: KUKUA NA MSHIKAMANO (1947 – 1959)

Baada ya vita Kuu ya Pili ya dunia, Kanisa lilikabiliwa na kazi ya kuyafanyia ukarabati na kujenga upya baadhi ya majengo. Vita ilikuwa imebadilisha kabisa hali ya mwonekano wa mengi ya mabara. Kazi za Misheni zilipewa kipaumbele na hivyo kupanuka kwa kazi kulishuhudiwa kila mahali ambapo kazi ya Kanisa ilikuwa ikifanywa katika kipindi hiki.

1947 - Kuundwa chama cha Kiasi cha Kimataifa
- Mkutano wa vijana wa kwanza katika Divisheni ya Amerika ya Kaskazini, San Fransisco

1948 - Chuo cha Waadventista cha Bugema kilichopo nchini Uganda kilianzishwa.

1949 - Hospitali ilifunguliwa kule Pakistani.

1950 - Kipindi cha kwanza cha Televisheni cha "Faith for Today" kilirushwa hewani huko New York.
- Chama cha Watafuta Njia kilitambuliwa na kuwa sehemu ya Jenero Konferensi
- W.H. Branson alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi.

1951 - Kituo cha Yatima (Sung Yuk Won) kilifunguliwa kule Korea.
- Hospitali ya Misheni ya Maluti ilifunguliwa Lesotho
- Kitengo cha Chama cha Vijana (MV) kilianza kazi ya uchapaji

1952 - Kuanzishwa kwa Shule ya Biblia ya "Faith for Today"

1953 - Kituo cha kudumu cha Uinjilisti kilinunuliwa kule London
- SDA Bible Commentary zilitolewa 1953-1957
- Mkutano wa chama cha Vijana wa Kimarekani ulifanyika San Francisco.
- Toleo la kwanza la mwongozo wa Kiongozi (Guide) ambao awali ulijulikana kama (Junior Guide)

1954 - Kitabu cha "Prophetic Faith of our Fathers" kilitolewa
- R.R. Figuhr alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi

1955 - Shule ya Sabato ilifikia matoleo ya kiwango cha Dola milioni 6.
- Masomo ya "Imeandikwa" "It is Written" yalianza kupelekwa kwa simu ya maandishi.
- Kazi ya uganga na Upasuaji ilianza katika hospitali ya Yuka, Zambia.
- Chama cha Maandiko ya Kiebrania (Isralite Heritage Instite) kiliundwa

1956 - Mpango wa Uinjilisti wa Vijana (MV) wa Sauti ya vijana ulitambuliwa na kuwa sehemu ya mipango ya Jenero Konferensi.

1957 - Kituo cha Uinjilisti cha New York kilianzishwa.
- Chuo Kikuu cha Potomac kilianzishwa
- Kitabu cha "Questions on Doctrine" kilichapishwa

1959 - Kituo cha Sunnyside kilifunguliwa kwa ajili ya Wazee kule Plumstead, Cape

Town.
- Idadi ya Washiriki ulimwenguni kote ilifikia 1,194,070.
- Mwanafunzi wa kwanza Mmishonari (Marlin Matiesen) alitoka Chuo cha Columbia kwenda Mexico.

**SEHEMU YA II: KUMALIZA KAZI YA INJILI (1960…)**

Wakati umekwisha, karibu miaka 6000 imepita na ujumbe wa Malaika wa tatu umehubiriwa kwa zaidi ya kipindi cha miaka 130. Ni wakati ambapo Bwana atakuja na watu wake wanahisia ukaribu wake.

Katika miaka hii ya mwisho, umeshuhudiwa uamsho na mkazo mpya juu ya Uinjilisti.

1960 - Union ya Afrika ya Kati iliundwa upya.
- Chuo Kikuu cha Andrews kikachukua nafasi ya Chuo Kikuu cha Potomac.
- Sherehe ya Maandiko Mataikatifu zilifanyika katika mji wa Atlantic

1961 - Chuo cha uinjilisti kwa njia ya Uganga kikaitwa Chuo Kikuu cha Loma Linda

1962 - Mpango wa siku tano wa kuzuia Uvutaji uliamshwa

1965 - Chuo cha Waadventista cha Kivu kilianzishwa

1966 - R.H. Pierson alichaguliwa kuwa Rais wa Jenero Konferensi

1967 - Kuanzishwa kwa Idara ya Uwakili na Maendeleo

1968 - Idara ya Huduma ya udhamini na chakula duniani ilianzishwa

1969 - Kongres ya vijana iliyofanyika Zurich, Switzerland

1970 - Mkutano Mkuu wa 51 wa Jenero Konferensi ulifanyika Atlantic City, New Jersey
- Washiriki wa Kanisa waliobatizwa walizidi idadi ya milioni 2
- Kulikuwa na Makanisa 16,505 katika ulimwengu mzima
- Toleo la kwanza la gazeti la "Insight" (ambalo lilichukua nafasi ya "Youth's Instructor")

1972 - Uinjilisti wa Ulimwengu mzima uliojulikana kama ujumbe wa 72 (Ujumbe wa 73, Ujumbe wa 74)
- Kuanzishwa kwa mradi wa Kasai (Zaire)

1973 - Idara ya Radio. Televisheni na Uhusiano ziliungana na kuzaa Idara ya Mawasiliano.
- Mpango wa kazi maalumu kwa Vijana wa Kiadventista ulianzishwa

1975 - Mkutano mkuu wa 52 wa Jenero Konferensi ulifanyika Vienna, Austria
- Semina ya kwanza huduma kwa vijana wa Kiadventista ilifanyika katika Chuo Kikuu cha Andrews.

1977 - Mkutano Mkuu wa mwaka ulioweka mkakati wa kumaliza kazi ulifanyika .
- Mkakati wa kubatiza watu 1000 kwa siku moja katika mwaka 1980.
- "Youth Ministry Accent" lilichapishwa kwa mara ya kwanza (badala ya (MV Kit).

1978 - Sherehe za mwanzo za Imani zilifanyika katika Amerika ya kaskazini
- Jina "Missionary Volunteers" (MV) lilibadilishwa na kuwa "Adventist Youth".

1979 - Neal C. Wilson akashika madaraka kama Rais mpya aliyechaguliwa na Jenero Konferensi.
- C.E. Bradford akachaguliwa kuwa Makamu wa Rais katika Divisheni ya Amerika ya Kaskazini

1980 - Mkutano Mkuu wa Jenero Konferensi ulifanyika Dallas, Texas April 17-26

**Zingatia:**

Katika mkutano wa Jenero Konferensi wa mwaka 1980, Divisheni mpya ilianzishwa ili kuhudumia maalumu nchi za Kiafrika zenye kutumia lugha ya Kifaransa pamoja na visiwa vinavyozunguka. Divisheni hii ilipewa jina la Divisheni ya Afrika - Bahari ya Hindi (Africa-Indian Ocean Division). Kufuatia mgawanyo mpya wa maeneo katika Afrika Northern Europe-West Africa Division lilibadilishwa jina na kuitwa European Division.

Idara zifuatazo za Jenero Konferensi ziliunganishwa kwa msingi wa majaribio katika miaka ya 1980 - 1985 kwa miaka mitano.

- Idara ya Afya na Kiasi
- Idara ya Huduma na Uwakili/Maendeleo